**9 APRILI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Pili – Tarehe 9 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. HUSSEIN H. AMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. RASHID ABDALLAH RASHID K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti wa UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. TAMIMA HAJI ABBAS K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Chege.

Na 16

**Ujenzi wa Stendi Wilaya ya Rorya**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa ujenzi wa Stendi Wilayani Rorya ili kuongeza mapato ya halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Wananchi wa Rorya kuwa na Stendi ya Mabasi kwa lengo la kuongeza mapato ya halmashauri na kuboresha huduma za usafiri kwa wananchi. Kwa sababu hiyo, Serikali kupitia halmashauri imetenga eneo la ardhi lenye ukubwa wa ekari 10 katika Kijiji cha Mika na Nyasoko kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, Halmashauri kupitia mapato ya ndani imetumia shilingi milioni 98 kujenga stendi ya muda katika Kijiji cha Mika ili kuwezesha wananchi kupata huduma ya stendi na kuongeza mapato ya Halmashauri ya Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri imefanya mazungumzo ya awali na Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)* chini ya Wizara ya Fedha ili kuweza kutekeleza mradi huo wa kimkakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili katika hili swali namba 16.

Swali la kwanza; Stendi ya Rorya imekuwa na ahadi ya muda mrefu sana, hata Mbunge aliyepita alikuwa na hoja hii hii

ya stendi ya Rorya. Je, ni lini sasa Serikali itatizimiza ahadi hiyo ya kuwajengea wananchi wa Rorya stendi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kijiji cha Nyamuswa, Kata ya Nyamuswa katika Jimbo la Bunda wamejenga Stendi kwa nguvu zao binafsi. Je, ni lini Serikali itawa-*support* wananchi katika Stendi hiyo ya Mji wa Nyamuswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hitaji la Stendi ya Mabasi ya Kisasa katika Halmashauri ya Rorya ni ya muda mrefu. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua; kwanza tuliielekeza halmashauri kutenga eneo lenye ukubwa unaostahili ambapo wamekwishapata eneo la ekari 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tayari Serikali imeshapeleka fedha milioni 98 na kujenga stendi ya mabasi kwa hatua za awali. Vilevile, katika mwaka ujao wa fedha tunawasiliana na kufanya mazungumzo na sekta ya mashirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuanza ujenzi huu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali imeshaweka mipango thabiti kwa ajili ya kwenda kujenga kituo cha mabasi pale Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na Stendi ya Nyamuswa, kwanza niwapongeze Wananchi na Serikali ya Kijiji cha Nyamuswa kwa kufanya jitihada za kujenga stendi hiyo. Pia, nimhakikishie kwamba Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri au fedha za Serikali Kuu tutakwenda kuunga mkono ujenzi wa stendi hiyo ili uweze kuwa bora zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jiji la Arusha liliingia kwenye Mradi wa *TACTIC* toka mwaka 2023 na Januari, 2024 ilitangazwa tenda kwa ajili ya kujenga Stendi ya kisasa Jiji la Arusha. Hata hivyo, mpaka leo ni mwaka

mmoja na miezi mitatu bado mkandarasi hajaenda *site*. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga stendi Jiji la Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kupitia Mpango wa *TACTIC* iliainisha Ujenzi wa stendi ya mabasi katika eneo la Bondeni *City* katika Jiji la Arusha na tayari taratibu za manunuzi zimekwishafanyika na ziko katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Mheshimiwa Mrisho Gambo amefuatilia kwa karibu sana suala la ujenzi wa stendi pale Bondeni *City*. Ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wote wa Jiji la Arusha, kwamba, Serikali wakati wowote kuanzia sasa itaanza ujenzi wa stendi pale Bondeni *City*. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi ya Kahama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishaweka Mpango wa kuainisha maeneo yanayohitaji stendi. Pia, katika Miji, Majiji na Manispaa, tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuainisha maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa stendi na kuandaa fedha za mapato ya ndani au kuandika miradi ya kimkakati na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, kuandaa andiko hilo na

kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini pia kuanza kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa stendi hizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Juliana Shonza.

Na 17

**Hitaji la Kituo cha Afya Kata ya Luswisi**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Luswisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 jumla ya vituo vya afya 367 vimejengwa na vinatoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Luswisi ipo umbali wa takribani kilometa tano kutoka Kituo cha Afya cha Lubanda na idadi ya wananchi wapatao 4,155 kati ya angalau 10,000 wanaohitajika kwa mujibu wa vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendeea kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini zikiwemo kata zitakazokidhi vigezo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wananchi wa Kata ya Kalembo wameanzisha ujenzi wa Kituo cha Afya, ninaomba kufahamu ni

lini Serikali itapeleka hizo fedha ili kuweza kumalizia hicho kituo cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Kata ya Malangali na Kata ya Kafule hazina Vituo vya Afya, ninaomba kufahamu ni lini Serikali itapeleka fedha ili vituo hivyo vya afya viweze kujengwa na akinamama wa kata hizo waweze kuondokana na changamoto ya afya? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa kata hiyo ambayo Mheshimiwa Juliana Shonza ameitaja ambao wameanza kwa nguvu zao kujenga kituo cha afya. Niwahakikishie kabisa kwamba dhamira ya Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na tutahakikisha tunatafuta fedha aidha kupitia mapato ya ndani ya halmsahauri au kupitia Serikali Kuu kwenda kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na kata hizo mbili ambazo hazina vituo vya afya, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na halmashauri hizo ili kuweza kuona kama kata hizo zinakidhi vigezo kwa maana ya idadi ya wananchi na umbali kutoka kituo cha jirani zaidi, lakini pia hali ya kijiografia na ikiwa inakidhi vigezo tutaziweka katika mpango wa ujenzi kwa awamu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Kyela iliyopo kwenye Mkoa wa Mbeya ina Vituo vya Afya vinne ambavyo havijamaliziwa ujenzi wake, viko kwenye Kata ya Itope, Njisi, Ngonga na Makwale. Je, ni lini sasa Serikali italeta fedha za kumalizia ujenzi wa vituo hivyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyouliza Mheshimiwa Suma Fyandomo, kwamba Vituo vya Afya katika Kata hizo za Njisi, Itope, Makwale na Ngonga vilianza na ujenzi na Serikali ilishapeleka fedha na tunafahamu kwamba vimejengwa kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, ujenzi wa vituo vyetu vya afya tunakwenda kwa awamu. Tuna awamu ya kwanza ya majengo yale matano ya kwanza, lakini tutakwenda awamu ya pili kwa ajili ya majengo yote yanayosalia. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge pamoja na wananchi wa Kyela, kwamba, vituo hivyo vya afya vitawekwa kwenye mpango kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Laini, Wilaya ya Itilima ina wakazi wengi na haina kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Laini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuandaa mpango mkakati wa ujenzi wa vituo vya afya katika kata zote za kimkakati, tulipitia halmashauri zote 184 ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Itilima. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutakwenda kutenga bajeti kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya ikiwa kinakidhi ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa mwongozo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ilitoa shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya

Myangayanga. Ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Kituo hicho kinakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Jonas, katika Jimbo la Mbinga Mjini tulishatoa fedha milioni 250, kwa ajili ya kituo hicho cha afya na tutapeleka milioni 250 nyingine katika mwaka ujao wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya kukamilisha majengo yaliyosalia. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, jiandae Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha *OPD* Himo, kilipandishwa hadhi ya kuwa kituo cha afya mwaka 2020 na kuahidiwa majengo ya *mortuary*, upasuaji na maabara. Mpaka leo kituo hicho kinatoa huduma kama kituo cha afya lakini majengo hayo hayajapatikana. Je, ni lini majengo hayo yatapatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei amefuatilia mara kadhaa na ameuliza mara kadhaa hapa Bungeni na Serikali tulimjibu na kumhakikishia kwamba tumekwishaingiza kwenye mpango wa Benki ya Dunia ili kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo kwenye kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tuko kwenye hatua za mwisho sana na tumeshapeleka orodha hiyo Wizara ya Fedha na wenzetu wa Wizara ya Fedha wakati wowote watatoa fedha hizo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo hayo katika kituo hicho cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, jiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Bugarama kilichopo Jimbo la Geita kililetewa milioni 475 za tozo na bajeti ilikuwa milioni 600, *balance* milioni 125. Ninataka kujua, je, ni lini milioni 125 italetwa ili kiweze kukamilika na kuanza kazi? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Bugarama, katika Halmashauri ya Geita Vijijini kimewekwa kwenye bajeti ya 2025/2026 na nimhakikishie Mheshimiwa Musukuma kwamba fedha hiyo itapelekwa na tutakamilisha majengo hayo yaliyobakia kwa maana ya milioni 125.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Ipogolo na Kituo cha Afya Ngome ni vituo vya zamani sana. Ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kujenga *combined Maternity ward?* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, viko vituo vya afya ambavyo ni vikongwe na chakavu vikiwemo vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja vya Ipogolo na Ngome. Hata hivyo, kwanza tuliweka mpango wa ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 91, tumeshakarabati 50 kwa maana ya kipaumbele cha kwanza na baada ya hapo tutakwenda kwenye kipaumbele cha vituo vya afya. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mbunge, kwamba, kwa sababu tayari tumeshaainisha vituo vya afya takribani 252 vikiwemo hivyo kwa ajili ya ukarabati na tutafanya ukarabati huo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Dkt. Florence kwa niaba yake Mheshimiwa Felix.

Na 18

**Ujenzi wa Mabweni Sekondari za Muhambwe**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, lini Mabweni ya Sekondari ya Busagara na Kumgogo – Muhambwe yatajengwa ili kuanza kidato cha tano na sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023/2024 Serikali ilipeleka shilingi milioni 680 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika Shule za Sekondari Busagara (mabweni matatu) na Kumgogo (mabweni mawili).

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari Busagara na Kumgogo zimeanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 2024 ambapo Shule ya Sekondari Busagara ilipangiwa wanafunzi 88 na Shule ya Sekondari Kumgogo ilipangiwa wanafunzi 93.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya shule za sekondari zikiwemo Shule za Busagara na Kumgogo kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza nipongeze na kushukuru. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari Muhinda, Muzeze katika Jimbo la Buhigwe, zipo kwenye Mchakato wa kupandishwa hadhi ili ziwe na *"A"Level.* Je, ni lini mchakato huo utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo ana nia ya kufuatilia ustawi wa Sekta ya Elimu katika jimbo lake. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Serikali tayari imeanza kufanya tathmini katika shule alizozitaja kwa ajili ya kuona kama zinakidhi vigezo kupandishwa hadhi. Pia, Serikali inaweka kwenye mipango na bajeti yake kupitia Halmashauri ili iweze kuanza kujenga shule hizo kwa maana ya kujenga mabweni kwa ajili ya hatimaye kuja kupandishwa hadhi shule hizo kuwa *form five* na *form six. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilituletea takribani shilingi milioni 470 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Sayuta ili iweze kupandishwa hadhi na kuwa shule ya kidato cha tano na cha sita, lakini bahati mbaya ni kwamba bweni la wavulana limejengwa, lakini halijakamilika na tuna uhitaji kama shilingi milioni 30. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutoa maelekezo tupate kiasi hicho ili shule iweze kuanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hili zuri kabisa ambalo linalenga kuhakikisha Sekta ya Elimu inaboreshwa katika jimbo lake. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumuagiza Mkurugenzi aweze kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kiwango cha shilingi milioni 30 ili aweze

kukamilisha miundombinu ambayo inahitajika kwa ajili ya shule hii kuanza kutumika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Shule ya Sekondari Mazinga ambayo ni shule ambayo iko katikati ya Ziwa Victoria, watoto ili waende shule lazima wapande *boats* na kipindi cha mvua na wakati wa upepo mkali hawawezi kwenda. Je, ni lini Serikali itatupatia pesa ya kujenga mabweni kwenye hiyo shule ili watoto wetu waweze kusoma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kwa swali lake hili zuri. Ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kufanya uwekezaji wa jumla ya shilingi trilioni 5.1 katika Sekta ya Elimu kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Awamu hii ya Sita pia yamejengwa mabweni 738 na Serikali bado inaendelea na jitihada hizo.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali kwa kuzingatia mazingira ambayo umeyataja itafika katika jimbo lake kwa ajili ya kuhakikisha shule hiyo inaweza kujengewa bweni ili wanafunzi wetu wapate sehemu nzuri na salama ya kusomea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Na. 19

**Utaratibu wa Kuwapandisha Watumishi Madaraja**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, upi utaratibu wa Serikali kuwapandisha madaraja watumishi waliofanya kazi zaidi ya miaka saba bila kupandishwa daraja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishaji wa vyeo kwa watumishi hufanyika kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyoainishwa katika Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Kada zao pamoja na mambo yote yaliyoainishwa katika Aya ya 4.4 ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma Toleo la Mwaka 2008, Kanuni D.51 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 2009. Pamoja na sifa na vigezo hivi, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Utumishi ana mamlaka ya kuwapandisha vyeo watumishi wenye sifa waliocheleweshwa kupandishwa cheo kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi kwa njia ya mserereko kwenye vyeo wanavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imewapandisha vyeo watumishi 1,556 waliocheleweshwa kupandishwa cheo kwa wakati kwa mserereko na mwaka wa fedha 2024/2025 watumishi 4,259. Hivyo, Serikali itaendelea kuwabaini na kuwapandisha vyeo watumishi waliochelewa kupandishwa vyeo na swali hili limeulizwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa fursa hii na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwenye Jimbo la Newala Vijijini wapo watumishi

ambao walipata athari za kutopandishwa vyeo kwa wakati kipindi kile cha uhakiki wa watumishi ambacho kilifanyika mwaka 2016 mpaka 2018. Watumishi hao mpaka leo bado wanalalamika hawajapanda vyeo. Je, upi mpango wa Serikali wa kuwanusuru watumishi hawa ili waende sambamba na wenzao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ninaomba Kiti chako kione namna ya kuwakwamua wale wote ambao walikwama kupandishwa madaraja kwa utaratibu wa kawaida ili waweze kuungana na wenzao wawekwe kwenye kundi moja kwa sababu sasa hivi wamepitwa hata na wale ambao waliajiriwa nyuma yao. Kwa hiyo ninaomba Serikali ione namna ambavyo itawafanya watu hawa wawe katika usawa na wenzao wale ambao walipandishwa vyeo huko nyuma bila kupata mkwamo. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna kipindi ambacho upandishwaji wa madaraja kwa watumishi ulisimama na hivyo njia pekee ya kuweza kufanya hivyo ilikuwa ni kuwapandisha kwa mserereko. Serikali imekuwa ikifanya hivyo na ndiyo maana nimesema watumishi 1,556 waliweza kupandishwa na tumeendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida moja ambayo inatokea ni kwa waajiri wetu wanapochelewa kuweka *data* zao vizuri kwa rekodi za watumishi na kuomba Wizarani kwetu ili tuweze kuchukua hatua hiyo. Hata hivyo, kuna kipindi cha mwaka 2023/2024, bajeti tuliyokuwa tumepanga kwa ajili ya kupandisha vyeo ilibaki kwa sababu hawakuweza kuleta watu wanaotakiwa. Kwa hiyo nitoe rai kwa Halmashauri zetu, waajiri wetu na waajiri wengine kuhakikisha kwamba wanaleta majina ya watumishi wanaotaka wapandishwe vyeo kwa mserereko ili maombi hayo tuyashughulikie kwa pamoja na hili ni kwa nchi nzima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali mnazofanya kwa upandishaji wa vyeo, lakini ili mtumishi afanyiwe ukokotozi wa kikokotoo chake ni lazima hicho cheo awe amekaa nacho si chini ya miezi sita. Je, hawa watumishi waliocheleweshwa na wengine wamebakiza mwezi kustaafu, wengine wanastaafu leo, Serikali itawachukulia vipi kwenye kikokotozi chao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janejelly kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kikokotoo kinazingatia sana ule muda aliopandishwa cheo mtumishi. Hata hivyo, tumekuwa kama Serikali tukiwashughulikia zaidi wale wanaokaribia kustaafu na kuhakikisha kwamba mambo yao yamekaa sawa. Shida moja inakuja tu pale ambapo waajiri hawafanyi kazi ile kwa wakati hata mpaka unakuta wakati hesabu inapigwa sasa bado mtumishi yule mwajiri wake hajaleta taarifa zake ipasavyo. Kwa hiyo tusaidiane wote sisi na waajiri tumewapa maelekezo kwamba wahakikishe wale wanaokaribia kustaafu basi taarifa zao zinakuja ili tuweze kuwawekea hesabu zao sawasawa ili zisiathiri maslahi yao ya kustaafu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kumekuwa na mkwamo mkubwa sana kwa wafanyakazi ambao wameongeza elimu wakiwa kazini kuweza kubadilishiwa madaraja au kuhamishiwa kwenye lile somo alilosomea. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia walimu hao au wafanyakazi wa aina hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto kwenye eneo hilo, lakini kwa sehemu fulani linachangiwa pia na watumishi wenyewe. Mtumishi ameruhusiwa na mwajiri wake akasome kitu hiki akienda kule anasoma kitu kingine ambacho pengine kinaweza kikahusisha *re-categorization* ili mambo yake mengine yaweze kuendelezwa. Sasa inapotokea mkanganyiko kama huo inakuja *issue* ya ushirikiano kati ya Wizara ya Utumishi pamoja na mwajiri na mtumishi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ninadhani tutaendelea kulishughulikia hili. Kwa upande wa Serikali tumekuwa tukifanya *re-categorization* sikumbuki takwimu, lakini pia tumekuwa tukitambua nafasi zao na elimu walizozisomea kwa wakati ili mtumishi aweze kupata motisha na kuendelea kufanya kazi vizuri. Hata hivyo, baadhi kwa kweli wanakwamishwa na waajiri wao kutokuwa *active* katika kuleta taarifa kwetu sisi kwa sababu kwetu sisi tunapokea taarifa kutoka kwa mwajiri na siyo kutoka kwa mtumishi mwenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Mohammed Zahor.

Na. 20

**Kupambana na Rushwa Wakati wa Uchaguzi**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kupambana na rushwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ikizingatia kuna upungufu wa Watumishi pamoja na vitendea kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga na kudhamiria kuwa na uchaguzi huru na wa haki ambao viongozi watachaguliwa kutokana na uwezo wao wa kuwaongoza na kuwahudumia wananchi na sio kwa kuwarubuni wapiga kura kwa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza azma hii ya Serikali, TAKUKURU imejipanga kudhibiti na kuzuia rushwa kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa kutoa elimu kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi, kufuatilia nyendo za wagombea na wapambe wao kwa lengo la kuzuia vitendo vya rushwa, kukusanya taarifa za kiintelijensia kuhusu vyanzo vya mapato ya wagombea, wapambe na vyama vya siasa ili kudhibiti matumizi ya fedha haramu, kuchunguza na kuwachukulia hatua za kisheria wagombea na wapambe watakaojihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023/2024, Serikali iliiwezesha TAKUKURU kuajiri watumishi 350, kununua magari 178 na vitendeakazi vingine ili kuimarisha utendaji kazi katika ngazi ya mikoa na wilaya. Serikali itaendelea kuiwezesha TAKUKURU kwa watumishi, fedha na vitendeakazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kuzuia na kupambana na rushwa hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zahor.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wataendelea kuwepo hapa kwa miezi mitatu inayokuja, lakini bado mazoezi kule kwenye majimbo yao yanaendelea kufanyika na kwa sababu Serikali imesema kwamba mwaka 2023/2024 imeajiri watumishi 350. Swali la

kwanza; Je, idadi hii ndiyo idadi hitajika au bado kuna mahitaji na kama yapo nini kinafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri ningeomba utusaidie kumekuwa kukijitokeza kwa dhahiri dalili za uvunjifu wa amani kwa lugha na kejeli na mambo mengi sana. Sasa ningeomba Serikali iliambie Bunge lako; je, wamejipangaje kama Serikali ili kuhakikisha kwamba uchaguzi unaokuja utakuwa wa salama, wa uhuru na haki na hakuna mtu ambaye anaweza kuzuia uchaguzi kwa mujibu wa Katiba? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri swali la kwanza linahitaji takwimu, kama unazo jibu, kama huna utazitoa baadaye.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Zahor majibu ya maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali ya Awamu ya Sita imeingia madarakani imeweka nguvu kubwa sana katika kuzuia na kupambana na rushwa. Katika kufanya hivyo tumeweza kupata vitendeakazi ambavyo kweli hatujawahi kupata kwa kiasi hicho toka chombo hiki cha TAKUKURU kuanzishwa. Kupata magari 178 kwa TAKUKURU ni jambo kubwa na imesaidia sana. Kwa sasa halmashauri zote zina magari mapya na ambao hawakupata magari mapya ya kwao ni mazima sana. Kwa hiyo itatusaidia katika kupambana katika ngazi ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka toka Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani 2022 mpaka 2025, hivi sasa tumeweza kuongeza watumishi 1,190. Watumishi hawa sisi tunaamini wanatosha karibu kila Ofisi sasa kwenye wilaya zetu zina watumishi kuanzia watano hadi 15. Sisi tunaamini hao wanatosha kuweza kupambana au kupeleka elimu kwa sababu sehemu kubwa ambayo tunataka kujikita nayo ni kuhakikisha kwamba elimu inatolewa kwa njia mbalimbali kuhakikisha kwamba wananchi wanajua madhara ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zahor pia ameuliza juu ya wale ambao wameanza harakati au dalili za kutumia rushwa, lakini kuanza harakati ambazo zinapelekea uvunjifu hata wa amani. Ninataka niseme tu nchi yetu ina uzoefu mkubwa katika kushughulika na chaguzi na mpaka sasa tumeshafanya chaguzi takribani mara saba. Uzoefu huu unaifanya nchi yetu kuwa Mwalimu wa demokrasia katika ukanda wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mbunge kwamba kwa wale ambao wamejiandaa kuleta fujo au kuleta mambo ambayo yanaleta sintofahamu kwa jamii, Serikali hata siku moja huwa haipumziki wala hakuna *gap*. Serikali ipo na hata kama tuko hapa na wengine wako hapa lakini Serikali ipo na vyombo vyetu katika kusimamia sheria huwa vina ushirikiano. Kwa hiyo hakuna mahali ambapo kutakuwa kuna upungufu wa watu wanaosimamia sheria. Ninataka nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali imejipanga katika kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kama ambavyo tumeshughulikia chaguzi nyingine kwa mafanikio makubwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

Na. 21

**Manufaa ya Fedha za Wadau wa Maendeleo - Zanzibar**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza:-

Je, kwa kiasi gani Zanzibar inanufaika na fedha zitolewazo na wadau wa maendeleo kupitia Serikali ya Muungano kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134 imeweka utaratibu wa namna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyopaswa kunufaika na mikopo, dhamana na misaada kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa muktadha huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipeleka fedha zitolewazo na wadau wa maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia fedha hizo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi hiyo imewasaidia wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki na kuinua hali zao za kiuchumi pamoja na kuongeza ajira kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pia niipongeze Serikali kwa kuendelea kupanua wigo wa upatikanaji wa fedha hizi kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo. Nipongeze vile vile ushirikiano mkubwa wa Serikali zetu mbili ambazo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar, lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa utaratibu wa mgawanyo wa fedha hizi zinazotolewa na wadau mbalimbali wa maendeleo utaratibu huu upo kwa muda mrefu sasa. Je, Serikali haioni ipo haja sasa kupitia upya utaratibu huu na kuweka utaratibu mpya ambao unaendana na wakati wa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni miradi ipi ya maendeleo ambayo Zanzibar inanufaika kupitia fedha hizi? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bakar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa kuwa amekuwa mdau mzuri wa mambo ya Muungano hasa katika kuielimisha jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu upo kwa mujibu wa sheria. Upo utaratibu maalum na utararibu huu ambao umewekwa umeshaeleza wazi kwamba Zanzibar kuna 4.5% na Bara ama kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa Tanzania Bara kuna 95.5%. Hata hivyo, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba bado vikao vinaendelea kukaliwa ili kuona namna ambavyo tunaweza tukaboresha zaidi utaratibu ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaweka Muungano huu katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miradi, miradi ipo mingi. Kuna miradi ya *Covid* ambayo ilisaidia kujenga shule, madarasa, hospitali pamoja na masoko. Kuna mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba tayari huo ni mradi ambao ulitokana na fedha hizi. Pia, kuna Mradi wa Ujenzi wa Barabara ambao nadhani kwa sasa umeshakamilika ambao unatoka Chake kupita Kisiwani kwa Binti Abeid kwenda Wete, kuna Mradi wa Barabara uliotoka Tunguu kuelekea Makunduchi pamoja na miradi mingi ya mazingira ambayo imetokana na fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kutatua changamoto na kujenga miradi ya maendeleo ya mazingira katika maeneo ya Nungwi kwa Mheshimiwa Simai, Gando hata Lindi kutokana na changamoto kubwa ya uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya wananchi. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo.

Na. 22

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Jimbo la Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Kitongoji cha Lupata Kata ya Kizumbi, Kijiji cha Lyela na Vijiji vya Mwinza na Izinga Kata ya Wampembe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imekamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara vikiwemo Vijiji vya Mwinza na Izinga vilivyopo katika Kata ya Wampembe. Aidha, Kitongoji cha Lupata kilichopo Kata ya Kizumbi kitapata umeme kupitia mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 15 vya kila Mbunge *(Hamlet Electrification Project)* na Kitongoji cha Lyela Kata ya Wampembe kitapata umeme kupitia miradi mingine itakayokuja kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina swali vijiji vyote vimepata umeme, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Tunashukuru sana Serikali kutusaidia kuwasha umeme kwenye vijiji vyote 72 katika Jimbo la Momba. Pamoja na hilo, ni upi mkakati wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vya Tarafa ya Ndalambo, Msangano na Kamsamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mkakati wa kuendelea kupeleka umeme katika vitongoji na sasa hivi tuna mradi ambao unapeleka umeme katika vitongoji 15 kwa kila Jimbo, ambapo wakandarasi wamemaliza *survey* na sasa hivi wapo katika hatua ya kupata vifaa ili taratibu nyingine za miradi ziendelee. Katika vitongoji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, Serikali inao mkakati wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 9,000 katika mwaka ujao wa fedha. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baadhi ya vitongoji katika tarafa hizo tutaziangalia kwa ajili ya kuwapelekea umeme. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

Na. 23

**Kupunguza Tozo na Kodi za Uingizaji wa Samaki**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza tozo na kodi za uingizaji wa samaki toka nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi *(Task Force on Tax Reforms)* katika vikao vyake, inaendelea kupokea mapendekezo yanayowasilishwa na wadau kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kina hufanyika ili kubaini hali ya soko, tabia za walaji, mahitaji, gharama, athari kwa mapato ya Serikali na kuzingatia umuhimu wa kulinda walaji na

wafanyabiashara wa ndani ili kuongeza mchango wa thamani katika mnyororo wa uchumi. Hivyo, maamuzi na mapendekezo ya kupunguza tozo na kodi za uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi yatafanywa kulingana na matokeo ya tathmini husika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niulize swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki wana protini nyingi sana, ambapo wajawazito wanatakiwa watumie samaki kwa wingi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba mtoto aliyeko tumboni anaweza kupata virutubisho hivyo pamoja na protini ili akizaliwa aweze kukua vizuri na pia watoto walioko shuleni waweze kutengeneza ubongo wao uwe ubongo wenye ufahamu mzuri.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa nini Serikali inachelewesha mchakato huu wa kuhakikisha samaki wanapatikana kwa wingi ikiwemo samaki kuingizwa kutoka nje ya nchi? *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya samaki pamoja na kuwa samaki ni kitoweo muhimu imekuwa ni ghali sana na sasa kula samaki imekuwa ni anasa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanatoa tozo kwenye chakula cha samaki ili kuhakikisha kwamba samaki wanapatikana kwa wingi ikiwa ni pamoja na kununua kwa bei nafuu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kabla ya kujibu swali moja la Mheshimiwa Ngonyani lenye sehemu (a) na (b), ninaomba nimpongeze sana kwa ufuatiliaji wa suala hili la samaki na chakula cha samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba Serikali inachelewesha kufanya tathmini ya tozo mbalimbali. Serikali ipo

katika mchakato na wakati huu ni wakati wa maboresho kama nilivyosema katika jibu la msingi. Pendekezo lake Serikali tumelichukua na baadaye tutaleta hapa na Bunge lako Tukufu litapitisha mapendekezo hayo kutoka kwa wadau mbalimbali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 24

**Ahadi ya Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Kilombero?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilombero ulianza mwezi Juni, 2024. Ujenzi umefika kwenye hatua ya umaliziaji na hadi sasa Serikali imeshatoa kiasi cha fedha shilingi 651,000,000 kwa ajili ya ujenzi huo. Kazi zinazoendelea kufanyika kwa sasa ni kuweka sakafu ya vigae, dari ya jasi, kuweka vioo kwenye madirisha na kupaka rangi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuishukuru Serikali hapa na kama ulivyosema jana kwamba Serikali iko kazini, ninathibitisha majibu haya ya Serikali kwamba Kituo cha Polisi kimejengwa na kimeshafikia 85% na mpaka viyoyozi vimeshanunuliwa. Ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa sababu ni Kituo cha Polisi cha Wilaya, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio na nyumba za Polisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mwaka 2023 Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alitembelea Jimbo la Kilombero na Kata ya Mwaya, akatembelea kituo cha Polisi cha mabanzi ya mbao na akaahidi kwamba ataleta pesa za kujenga Kituo cha Polisi cha Kata ya Mwaya. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Asenga kwa ufuatiliaji mzuri wa kituo hicho cha Polisi ambacho kimefikia hatua nzuri ya 85%. Ninaomba kujibu maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi litafanya tathmini ya gharama ya uzio pamoja na nyumba ya *OCS,* tayari kwa ajili ya kujenga nyumba hizo ili kuziweka kwenye mpango, kutengewa fedha na kuanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ya Serikali ya mwaka 2023, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali imekuwa ikiahidi na kutekeleza. Katika Kata ya Mwaya ambayo ameitaja tutaiweka kwenye mpango na kutengewa fedha, tayari kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kata ya Mwaya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiahidiwa kila bajeti, juu ya ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Sasa ninaomba nipate *commitment* ya Serikali, ni lini ujenzi huu utaanza? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka tarehe 5 Aprili, 2024 nilijibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha 2025/2026, tunaenda kutenga fedha na kujenga Kituo cha Polisi cha Ushetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kata ya Matemanga haina kabisa kituo kidogo cha Polisi na Polisi wale wanafanya kazi katika chumba ambacho walipewa kwenye jengo lililoachwa na wakandarasi wa barabara. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha ya kwenda kujenga Kituo Kidogo cha Polisi katika Kata ya Matemanga? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga vituo vya Polisi kwenye Kata zote ila inajenga awamu kwa awamu. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Kata ya Matemanga ambayo ameitaja, tutaiweka kwenye mpango na kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi kwenye Kata hiyo aliyoitaja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Peter Cherehani. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Cherehani, una swali Namba 25.

Na. 25

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji – Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Skimu ya Umwagiliaji katika Jimbo la Ushetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ushetu na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu lina mabonde mengi yaliyoainishwa kufaa kwa kilimo cha umwagiiliaji ikiwemo Ulowa, Kisuke, Bulugwa, Butibu, Nimbo, Nyamilangano, Sabasabini, Chona, Chambo, Mpunze, Mwadui na Bugomba B.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa mabwawa na skimu za umwagiliaji katika Mabonde ya Kisuke, Nimbo na Bulugwa, Butibu kupitia mshauri elekezi ikiwa ni hatua ya kwanza kabla ya kuanza ujenzi. Aidha, kukamilika kwa kazi hii kutasaidia kujua gharama halisi za utekelezaji wa mradi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Pia, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ni kweli timu ya wataalam imeshafika na Mheshimiwa Waziri pia alifika. Ninaendelea kuipongeza Serikali lakini ombi langu ni kwamba miradi hii ikamilike kwa wakati ili wananchi wetu wa Jimbo la Ushetu na wanaozunguka maeneo haya ya umwagiliaji waweze kupata manufaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, yote ambayo Serikali tunaahidi kupitia Wizara ya Kilimo tutayatekeleza kwa wakati. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Je, ni lini Serikali itachimba kisima katika Kijiji cha Mwamanongu, Kata ya Mwamanongu kwa kuwa tayari wananchi wameshatenga heka 150 kama mpango ulivyo? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Kilimo tayari tumeshanunua magari manne kwa ajili ya uchimbaji wa visima katika maeneo yote ambayo tumeyalenga kuwasaidia wakulima. Kwa hiyo, mawili yameshafika na mawili yako njiani, kwa hiyo, tutaanza pamoja na Meatu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Mabula ujiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua ni hatua ipi imefikiwa na Serikali kwa Miradi wa Umwagiliaji ya Kikongola, Bugolola na Miyogwezi ambayo ilitangazwa mwishoni mwa mwaka jana. Ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, katika miradi ambayo ipo katika Jimbo la Ukerewe, Wizara ya Kilimo hatua tuliyopo sasa hivi ni kwamba, tumeomba fedha Wizara ya Fedha, zikishafika sasa tutapeleka *advance payment* katika maeneo yote ambayo tayari tulishasaini mikataba na ambayo zipo hatua za mwisho. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ilemela kama lilivyo Jimbo la Ushetu, linayo mabonde mazuri kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, bahati nzuri Wizara ya Kilimo ilishakuja kufanya upembuzi yakinifu katika Kata ya Nyamhongolo, eneo la Nyamadoke na Kata ya Sangabuye, eneo la Igalagala na wakakamilisha upembuzi huo. Je, ni lini sasa kazi ya kuchimba visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa

mbogamboga utakamilika ili wale watu waweze kufanya kazi yao vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, kama nilivyojibu katika jibu la Mbunge wa Ushetu, tutafanya vivyo hivyo na Ilemela. Tayari magari tunayo na sasa hivi hatua iliyopo Wizara ya Kilimo ni kwamba, wanakwenda kufanya *surveys* kwa ajili ya kupata urefu wa maji ili yale magari tuliyonayo yaweze kuelekea katika maeneo yenu. Kwa hiyo, mambo hayo yataanza kuanzia mwaka huu wa fedha na mwaka ujao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Bonde la Eyasi katika Wilaya ya Karatu kuna mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji, mradi ule una thamani ya shilingi bilioni 21, lakini mradi ule umesimama kwa muda mrefu karibu mwaka mzima. Je, ni nini kilichosababisha mradi huo usimame na ni lini utaratibu wa kukamilisha skimu hizo utaendelea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachoeleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mradi wa Bonde la Eyasi thamani yake ni shilingi bilioni 21.8 na tayari sisi kama Serikali tumeshatoa shilingi bilioni 6.4 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, Mkandarasi anaendelea na kazi iliyoko pale. Kulikuwa tu na changamoto zikiwemo za mvua, lakini vilevile tumeshakubaliana kwamba atarudi *site* kumalizia ile kazi kwa wakati, kwa sababu fedha iliyopo inatosha kwenda zaidi ya asilimia 30 ya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Kuchauka. *(Makofi)*

Na. 26

**Ujenzi wa Barabara ya Nangurukuru – Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Liwale yenye urefu wa Km 231 utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Nangurukuru – Liwale yenye urefu wa kilometa 225.8 umekamilika. Ili kurahisisha kazi za ujenzi, barabara hii imegawanywa katika sehemu tatu, sehemu ya kwanza ni Nangurukuru – Zinga yenye urefu wa kilometa 78.7, sehemu ya pili ni Zinga – Choya (kilometa 71.4) na sehemu ya tatu ni Choya – Liwale (kilometa 75.7).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya usanifu kukamilika, Serikali imeanza ujenzi wa sehemu ya tatu ya Liwale – Choya (kilometa 75.7) ambapo zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha kilometa 10 kutoka Liwale kuelekea Choya zimetangazwa tarehe 3 Februari, 2025 na kwa sasa iko katika hatua ya uchambuzi *(evaluation)*. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Juni, 2025. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuendelea na ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo kwani wahenga wanasema, usiposhukuru kwa kidogo huwezi kushukuru kwa kingi na asiye na shukrani ya kumshukuru mwanadamu mwenzie basi hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; iko Barabara ya Morogoro

inayounganishwa na Mkoa wa Lindi kupitia Wilaya ya Liwale – Mahenge – Kilombero mpaka hapa Dodoma, ambayo ni barabara fupi sana iwe *backup* ya barabara hii ambayo sasa inatusumbua badala ya hiyo *route* wanayotuambia ya kwenda Njombe – Iringa mpaka Songea. Hiyo *route* ingekuwa ni fupi sana kwa kuja Dodoma kwa sababu ni barabara inayotoka Mahenge – Kilombero – Dumila uko Dodoma. Je, ni nini mpango wa Serikali kuijenga barabara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; iko Barabara ya *EPC+F* kilometa 175 kutoka Masasi mpaka Liwale kupitia Nachingwea ni mwaka wa tatu sasa tangu tumesaini mikataba ya barabara hiyo. Je, nini mpango wa Serikali wa kuijenga barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali la kwanza la Mheshimiwa Kuchauka, ni kweli kwamba upo mpango wa kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara ya Liwale kwenda Ulanga, barabara hii inapita kwenye Mbuga ya Selous. Kwa hiyo, Wizara ya Ujenzi kwa kusaidiana na wadau wengine, tulishatenga ipo kwenye mpango na tulishatenga bajeti kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa sababu ni barabara ambayo inapita kwenye mbuga, kwa hiyo kuna wadau wengi ambao wanahusika katika kufanya hivyo. *Once* tukishakamilisha, tutakuwa tayari kuanza kuijenga hiyo barabara kati ya Mkoa wa Lindi na Morogoro kuja Dodoma ambayo itakuwa ni fupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili ambalo ni la Barabara kilometa 175 ya Liwale – Nachingwea – Masasi, tulishaeleza kwamba ule mpango wa *EPC+F* baada ya kuachana nao tunakwenda sasa kwenye sanifu jenga na hizi barabara zimewekwa kwenye vipande. Katika hii barabara tutaanza kujenga kilometa 55 ambayo tutaanza kutokea Liwale hadi eneo linaitwa Kiangala na tunavyoongea tayari tumeshasaini mkataba. Mkandarasi ni yuleyule ambaye tulikuwa naye awali, kwa hiyo, tunategemea baada ya taratibu zote kukamilika tutaanza kujenga hiyo barabara ya kilometa 55 tukianzia Liwale. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mtwara – Kibiti – Lindi ni barabara ambayo sasa imeshakuwa kongwe na ilijengwa huko nyuma ndani ya miaka kama 40 iliyopita. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja. Je, ni lini sasa ujenzi huu wa madaraja utakamilika kwa sababu imekuwa sasa kila tunapozungumza tunaambiwa upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu! Tunaiomba Serikali itueleze ni lini madaraja yale yatajengwa na lini yataisha? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni kongwe na sasa hivi imekuwa ni kati ya barabara moja ambayo inapitisha magari mengi sana makubwa na mazito. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya mafuriko ya mwaka jana, Mheshimiwa Rais alitafuta fedha na ni fedha ambazo katika madaraja yote ya hii Barabara ya Kibiti – Lindi yapo kwenye mpango, wakandarasi tulishawapata, kazi za kuyajenga madaraja yote zimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi ambao umefanyika ni kulingana na ukubwa wa matokeo tuliyoyaona mwaka jana. Kwa hiyo, madaraja yote yanapanuliwa na tulishapata wakandarasi kwenye barabara hiyo yote ambapo wameshaanza kazi ya kuyajenga hayo madaraja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kumba

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya kutoka Somanga – Nangurukuru hadi Mbwemkuru imekuwa ikisumbua sana na hadi wakati huu kuna changamoto kubwa sana kule. Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha hiyo barabara haikatiki mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Mtenga; maeneo mengi yaliyokatika ni yale ambayo mito inapita ama kuna mabonde. Maeneo yote hayo ambayo tuliwaonesha mwaka jana, yote yametengewa fedha za dharura na tunavyoongea sasa hivi tumeshapata wakandarasi ambao wameanza kazi na tunajua itakuwa ni tiba ya kudumu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Amandus.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Tarafa za Rulenge na Murusagamba wanafahamu kwamba, Barabara yao ya Murugarama – Rulenge hadi Nyakahura ina mkandarasi na wanafahamu mkandarasi ameomba *advance payment* zaidi ya mwaka mmoja uliopita, hajalipwa. Ni upi mkakati wa Wizara ya Ujenzi kuhakikisha mkandarasi analipwa *advance payment,* ili barabara ya wananchi hawa ianze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge wa Ngara, barabara hii tayari mkandarasi ameshapatikana na sisi, kama Wizara ya Ujenzi, tumeshakamilisha taratibu zote, tumeshawasilisha maombi ya mkandarasi kwa Wizara ya Fedha na tayari tumeshaanza kulipa *advance payment* nyingi sana kwenye barabara. Ninaamini muda si mrefu tutamlipa huyo mkandarasi, ili aweze kuanza kufanya hiyo kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Amandus, jiandae Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya Nachingwea – Mkotokuyana na Nanganga ni muhimu kwa uchumi wa Nachingwea na pia, kimawasiliano kuelekea makao makuu ya mkoa. Ni lini Serikali itaijenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikiri kwamba, hii barabara ipo kwenye mpango, ni barabara ambayo haizidi kilometa 45 na tayari tumeshakamilisha usanifu. Tunachofanya sasa hivi katika mpango wa mwaka ujao ni tunaamini, tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, jiandae Mheshimiwa Amar.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Newala kuelekea Mbuyuni ilikuwa katika utekelezaji wa upembuzi yakinifu. Je, suala hili limefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulishaiweka kwenye mpango na taratibu za kukamilisha huo upembuzi yakinifu zinaendelea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ninapenda majibu yako ni mafupi, lakini yako sahihi. Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo naongea polepole. Mheshimiwa Waziri aliniahidi kwamba, upembuzi yakinifu ama mshauri elekezi, kwa ajili ya ujenzi wa Barabara yetu kwa kiwango cha lami kutoka Kahama – Nyang'hwale kwenda Busisi, mkandarasi huyu atamtangaza mwezi Februari na leo ni mwezi Aprili na ninasimama kila mara hapa, ama anataka niruke sarakasi? Ninaomba majibu sahihi kabisa leo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Amar kwamba, kazi hizi za upembuzi yakinifu zinapofanyika wakati fulani unaweza usiwaone. Nimwombe baada ya kipindi hiki mimi na yeye, Mheshimiwa Mbunge, tuweze kuongea pamoja tuone changamoto itakuwa ni

nini? Maana hii inasimamiwa na makao makuu kwa sababu, ni barabara ambayo inaunganisha mikoa takribani mitatu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini ujenzi wa Barabara ya kutoka Rangi Tatu – Kokoto – Kongowe utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara tutakachoanza kwanza ni kujenga daraja, lakini mpango tumeshauweka; Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba, tumeshapanga. Tunachotegemea sasa hivi ni kupata *advance payment* ili mkandarasi aanze kujenga hiyo barabara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, kwa niaba ya Mheshimiwa Kiswaga.

Na. 27

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nane Kibaha – Chalinze – Morogoro**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA K.n.y. MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaendeleza upanuzi wa Barabara kipande cha Kibaha – Chalinze kuwa njia nane ili kuondoa msongamano wa magari Kibaha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitaendeleza upanuzi wa Barabara sehemu ya Kibaha – Chalinze, badala yake Serikali itajenga *Express Way* ya kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro

(kilometa 220) kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership (PPP))*. Kwa sehemu ya Kibaha – Chalinze, zabuni ya kumpata mwekezaji iko katika hatua ya mwisho ya majadiliano. Ujenzi unatarajiwa kuanza baada ya majadiliano kukamilika na mkataba *(Concession Agreement)* kusainiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Koka ninaishukuru Serikali kwa mkakati huo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwanza naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Jimbo la Kalenga inajenga barabara tatu za lami, lakini imejenga Barabara kutoka Wenda – Mgama, sasa kutoka Mgama kwenda pale Iheme kuna kilometa sita. Je, ni lini Serikali itatusaidia na hicho kipande cha kilometa sita kijengwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali inajenga Barabara kutoka Tosamaganga kwenda Ugwachanya, kuna kipande kama cha mita 900 na kilikuwa katika mpango wa kujengwa mwaka huu. Je, lini Serikali itatupelekea fedha ili tuweze kukamilisha hicho kipande? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali yote mawili kwa pamoja. Dhamira ya Serikali, kama alivyosema Mheshimiwa, ni kujenga hiyo Barabara ya Wenda – Mgama na Tosamaganga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ujenzi wake utategemea na upatikanaji wa fedha ambayo ndio dhamira ya Serikali kuzijenga barabara hizo kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Subira Mgalu kwa niaba Mheshimiwa Leah.

Na. 28

**Ujenzi wa Daraja la Mpiji Chini, Kata ya Mapinga**

**MHE. LEAH J. KOMANYA K.n.y. MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Daraja la Mpiji Chini, Kata ya Mapinga, utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* itajenga Daraja la Mpiji kupitia Mpango wa Matengenezo ya Dharura yanayogharamiwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia, kupitia *Crisis Response Window*. Kwa sasa taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa daraja hilo zinaendelea na mara baada ya kukamilika ujenzi utaanza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili. Swali la kwanza; je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Daraja la Itembe lililopo Jimbo la Meatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, lini Serikali itaanza ujenzi wa madaraja katika Mto Chobe, Liusa na Nkoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Itembe lipo kwenye barabara kubwa ya kutoka Maswa, kuja Sibiti, kuja Singida na Mheshimiwa Mbunge ni shahidi kwamba, tuko kwenye asilimia za juu kabisa katika ujenzi. Kitu ambacho sasa hivi tunafanya, tumeshapokea *certificate* ya mkandarasi, ili aweze kulipwa na kuendelea na kazi na tunatamani kazi hiyo ikamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraja mengine aliyoyataja, Serikali ina mpango wa kuyajenga, lakini itategemea na upatikanaji wa fedha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ujenzi wa Daraja la Mto Nakiu kutoka Nanjirinji kuelekea Ruangwa lini utakamilika? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa hilo daraja bado haujaanza, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kati ya madaraja ambayo yako kwenye mpango wa madaraja ya dharura ambapo wenzetu wa *World Bank* watatukopesha na tayari hizo fedha tumeshazipata. Kwa hiyo, tuwe na uhakika kwamba, daraja hilo linaenda kukamilika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Daktari Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa hii nafasi. Je, ni lini Daraja la Mto Kikavu litajengwa upya pamoja na kuipanua Barabara ya Moshi – Arusha, ambapo sasahivi kuna msongamano mkubwa kati ya Moshi mpaka Sangisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia vizuri daraja alilolitaja na barabara yake.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, narudia. Je, ni lini Serikali itakwenda kujenga upya Daraja la Mto Kikavu katika Barabara ya Moshi – Arusha, pamoja na kuipanua barabara ile kuanzia Sangisi – Tengeru mpaka Moshi kwa sababu, sasahivi ina msongamano mkubwa wa magari? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, Daraja la Kikavu kwanza lilipo linahamishwa na itajengwa kwa njia nne na tunajenga kupitia Mfuko wa *JICA* ambao usanifu umeshakamilika. Muda wowote tunategemea kazi hiyo ya kupanua hiyo barabara na kulijenga daraja hilo upya ianze. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

Na. 29

**Maeneo Mapya ya Utalii Nchini**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanua wigo wa maeneo mapya ya utalii nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na utalii imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini, ili kuvutia watalii wengi zaidi, kuongeza siku za watalii kukaa nchini, kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii pamoja na kupunguza utegemezi katika zao la utalii wa wanyamapori nchini. Mikakati inayotekelezwa ni pamoja na kufanya mazoezi ya kubaini vivutio vipya vya utalii nchini; ambapo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara imebaini vivutio vipya 337 katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Kigoma. Aidha, zoezi la kubaini vivutio vipya vya utalii ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, ikiwemo utalii wa fukwe, meli, mikutano na matukio, malikale na utamaduni na

michezo. Mathalani, katika kuendeleza utalii wa meli nchini, Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau wa sekta binafsi wenye mtandao mkubwa katika soko la kimataifa la utalii wa meli kutangaza zao hili. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya meli za kitalii tisa ziliwasili nchini na kuleta watalii 2,944 waliotembelea vivutio mbalimbali vya utalii.

**NAIBU SPIKA:** Profesa Patrick.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; moja ya changamoto kubwa inayowakabili watalii kupanda Mlima Kilimanjaro au kufikia vivutio vya Mlima Kilimanjaro ni ubovu wa Barabara. Mifano ya barabara ambazo ni mbovu sana ni Barabara ya Kata ya Mbokomu inayopeleka watalii kuona mti mrefu kuliko yote Afrika na Barabara ya Umbwe ambayo inapeleka watalii kwenda mlimani. Kwa kuwa, kuna wingi wa kazi upande wa *TARURA*.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia pesa zinazotolewa kwa jamii inayozunguka Mlima Kilimanjaro, kama *CSR,* kufanya ukarabati wa barabara hizi, ikiwa ni pamoja na kuziwekea lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wa Kata ya Uru Shimbwe wamekuwa na kiu kubwa sana ya kujengewa lango la kuingia Mlima Kilimanjaro kupitia katika Kata hii, ili wananchi wapate ajira ikiwa ni vijana na wananchi wanaoishi pale. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wananchi hawa wapate hili lango?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *KINAPA* imekuwa na utaratibu wa kujenga barabara hizi zinazopeleka watalii kwenye maeneo ya vivutio vya utalii. Mfano kule Kilimanjaro tumeweza kujenga barabara ya kutoka kwenye Chuo chetu cha Mweka mpaka kwenye Lango la Mweka, lile ni eneo ambalo limefungua sana utalii kwenye maeneo yetu kwa hiyo, tutaendelea kufanya shughuli hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge; kwa sababu, fedha hizi za *CSR* zina umuhimu mkubwa sana wa kuwafanya wananchi wajione kuwa ni sehemu ya uhifadhi katika maeneo haya. Fedha hizi tuzielekeze kwenye shughuli hizi za elimu, maji na ulinzi wa mazingira. Ndani ya Serikali tutahakikisha tunatenga fedha za kutosha kuhakikisha *TARURA* nayo inatimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la pili la kufungua Lango la Shimbwe. Kwa sasa Serikali imejipanga kujenga barabara mbili, barabara ya eneo la Tesheni upande wa Kaskazini – Magharibi mwa hifadhi. Vilevile, kwenye njia ya kupandia kule Kidia na yenyewe ipo kwenye mpango wa ujenzi kwa sasa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kwamba, Serikali ijielekeze kwenye kukamilisha barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lake tumelipata. Baada ya kukamilisha ujenzi huu, basi kulingana na upatikanaji wa fedha tutaendelea kufanya kwenye lile eneo alilopendekeza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Moshi Vijijini kuna vivutio vingi yakiwemo makazi waliyokaa Mangi wetu kama Marealle, Mandara na Malamia. Je, ni lini Serikali itakarabati maeneo haya, ili Serikali iweze kuingiza kipato na wananchi wa pale, mmoja mmoja, waweze kupata ajira? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, kutambua vivutio vipya vya utalii ni kazi endelevu. Miongoni mwa maeneo ambayo tumeyatambua ni pamoja na haya aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge. Tunaomba atupe muda, ili tuweke huo mpango wa kuhakikisha kwamba, vivutio vyote hivi ambavyo tumevitambua vinafikika na viweze kutumika katika kuendeleza utalii katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni upi mpango wa Serikali wa kutafuta wawekezaji wa kujenga hoteli za kitalii, hususan katika Mkoa wangu wa Arusha, ambazo zimekuwa ni changamoto kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia taasisi zake imekuwa ikishiriki katika makongamano mbalimbali ya uwekezaji, kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji kuongeza nguvu kuwekeza katika maeneo ya malazi. Nimhakikishie kwamba, kupitia *TTB* na taasisi zetu nyingine jukumu hilo tunalifanya kwa umakini mkubwa kwa sababu, tunaelewa kwamba, tunayo changamoto ya maeneo ya malazi katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Maporomoko ya Mto Kalambo ni ya pili Afrika, lakini ukweli usiopingika ni kwamba, matangazo hayajafanyika vya kutosha. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, inatangaza ili yaweze kujulikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kandege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Maporomoko ya Kalambo ni maporomoko ambayo yana sifa ya kipekee na moja ya zao muhimu sana kuendelezwa. Sisi Wizara tumekwishachukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba utangazaji wa maeneo haya unafanyika kwa nguvu kubwa. Kama anafuatilia, kwenye Ligi Kuu yetu ya Tanzania moja ya vivutio vinavyotangazwa kwa nguvu kubwa kwenye matangazo ya viwanja vyetu vya mipira na kwenye makongamano mbalimbali ya uwekezaji ni pamoja na kivutio hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira naamini ndani ya kipindi kifupi mambo mazuri yanakuja katika eneo hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mheshimiwa Mariam Madalu.

Na. 30

**Elimu ya Mikopo kwa Makundi Maalum**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu ya mikopo ya Mifuko mbalimbali inayokopesha makundi maalum?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Halmashauri

na viongozi wa wafanyabiashara ndogondogo tunaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kupitia mikutano ya hadhara, vyombo vya habari na watu mashuhuri kupitia majukwaa yao kutoa elimu juu ya uwepo wa mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa na Serikali kwa makundi maalum. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Madalu.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ipo Mifuko mingapi hadi sasa ambayo ina lengo la kukopesha kundi hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kuunganisha Mifuko hii ili kuwa na uratibu mzuri zaidi hasa kwa kundi hili maalum? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la kwanza; Serikali ina idadi ya Mifuko 75 ambayo inawezesha wananchi kuendeleza kiuchumi na kwa mikopo ya bei nafuu. Katika Mifuko hiyo tuna Mifuko ya 10% ambayo ni mapato ya halmashauri, tuna Mifuko ya Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga) na vilevile lakini tuna Mfuko wa Uwezeshaji wa Wanawake *(WDF)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, Serikali inaendelea na mchakato wa kukusanya pamoja Mifuko hii ili kuendelea kuleta ufanisi zaidi kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mikopo ile kwa kunufaika. Pia Serikali inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Baraza la Taifa la Uwezeshaji ili kuhakikisha kwamba kazi hiyo inafanyika kwa haraka. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa haya maswali yamekwisha, tunaanza kipindi cha wageni. Ninamwita Mwenyekiti atangaze wageni Mheshimiwa Najma.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi chetu cha maswali na sasa ni wakati wa matangazo. Nitaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Wageni 28 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawa ni Viongozi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Wakuu wa Taasisi ambao ni Dkt. Jim James Yonazi - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu; Ndugu Mary Maganga - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu; Dkt. James Kilabuko - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu; na Ndugu Zuhura Yunus - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Jaji Mstaafu Jacobs Mwambegele - Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi; Mheshimiwa Jaji Mstaafu Francis Mutungi - Msajili wa Vyama vya Siasa; Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mbarouk S. Mbarouk - Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi; Mheshimiwa Ramadhani Kailima - Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi; Ndugu Aretas Lyimo - Kamishna Jenerali, Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; na Ndugu Mwamini Juma - Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Joyce Mapunjo - Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF);* Ndugu Renata Rugarabamu - Mwenyekiti wa Bodi ya Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF);* Alhaj Dkt. Almasi Selemani - Mwenyekiti wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA);* Dkt. Suleiman Mohamedi - Mwenyekiti wa Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara Sekta Binafsi; Ndugu Pelesi Jonathan - Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya *LESCO;* na Ndugu Tungi Mwanjala - Makamu Mwenyekiti SHIVAWATA, karibuni sana. *(Makofi)*

Aidha, wapo Ndugu Abdul-Razaq Badru - Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF);* Ndugu Masha Mshomba - Mkurugenzi Mkuu, Mfuko wa Taifa wa Uhifadhi wa Jamii *(NSSF)* na Ndugu John Mduma - Mkurugenzi Mkuu, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)*.

Yupo pia Ndugu Khadija Mwenda - Mtendaji Mkuu, Wakala wa Usalama wa Afya Mahala Pa Kazi *(OSHA);* Ndugu Usekelege Mpulla - Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*; na Ndugu Suzan Mkangwa - Kamishna wa Kazi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Beng'I Issa - Katibu Mtendaji, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Ndugu Dkt. Tumaini Nyamhokya - Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA);* Ndugu Oscar Mgaya - Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri *(ATE);* Ndugu Dkt. Lucas Kija - Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu; Ndugu Mark Bryan Schreiner - Mwakilishi Mkazi *(UNFPA);* na Ndugu Catherine Joachim - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI, karibuni sana wageni wetu wote ambao mpo kwenye Jukwaa la Spika, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu wa taasisi zake. Karibuni wote katika Bunge letu.

Wageni wengine ni Wageni 35 wa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ambao ni Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha Bahari Dar es Salaam. Karibuni sana Wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, kutoka Mkinga Mkoani Tanga, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambaye ni Ndugu Joseph Magesa, Rais wa Shirikisho la Wanafunzi Wanaosoma Ugavi na Manunuzi Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Boniphace Getere ambaye ni Ndugu Giragu Nyarumuga, Mwenyekiti wa Kijiji cha Sarakwa Bunda, Mkoa wa Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, kutoka Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni Ndugu Elson Jackson, mwanafunzi wa Shahada kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna pia wanafunzi 80 na viongozi nane ambao ni Wanachama wa Skauti kutoka Shule ya Msingi Aniny Nndum ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu.

Baada ya matangazo hayo ya wageni, tuna tangazo hapa. Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuwa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu J. K Nyerere inawaalika kwenye Maadhimisho ya Kumbukizi ya Miaka 103 ya Baba wa Taifa, Mwalimu J. K. Nyerere. Maadhimisho haya yatafanyika siku ya Jumapili, tarehe 13 mwaka huu 2025 kuanzia saa mbili asubuhi katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Jijini Dodoma. Kauli mbiu ni Chagua Viongozi Bora kwa Ustawi wa Jamii na Maendeleo Endelevu ya Taifa Letu. Maadhimisho haya ni mwendelezo wa Utekelezaji wa Mpango wa Miaka 10 ya Kuenzi na Kusherekea Urithi wa Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere ambao ulizinduliwa Kitaifa Mwaka 2022 Butiama, Mkoani Mara.

Madhumuni makubwa ya maadhimisho haya ni kwanza kuwashirikisha Watanzania, Wizara na taasisi wakiwemo watoto na vijana wa Taifa letu katika kumuenzi Baba wa Taifa kwa kazi nzuri aliyoifanyia Taifa letu.

Pili, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi uliotukuka kwa kuongoza nchi yetu kwa

mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake. Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya atakuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa wote mnaalikwa kuhudhuria maadhimisho haya muhimu.

Kuna tangazo lingine kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuwa *Bunge Marathon,* awamu ya pili itafanyika siku ya Jumamosi tarehe 12 mwaka huu, Aprili, 2025. *Marathon* hii itahusisha mbio za kilometa tano, kilometa 10 na kilometa 21 na washindi watapewa zawadi mbalimbali ikiwemo fedha tasilimu. *Marathon* hii imelenga kukusanya fedha kwa ajili ya kujenga Shule Maalum ya Sekondari ya Bunge ya Wavulana wa kidato cha tano na sita. Kauli mbiu ni Shiriki Michezo kwa Maendeleo ya Taifa letu.

Mgeni Rasmi katika mbio hizi atakuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa wote mnakumbushwa kushiriki bila kukosa *Marathon* hii ili kuimarisha afya zetu na kujenga umoja na ushirikiano kwa maendeleo ya nchi yetu.

Baada ya matangazo hayo nampisha Mheshimiwa Naibu Spika ili aweze kuendelea na kazi.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote Chama Cha Mapinduzi, mnatangaziwa kikao cha *Party Caucus* kitachofanyika leo jioni, saa kumi na mbili na nusu jioni *White House* (CCM) Makao Makuu wote muhudhurie bila kukosa. Tangazo linatolewa na Katibu wa Bunge *Party Caucus Fascist* Shangazi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Mfuko wa Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu. Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2025/2026. Pia, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zilizopo chini yake na Mfuko muhimu kwetu Waheshimiwa Wabunge wa Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wenye afya njema tayari kwa kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali ya Awamu ya Sita zilizotekelezwa kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 na mwelekeo wake kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Waislamu wote kwa kumaliza salama Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikukuu ya *Eid el Fitri* kwa amani. Aidha, niwatakie kila la heri Wakristo wote wanaoelekea

kuhitimisha Mfungo wa Kwaresma pamoja na maandalizi mema ya Sikukuu ya Pasaka kwa mwaka huu wa 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu za pole; wakati tukiendelea na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 Bunge lako Tukufu lilipoteza viongozi mashuhuri pamoja na wanasiasa wakongwe ambao wamewahi kutumika katika nafasi mbalimbali zikiwemo za ubunge na nyingine katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 27 Novemba 2024, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani ukanda wa Afrika. Ninatoa salamu za pole kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 17 Desemba, 2024 taifa letu liliondokewa na Mheshimiwa John Tendwa, Msajili Mstaafu wa Vyama vya Siasa. Marehemu John Tendwa atakumbukwa kwa kujenga misingi imara kwa vyama vya siasa. Pia, atakumbukwa kwa ukomavu wake hususan katika kusimamia demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, tarehe 27 Desemba, 2024 tuliondokewa na Mheshimiwa Mwanaisha Athumani Kwariko - Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi. Marehemu Mwanaisha Kwariko, atakumbukwa kwa utumishi wake ndani ya mahakama na mchango wake mkubwa katika Tume Huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 Desemba, 2024 tuliondokewa na Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema aliyewahi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marehemu Jaji Fredrick Werema, pamoja na kazi nyingine atakumbukwa kwa ushauri na mchango wake wa kisheria katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Februari 2025, nchi ilimpoteza Bibi Sifael Mushi, mwanamke aliyeshiriki katika tukio la kuchanganya udongo wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar. Bibi Sifael Mushi atakumbukwa kwa uzalendo na historia ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, tarehe 5 Machi, 2025, tulimpoteza Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi aliyewahi kutumikia Taifa letu kwa nafasi ya Mbunge, Mkuu wa Mkoa na Waziri katika Wizara mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa marafiki na Watanzania wote walioguswa na msiba huo. Mheshimiwa Profesa Sarungi atakumbukwa kwa utumishi wake uliotukuka, uwajibikaji na uzalendo kwa nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, usiku wa kuamkia tarehe 13 Machi, 2025, tulimpoteza mwanasiasa mkongwe Mheshimiwa Tabitha Siwale, aliyewahi kuhudumu katika nafasi ya Mbunge na Waziri katika Wizara mbalimbali. Itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 3 Novemba, 1975, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Tabitha Siwale kuwa Mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mchango wake katika jamii, Hayati Mheshimiwa Tabitha Siwale, alitunukiwa Tuzo ya Mwanamke Mahiri wa Karne ya 21 mwaka 2000 na Tuzo ya Mwanamke wa Mwaka katika mwaka 2008. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na kwa Watanzania wote walioguswa na msiba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Machi, 2025 nchi yetu pia iliondokewa na mwanadiplomasia mkongwe Mheshimiwa Balozi Juma Volter Mwapachu. Balozi Mwapachu aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki aliwahi kuwa mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)*. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na kwa Watanzania wote walioguswa na msiba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha hivi karibuni, wapo Watanzania wenzetu waliofikwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali ikiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo, Ninawaombea marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pongezi; sote tunafahamu kuwa, mwaka huu, Bunge la Kumi na Mbili, linahitimisha shughuli zake kwa kipindi cha miaka mitano kilichoanza Novemba, 2020. Kwa msingi huo, hotuba yangu itaeleza kwa muhtasari mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii pia, imeainisha baadhi ya kazi zilizotekelezwa na Serikali kwa kuzingatia mipango na mikakati mbalimbali ya Taifa. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026, ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Ajenda ya Mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika; na Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri tangu alipoanza kuiongoza nchi hii tarehe 19 Machi, 2021. Ninampongeza pia kwa mafanikio makubwa aliyoyapata katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020. Kwa hakika ametekeleza kwa vitendo na matokeo yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu; kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii. Pia, kusimamia utawala bora; kuongoza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi; na kuhamasisha uwekezaji, diplomasia

ya kiuchumi nayo imesimamiwa na mahusiano ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuliongoza Taifa letu. Kwa hakika, miongoni mwa maelekezo ya viongozi wetu yamekuwa yakitoa mwelekeo sahihi wa utekelezaji wa wajibu wetu kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuhakikisha kuwa Ilani ya CCM kwa upande wa Zanzibar inatekelezwa kikamilifu na kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi na usimamizi wa sekta mbalimbali za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kipekee kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa Chama Cha Mapinduzi katika nafasi ya Urais kwenye Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wao ni kielelezo cha ukomavu na imani kubwa waliyonayo wana CCM wote kwa viongozi hawa kutokana na uongozi wao makini na imara unaozingatia maslahi ya wananchi wote. Nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi ni mwanasiasa mkongwe mwenye uzoefu mkubwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali na Jumuiya za Kimataifa.

Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Steven Masatu Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Bara. Nirudie kauli yangu niliyoitoa katika Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 14 Februari 2025 kuwa, Chama kimepata mtu sahihi kwa wakati sahihi kutokana na uzoefu wake na busara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Wasira ni kiongozi na Mwanasiasa mkongwe, ambaye mchango wake unaendelea kuhitajika katika kuimarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu kupitia Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Mbunge Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Vilevile, ninampongeza sana kwa kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati, jitihada zake zimeleta mwelekeo na matokeo chanya katika upatikanaji wa nishati nchini. Sote tumeendelea kushuhudia mtandao wa umeme ukiendelea kuongezeka hadi vijiji na sasa tunaelekea kwenye vitongoji. Pia, nimpongeze sana kwa kusimamia ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge Duniani. Pia wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu katika kuisimamia Serikali, kuhakikisha kuwa inatekeleza wajibu wake wa kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa na nzuri za kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; pia, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi; Kamati ya Kudumu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati hizo yamesaidia sana kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Mashirika, Wakala na Idara zinazojitegemea kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya nafasi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Hamza Saidi Johari Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushauri wake wakati wote wa mikutano ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, ninamshukuru sana Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, kwa ushirikiano wake wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru watumishi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa. Jitihada zao, zimechangia tija na ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali. Vilevile, ninawashukuru kwa michango yao, inayowezesha kukamilisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, ninawashukuru:-

(i) Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrsiho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu); *(Makofi)*

(iii) Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Pamoja na Mheshimiwa Patrobas Katambi, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu); *(Makofi)*

(iv) Makatibu Wakuu wakiongozwa na Dkt. Jim Yonazi, Katibu Mkuu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Bi. Mary Maganga (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu);

(v) Naibu Makatibu Wakuu akiwemo Dkt. James Kilabuko anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu na Bi. Zuhura Yunus Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); na *(Makofi)*

(vi) Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuwashukuru washirika na wadau wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga uchumi na kuiletea nchi yetu maendeleo. Mipango yao imekuwa muhimu katika kuwezesha

nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa kuzingatia mipango tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kushirikiana nami na kuniunga mkono katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya pamoja. Wanaruangwa wamekuwa wavumilivu katika kipindi chote nilipokuwa mbali nao wakati nikitekeleza majukumu ya kiserikali, hii imeonesha ni kwa namna gani wamekuwa wastahimilivu na waungwana kwa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushirikiano wao kwa Serikali umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninapenda kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa Bi. Mary Majaliwa, watoto wangu na familia yangu kwa ujumla kwa upendo, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa. Ninawashukuru sana na ninawapenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita; kama nilivyoeleza hapo awali, katika hotuba yangu ya mwaka 2025 nitaanza kueleza kwa muhtasari mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Mheshimiwa Rais mara baada ya kushika hatamu ya kuliongoza Taifa letu, aliweka bayana vipaumbele na mwelekeo thabiti unaolenga kuwatumikia Wananchi wa Tanzania wakati alipolihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais aliahidi kudumisha mazuri yote ya awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuibua mengine mapya. Alisisitiza utekelezaji wa ahadi hizo kupitia salamu ya 'Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Kazi Iendelee', na kwa hakika kazi

imefanyika, yaliyoachwa yametekelezwa, mapya yameibuliwa tena kwa mafanikio na tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Mheshimiwa Rais alielekeza Serikali anayoiongoza kutekeleza majukumu kwa kuzingatia falsafa ya *4Rs* ambayo inasisitiza umuhimu wa kuwa na Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga upya. Falsafa hiyo inalenga kulileta Taifa pamoja, kujenga hali ya kuvumiliana, kuwa na makubaliano ya pamoja na kulijenga upya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mwelekeo na maono ya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha uongozi wake, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Shughuli hizo ni pamoja na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya uchumi, kuongeza fursa za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kupitia sekta za uzalishaji, kuboresha huduma za kijamii ikiwemo afya, elimu na maji, kutekeleza mikakati thabiti ya kuvutia uwekezaji nchini na kukuza uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana yanawezesha kukua kwa uchumi wa nchi yetu pamoja na kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nilitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi wote wanaotusikiliza kupitia Vyombo vya Habari kwamba, baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uongozi wa Awamu ya Sita ni haya yafuatayo:-

(a) Uzalishaji wa Ajira; Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuzalisha fursa za ajira nchini kupitia uwekezaji na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki, reli ya kisasa, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kupanua wigo wa uzalishaji

wa ajira hapa nchini. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Februari, 2025 jumla ya ajira 8,084,204 zimezalishwa katika sekta ya umma na sekta binafsi. *(Makofi)*

(b) Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa; Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe Mosi Agosti, 2024, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua huduma za usafiri wa reli kati ya Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma. Hadi kufikia Februari, 2025, abiria 1,809,983 wamesafirishwa na jumla ya shilingi bilioni 54.9 zimekusanywa. Uwepo wa huduma hiyo ya treni, umepunguza muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kutoka wastani wa saa 10 kwa basi hadi kati ya saa tatu na nne na kuchagiza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Hadi kufikia Februari, 2025 ujenzi wa kipande cha kutoka Mwanza - Isaka (kilometa 341) umefikia 62.37%; Makutupora – Tabora (kilometa 368) umefikia 14.35%; Tabora – Isaka (kilometa 165) umefikia 6.33%; na Tabora – Kigoma (kilometa 506) umefikia 7.34%. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa kipande cha Uvinza - Malagarasi - Musongati (kilometa 282) yameanza ambapo Serikali za Tanzania na Burundi zilisaini mkataba wa ujenzi wa kipande hicho Siku ya tarehe 29 Januari, 2025. *(Makofi)*

(c) Uimarishaji wa Huduma za Bandari ya Dar es Salaam; Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ushindani wa kibiashara uliopo katika ukanda wa Bahari ya Hindi, nchi yetu imechukua hatua mahsusi ili kunufaika na fursa ya kijiografia ambayo tunayo ya kuwa ni lango kuu la biashara kwa nchi jirani. Hatua hizo ni pamoja na uboreshaji wa bandari zetu zilizopo katika Bahari Kuu na uwekezaji wa sekta binafsi katika kutoa baadhi ya huduma bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya makasha yanayohudumiwa yameongezeka na kufikia 686,515 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 ikilinganishwa na makasha 670,724 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Ongezeko hilo lilichangiwa na uwekezaji uliofanyika

katika gati 0-7 ambapo idadi ya makasha yaliyohudumiwa katika eneo hilo yaliongezeka kutoka 122,339 hadi 160,286 katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, muda wa meli za makasha kusubiri nangani umeondolewa kabisa. Hivi sasa, meli hufunga gatini mara tu zinapowasili katika Bandari ya Dar es Salaam. Hali hiyo imepunguza wastani wa muda wa meli zisizokuwa za makasha kusubiri nangani kutoka siku 46 za awali hadi siku saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na kupungua kwa idadi ya meli zinazosubiri nangani kutoka meli 30 hadi tatu; muda wa meli wa kuhudumiwa nao umepungua kutoka siku nane hadi tatu kwa meli za makasha; muda wa kuhudumia meli za mafuta umepungua kutoka siku 10 hadi siku tatu. Kuimarika kwa utoaji wa huduma hizo kumepunguza tozo ya meli kusubiri nangani na hivyo kuchangiza kupunguza gharama za bidhaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, mapato ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa mwezi yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 mwaka 2023/2024, hadi kufikia wastani wa shilingi trilioni moja mwaka 2024/2025. Aidha, mapato yanayokusanywa kutokana na Ushuru wa Forodha nayo pia yameongezeka kutoka shilingi trilioni 9.35 mwaka 2023/2024, hadi shilingi trillioni 9.86 kufikia Februari, 2025.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, tunaimarisha Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)*. Serikali imeendelea kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania ili kutoa huduma bora za usafiri wa anga kwa abiria na mizigo yake, ndani na nje ya nchi. Serikali katika kipindi cha Novemba, 2020 – Februari, 2025 ilitumia shilingi trilioni 1.49 kununua ndege saba, ambapo ndege sita ni za abiria na ndege moja ni ya mizigo. Ununuzi wa ndege hizo umelifanya Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 ambazo zimeimarisha na kuongeza safari za ndege za ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Shirika la Ndege Tanzania limeongeza safari za ndege kwenda nje ya nchi, ambapo ndege

zake zinasafiri kwenda Johanesburg Nchini Afrika Kusini, Guangzhou Nchini China, Mumbai Nchini India, Lubumbashi Nchini *DRC,* Lusaka na Ndola Nchini Zambia, Harare Nchini Zimbabwe, Dubai kwenye Falme za Kiarabu, Nairobi Nchini Kenya, Entebbe Nchini Uganda, Bujumbura Nchini Burundi, Moroni Nchini Comoro na hivi karibuni litaanza safari za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi Kinshasa, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la ndege limechangia pia kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaohudumiwa kutoka abiria 822,232 kwa mwaka 2021, hadi abiria 3,818,567 Februari 2025; mizigo kutoka tani 2,567 mwaka 2021 hadi tani 5,730.48 Februari 2025. Kadhalika, mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 254 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.5 Februari 2025 mwaka huu. *(Makofi)*

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa madaraja makubwa; Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa ya *Tanzanite* lililoko Jijini Dar es Salaam, lenye urefu wa kilometa 1.03 na kule Wami Mkoani Pwani lenye urefu wa mita 510. Aidha, inaendelea kutekeleza ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi, Mkoani Mwanza, lenye urefu wa kilometa 3.2 ambao umefikia 98%. Lengo la ujenzi wa madaraja hayo ni kurahisisha shughuli za kiuchumi na ufikiwaji wa huduma za kijamii kwa haraka, kwa kupunguza foleni na muda wa usafiri wake. *(Makofi)*

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu; utoaji wa huduma za usafiri katika Maziwa Makuu umeendelea kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapiga hatua za kiuchumi. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa Meli ya *MV Mwanza* kwa gharama ya shilingi bilioni 109. Ujenzi wa meli hii umefikia 98%, na itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 pamoja na tani 400 za mizigo; vilevile, magari madogo 20 na malori matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali inaendelea na ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika ambazo ni *MT Sangara* kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 3.60, ambao vilevile

umefikia 98%. Mradi huo utakapokamilika utawezesha kubeba shehena ya mafuta kiasi cha lita 410,000. Pia, *MV Liemba* kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 13.19 ambao umefikia 15%, na mradi huo utakapokamilika utawezesha kubeba abiria 600 na tani 200 za mizigo.

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere wa Megawati 2,115; Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme katika Bwawa la Julius Nyerere kwa gharama ya shilingi trilioni 6.6. Ujenzi wa mradi huo wenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 kwa siku umekamilika. Hadi Machi, 2025, jumla ya megawati 2,115 zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na hivyo kuongeza kiwango cha umeme katika Gridi ya Taifa kufikia megawati 4,031.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika mradi huo kumeongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuwa chachu ya kasi ya maendeleo ya nchi yetu.

(h) Mheshimiwa Naibu Spika, uunganishaji wa umeme vijijini; katika kipindi cha Novemba, 2020 – Februari, 2025, Serikali imeunganisha umeme katika vijiji 4,071 kwa gharama ya shilingi 1,593,000,000 na hivyo kuwezesha vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kuunganishwa na umeme. Hatua inayofuata baada ya kukamilisha mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vyote ni kupeleka umeme kwenye vitongoji, ambapo jumla ya vitongoji 33,657 kati ya 64,359, sawa na 52.3% vimeunganishwa na huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa umeme katika vijiji na vitongoji utawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi hususan zinazohitaji nishati ya umeme, zikiwemo kuchomelea vyuma, useremala, kuchakata nafaka na kuchenjua madini.

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanga, Nchini Tanzania. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya

Uganda inatekeleza ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki lenye urefu wa kilometa 1,443 kutoka Hoima Nchini Uganda mpaka Tanga hapa Nchini Tanzania. Utekelezaji wa mradi huo umefikia 55%, ambapo kilometa 1,115 za bomba hilo zinapita hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeshachangia mtaji wa Dola za Marekani milioni 376, sawa na 15% ya hisa. Kupitia mradi huo, jumla ya ajira 6,610 za muda na ajira 114 za kudumu zimeshaanza kuzalishwa. *(Makofi)*

(j) Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nieleze ujenzi wa Shule za Sayansi za Wasichana katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kama ambavyo mnakumbuka, wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani alieleza azma yake ya kumsaidia mwanamke. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita imejenga shule za wasichana katika mikoa 26 zenye michepuo ya masomo ya sayansi. Hadi sasa, ujenzi wa shule hizo umegharimu shilingi za Tanzania bilioni 121.55, na tayari wanafunzi 10,274 wameshadahiliwa na wanaendelea na masomo. *(Makofi)*

(k) Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa wanafunzi wa vyuo vikuu na vyuo vya kati; kwa upande mwingine, Serikali ya Awamu ya Sita imeanzisha programu ya ufadhili wa wanafunzi wa elimu ya juu, inaitwa *Samia Scholarship Program,* kwenye fani za sayansi, teknolojia, ubunifu, uhandisi, hisabati na tiba, hasa kwa wenye ufaulu wa kiwango cha juu. Fedha shilingi bilioni 6.63 zimekwishatolewa tangu kuanza kwa programu hiyo na kunufaisha wanafunzi 1,313. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali inatoa ufadhili wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati, wanaosoma stashahada za fani na ufundi. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo, shilingi bilioni 20.08 zimetolewa na kunufaisha wanafunzi 7,732. Pia, Serikali imeanzisha Mfuko wa Wabunifu unaojulikana kama *Samia Innovation Fund*, ili kusaidia wabunifu kuchochea biashara za ubunifu na kuongeza fursa za ajira. *(Makofi)*

(l) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya; utoaji wa huduma za afya nchini umeendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Sekta Binafsi. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vituo 8,458 mwaka 2020, hadi vituo 9,826 Februari mwaka huu wa 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, idadi ya hospitali zinazotoa huduma ya magonjwa ya dharura zimeongezeka kutoka saba mwaka 2020, hadi 116 mwaka 2025. Pia, vituo vya kutolea huduma za afya vyenye majengo ya mama na mtoto vimeongezeka kutoka 6,081 mwaka 2020, hadi 7,397 Februari 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada hizo, vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua sana kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020, hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kufikia Februari 2025. Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano navyo vimepungua sana, kutoka vifo 67 mwaka 2020 hadi vifo 43 Februari mwaka huu wa 2025. *(Makofi)*

(m) Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia Huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi na hali ya upatikanaji wa dawa na vifaatiba. Huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi zimeendelea kuimarika. Hivi sasa huduma hizo zinapatikana katika hospitali za rufaa za mikoa na zinatoa huduma nane za kibingwa ambazo hapo awali zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya kanda. Huduma hizo ni pamoja na afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, afya ya watoto, magonjwa ya ndani, upasuaji, upasuaji mifupa na ajali, huduma za dharura, huduma za mionzi, huduma za ganzi na huduma za dawa za usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa dawa, vifaatiba na vitendanishi vya kisasa, na bidhaa za afya imeimarika sana kutoka 47% ya mwaka 2020, hadi 89.3% kwa Februari 2025. Mafanikio hayo makubwa yameendelea kuwavutia wagonjwa kutoka nje ya nchi pia na kuimarisha Tibautalii ambapo hadi Februari 2025, wagonjwa 7,843 kutoka nje ya nchi wametibiwa, ikilinganishwa na wagonjwa 5,705 mwaka 2020. *(Makofi)*

(n) Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kueleza kwenye eneo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini. Hali ya upatikanaji wa maji imeendelea kuimarika kutokana na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma ya maji vijijini na mijini. Jumla ya miradi 1,633 imekwishatekelezwa. Kati ya hiyo, miradi 1,335 ni ya vijijini na miradi 298 ni ya mijini. Miradi hiyo imeongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa 70.1% kwa mwaka 2020, hadi wastani wa 79.6% kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mijini, kutoka wastani wa 84% kwa mwaka 2020, hadi wastani wa 90% kwa mwaka 2025. Kutokana na ongezeko hilo, wananchi 12,547,526 wamenufaika na huduma ya maji safi na na yaliyo salama.

(o) Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia idadi ya watalii waingiao nchini. Kutokana na mchango mkubwa wa Sekta ya Utalii katika kuingiza fedha za kigeni nchini na kukuza uchumi na maendeleo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mahususi ili kuhakikisha Sekta hiyo inaendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa letu. Kutokana na umuhimu huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliamua kufanya jitihada binafsi za kutangaza vivutio vya utalii nchini kupitia filamu ya Tanzania ijulikanayo kama '*The Royal Tour*' na '*Amazing Tanzania*'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada hizo zimechangia kuongeza idadi ya watalii kutoka watalii 1,711,625 kwa mwaka 2021, hadi watalii 5,360,247 kufikia mwaka 2024. Kati yao, watalii wa Kimataifa waliongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021, hadi 2,149,895 kufikia mwaka 2024, sawa na ongezeko la 132.24%. Idadi ya watalii wa ndani nayo imeongezeka kwa 307.94%, kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 3,218,352 kufikia mwaka 2024. *(Makofi)*

(p) Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie hali ya ujenzi wa Mji wa Serikali pale Mtumba. Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa Mji wa Serikali unaojumuisha majengo 34. Kati ya hayo, majengo 24 ni ya Wizara na mengine 10 ni ya taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wastani wa hatua za ujenzi wa majengo umefikia 89.7%. Licha ya majengo hayo, pia Seikali imejenga jengo la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi Tanzania katika eneo la Kikombo. Mradi huo unaotekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 534.4, utakapokamilika utawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi na kupendezesha Jiji letu la Dodoma, na hivyo kuwa moja ya vivutio vya utalii hapa Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

(q) Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha Diplomasia ya Kiuchumi; katika kipindi cha Novemba, 2020 – Machi, 2025, Serikali imeimarisha ushiriki wake katika nyanja ya kidiplomasia kwa kujumuisha ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na diplomasia inayozingatia maslahi ya kiuchumi. Katika kipindi hicho, nchi yetu imeshiriki katika mikutano 312 ya Kikanda na Kimataifa na Mikutano 42 ya Tume za Kudumu za Pamoja ambayo imewezesha kusainiwa kwa hati za makubaliano 229. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuimarika kwa uhusiano wa Kimataifa, Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika tarehe 15 Februari mwaka huu wa 2025, Jijini Addis Ababa, Ethiopia, uliichagua Tanzania kuwa Mjumbe wa Kamati ya Uongozi wa Umoja wa Afrika kwa mwaka 2025. Kuchaguliwa huko kwa Tanzania katika nafasi hiyo kutawezesha nchi kunufaika na nafasi za ajira zinazotolewa kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi katika nchi wanachama na kujenga mtangamano imara na wenye maslahi kwa pande zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Agosti, 2024, Serikali iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 44 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika Harare, kule Zimbabwe. Katika mkutano huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya *SADC* ya Siasa, Ulinzi na Usalama, kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Agosti, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikutano na ziara hizo, pamoja na jitihada kubwa za kidiplomasia zinazofanywa na Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, zimeleta mafanikio makubwa kwa nchi yetu. Mafanikio hayo ni pamoja na upatikanaji wa fursa za masoko nje ya nchi, wawekezaji kutoka nje wameendelea kupatikana, misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo nayo pia imeendelea kupatikana pamoja na ongezeko la fursa za ajira na ufadhili wa masomo nje ya nchi ambazo pia zimeendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kuzungumzia utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Baada ya kuainisha baadhi ya mafanikio makubwa ambayo nimeyataja, yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ninaomba nieleze utekelezaji wa shughuli za Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, ambao pia tumeuweka katika vitabu tulivyowapa na tumeuweka pia kwenye vishikwambi vyenu mlivyo navyo. Mimi nitawaongoza kwa kusoma kwa kifupi kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na ukuaji wa uchumi. Mwenendo wa viashiria vya uchumi na bajeti katika mwaka 2024/2025 umeendelea kuwa wa kuridhisha. Katika mwaka 2024, pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa 5.5% ikilinganishwa na 5.1% ya mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la uzalishaji wa umeme, uimarishaji wa huduma za jamii, kuongezeka kwa mikopo kwa Sekta Binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi, kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na kuimarika kwa Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sekta zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji katika kipindi cha mrejeo ni pamoja na shughuli za sanaa na burudani kwa 17.1%, fedha na bima 16.3%, na habari na mawasiliano 14.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei kwa mwaka 2024 umepungua hadi kufikia wastani wa 3.1%, ikilinganishwa na wastani wa 3.8% kwa mwaka 2023. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi na Jumuiya za Kikanda la wigo wa asilimia tatu hadi tano, katika muda wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na bajeti, uwepo wa utoshelevu wa chakula nchini na uboreshaji wa miundombinu ya uchukuzi iliyorahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka maeneo ya uzalishaji hadi kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu akiba ya fedha za kigeni na mwenendo wa ukusanyaji wa mapato inaelezwa zaidi kwenye aya ya 74 hadi aya ya 76 ya hotuba yangu iliyopo kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwekezaji na uendelezwaji wa sekta binafsi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi na kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini. Hatua hizo ni pamoja na kufanya maboresho ya sheria 12 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2024 na kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira na biashara ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeanza maandalizi ya mpango wa pili wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini unaolenga kuvutia uwekezaji wa nje na ndani kwa kuongeza fursa za ajira, uboreshaji wa miundombinu, upatikanaji wa soko la Kimataifa na bidhaa za ndani za kukuza ushindani na ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu uwekezaji na uendelezaji wa sekta binafsi, yanapatikana kwenye hotuba yangu aya ya 80 hadi ya 83 ambayo pia imewekwa kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusimamia utawala wa sheria ambao unazingatia misingi ya utawala bora na haki za binadamu, Serikali imefanya marekebisho ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuinua ustawi wa wananchi. Katika mwaka 2024/2025 sheria Namba 19, kanuni ya 65, amri 116, Notisi 313, sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa 76, matamko mawili na hati idhini moja zilitungwa na kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imekamilisha maandalizi ya sheria ndogo kifani 40 ili kuziongoza Wizara, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uandaaji wa sheria ndogo. Maelezo zaidi kwenye masuala ya upatikanaji wa haki, yanapatikana katika aya 85 hadi 88 kwenye vishikwambi vyenu na kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sekta ya uzalishaji na nianze na Kilimo. Sekta ya Kilimo ni muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini kutokana na mchango wake katika uzalishaji wa ajira na mazao ya chakula, biashara pamoja na malighafi za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuendeleza sekta hii muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Moja ya hatua hizo ni utekelezaji wa programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ambayo inajulikana kama *ASDP*. Tayari Serikali imeshakamilisha mapitio na uhuishaji wa programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili kwa muhula wa mwisho utakaokamilika mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapitio hayo, baadhi ya masuala yaliyobainika ni pamoja na kufikiwa kwa malengo ya awali kwa 66% na kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa programu hiyo na mikakati inayolenga kuitekeleza ili kuimarisha Sekta ya Kilimo. Hii ni pamoja na kuimarisha uratibu wa programu, kuweka mkazo kwenye masuala ya hifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu, kuongeza nguvu katika utekelezaji wa afua za kuongeza usalama wa chakula na lishe na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama wa chakula, sambamba na utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati madhubuti ya kuendeleza sekta ya kilimo. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa mbegu na pembejeo za kilimo, kutoa mikopo ya kilimo kwa wananchi, kuanzisha skimu za umwagiliaji na kusimamia ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendelea kujitosheleza kwa chakula kwa 125%. Utoshelevu huo unatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 20.4 katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 hadi tani milioni 22.8 msimu wa mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limetokana na ongezeko la matumizi ya mbolea iliyotolewa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na pia kuongezeka kwa mtandao wa kilimo cha umwagiliaji, kuimarika kwa huduma za ugani, na vilevile matumizi ya mbegu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa mbolea nchini imeendelea kuimarika ambapo hadi tarehe 31 Januari mwaka huu 2025 kulikuwa na jumla ya tani milioni 1.21 sawa na 80.9% ya makisio ya mahitaji ya tani milioni 1.5 za mbolea kwa msimu wa mwaka 2024/2025. Aidha, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2024/2025 tani 388,619.87 za mbolea yenye ruzuku ya thamani ya shilingi bilioni 131.66 imeshasambazwa kwa wakulima 4,223,278.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake kupata mitaji na pembejeo, pia kuwahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, sukari, chai pamoja na zao la mchikichi lililopo Mkoani Kigoma; kujenga na kugharimu gharama za kuhifadhi mbolea na kuendelea na mpango wa utoaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi ya huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, mikopo ya kilimo na maendeleo ya ushirika yanapatika aya ya 94 mpaka ya 98 kupitia hotuba yangu na kwenye vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo. Sekta ya mifugo imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Serikali kwa kutambua umuhimu wa mifugo hapa nchini imeendelea kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za mifugo, kuimarisha huduma za ugani na kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayovuka mipaka. Katika kipindi cha

Julai, 2024 hadi Januari, 2025 Serikali imenunua chanjo zenye thamani ya shilingi bilioni 10.1 kwa ajili ya mifugo na hasa kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo, lakini pia imetoa chanjo kwa mifugo zaidi ya milioni 370 dhidi ya magonjwa kipaumbele ikiwemo kimeta na homa ya mapafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchanjaji wa mifugo unaifanya Tanzania kukidhi matakwa ya viwango vya Kimataifa katika biashara ya mifugo na mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada zilizofanyika katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 uzalishaji wa mifugo umeongezeka hadi milioni 189.8 kutoka mifugo milioni 181.8 kwa mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama kutoka tani 963,856.55 mwaka 2023/2024 hadi tani 1,054,114.03 kufikia Februari mwaka huu 2025. Thamani ya nyama iliyozalishwa imeongezeka kutoka shilingi trilioni 7.71 mwaka 2023/2024 hadi shilingi trilioni 8.43 Februari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itendelea kuimarisha miundombinu na huduma za chanjo ya mifugo, itajenga na kukarabati minada ya mifugo, itajenga machinjio ya kisasa na kujenga mashamba darasa ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali kuimarisha ufugaji bora na wa kisasa yanapatikana katika aya 100 mpaka aya 101 ya hotuba yangu na tumeweka pia kwenye vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuweka mkazo katika ukuaji wa sekta ya uvuvi kwa kuboresha miundombinu, kuweka mazingira wezeshi katika uzalishaji wa samaki na biashara ya mazao ya uvuvi na kuimarisha kilimo cha mwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada hizo, kati ya Julai, 2024 hadi Februari, 2023 jumla ya tani 352,004.55 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.36 zilivunwa ikilinganishwa na

tani za samaki 323,856.83 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.92 zilizovunwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa bandari za uvuvi kule Kilwa Masoko Mkoani Lindi, kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi kule Wilayani Bagamoyo na kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na ugani hapa nchini. Maelezo zaidi kuhusu uwezeshaji wa wananchi na ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa Masoko na pia Bagamoyo yanapatikana katika aya ya 105 mpaka 106 kwenye hotuba yangu na kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maliasili na utalii. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kukuza utalii na kuendeleza maliasili zilizopo hapa nchini ili kuiwezesha nchi kupata mapato na kukuza ustawi wa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 tumeshuhudia ukuaji wa utalii, wa mikutano na matukio mbalimbali, ambapo mikutano hiyo ya Kimataifa ilifanyika nchini ikiwemo Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika Januari, 2025. Kadhalika jukwaa la pili la utalii wa chakula duniani Kanda ya Afrika lililoandaliwa na Shirika la Utalii Duniani linatarajiwa kufanyika hapa nchini katika mwezi huu wa Aprili mwaka huu wa 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali yetu itaendelea kutangaza utalii wa ndani na utalii wa nje huko nje ya nchi, tutaibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati na kuimarisha usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za kitalii na uhifadhi. Maelezo zaidi ya fursa na tuzo za utalii yanapatikana katika aya 109 mpaka aya 110 kwenye hotuba yangu na kwenye vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini imeendelea kukua na imeendelea kuimarika kutokana na mikakati mbalimbali inayotekelezwa ambayo imechagiza kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na kuongeza pato la Taifa letu. Mikakati hiyo ni pamoja na ugunduzi wa maeneo mapya ya uchimbaji, kuendeleza madini muhimu ya kimkakati lakini pia tunahamasisha uwekezaji, uanzishaji minada na maono ya madini ya vito,

uongezaji thamani ya madini, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili, maelezo kuhusu leseni za wachimbaji na madini, mapato yaliyokusanywa na utoaji hati kwa wachimbaji wadogo yanapatikana katika aya 112 hadi 115 ya hotuba yangu na iliyopo kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya nishati ya umeme, Serikali imeendelea kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa uhakika na unaokidhi mahitaji na shughuli za kiuchumi na kijamii. Hadi Machi, 2025 kiwango cha umeme uliounganishwa katika gridi ya Taifa ni *Megawatt* 4,031.44 ikilinganishwa na *Megawatt* 1,889.84 za Februari mwaka 2024. Ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya kuzalisha umeme, ikiwemo mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere *Megawatt* 2115 na kule Rusumo Nyakanazi *Megawatt* 26.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme na kuwafikia wananchi, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Hadi Februari, 2025 njia ya kusafirisha umeme imeongezeka na kufikia urefu wa kilometa 8,025.38 kutoka kilometa 7,745.38 zilizokuwepo kufikia mwaka jana, 2024. Vilevile njia za kusambaza umeme zimeongezeka na kufikia urefu wa kilometa 198,215.17 ikilinganishwa na kilometa 176,334.14 ambazo zilikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliendelea na utekelezaji wa shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi asilia, ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2025 wastani wa kiasi cha gesi asilia kilichozalishwa nchini kilikuwa futi za ujazo milioni 177.18 kwa siku. Kiasi cha gesi hiyo kilitoka katika vitalu vya Songosongo futi za ujazo 87.78 na kule Mnazi bay Mtwara futi za ujazo 89.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kasi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za gesi asilia unaendelea na unatarajiwa pia kuchochea zaidi matumizi ya gesi asilia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, gesi na mradi wa kupeleka nishati ya umeme ambao pia utakwenda mpaka kwenye vitongoji vyote Tanzania Bara, miradi ya kielelezo ya kimkakati ya mafuta na gesi asilia nayo pia itatekelezwa. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijiji. Maelezo zaidi kuhusu vibali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za gesi yanapatikana katika aya ya 119 ya hotuba yangu na kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha matumizi bora ya ardhi, Serikali inaendelea kusimamia mpango wa kupima na kupanga na kumilikisha ardhi hapa nchini. Lengo ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, kuipa thamani ardhi kuwa mtaji kwa wananchi, kuwawezesha kukopesheka na kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha imepima viwanja 7,550 katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma na Njombe. Kuhusu upangaji wa miji, michoro ya mipango miji yenye viwanja 126,935 iliidhinishwa na hati miliki za viwanja 3,569,994 imebadilishwa kuwa za kidigitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, kuandaa na kumilikisha mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vilivyosalia na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi wa kazi, ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kwenye eneo hili la ardhi mfumo wake wa utunzaji wa taarifa za ardhi, miradi ya ujenzi wa nyumba yanapatikana kwenye aya ya 122 hadi 124 ya hotuba yangu na kwenye vishikwambi mlivyonavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia maendeleo ya viwanda vya biashara. Ili kupunguza utegemezi wa bidhaa

kutoka nje ya nchi, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya uanzishaji wa viwanda hapa nchini, jumla ya leseni za viwanda 225 na vyeti vya usajili vya viwanda 29 vimeshatolewa. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na sukari inayotosheleza kupitia viwanda vilivyojengwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki kilichozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siku ya tarehe 7 Agosti, 2024. Kiwanda hiki kinao uwezo wa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka. Tayari kiwanda hicho kimeshazalisha tani 19,124 za sukari za majumbani tangu kuanza rasmi uzalishaji Julai, 2024 na kimetoa ajira rasmi 2,172 na zisizo rasmi zaidi ya 8,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya kimkakati, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi, utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutaendelea kuhamasisha uanzishaji unaozingatia viwango vya Kimataifa, tutaongeza uwezo wa mifumo ya masoko nchini ikiwa ni pamoja na mfumo wa stakabadhi za ghala. Vile vile tutatumia fursa ya diplomasia ya uchumi kupata masoko mengi zaidi katika nchi mbalimbali rafiki huko duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina yanayohusu viwanda vilivyoanzishwa, ujenzi wa kongani ya Kwala na maandalizi ya mkakati wa Kitaifa wa utekelezaji wa mkataba wa soko huru la Afrika yanapatikana katika aya ya 128 hadi 131 kwenye hotuba yangu na kwenye vishikwambi tulivyowagawia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Usafiri na Usafirishaji. Serikali imeendelea kufanya utanuzi wa mtandao wa barabara ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025, barabara zenye urefu wa kilometa 246 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 1,494.62 kwa kiwango cha changarawe. Aidha,

imefanya matengenezo ya barabara kilometa 3,107.38 kwa kiwango cha lami na kilometa 5,193.09 kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kutatua changamoto ya msongamano wa magari na kuboresha mfumo wa huduma za usafiri na usafirishaji katika majiji yenye msongamano kama vile Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Dar es Salaam, awamu ya tatu ya ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka kutoka Posta hadi Gongolamboto, yenye kilometa 23.3 umefikia 80%, na awamu ya nne ya ujenzi wa Barabara ya Kivukoni hadi Tegeta yenye urefu wa kilometa 30.1 umefikia 22.2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jiji la Dodoma, Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje yenye urefu wa kilometa 112.3. Pia, ujenzi wa sehemu ya kwanza kutoka Nala - Veyula - Mtumba - Ihumwa mpaka Bandari Kavu yenye urefu wa kilometa 52.3 umeshafikia 84.72% na kwa sehemu ya pili, kutoka Ihumwa Bandari Kavu - Mtumba – Matumbulu - Nala yenye urefu wa kilometa 60 umefikia 81.5%. Kule Jiji la Mbeya, ujenzi wa njia nne za barabara kutoka Nsalaga (Uyole) mpaka Ifisi (Kiwanja cha Ndege cha Songwe) yenye urefu wa kilometa 29 umefikia 22%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2025/2026, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara zinazounganisha Makao Makuu ya mikoa, nchi jirani pamoja na barabara za ulinzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo miundombinu ya vivuko na madaraja ili kuunganisha maeneo ya nchi kavu ambayo yametenganishwa na maji katika maeneo ya bahari, maziwa na mito.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi ya miradi ya dharura ya miundombinu yanapatikana katika aya ya 136 mpaka aya ya 137 za hotuba yangu na kwenye vishikwambi vyenu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Uchukuzi, kwa upande wa viwanja vya ndege, Serikali yetu ya Awamu ya Sita imedhamiria kuhakikisha huduma ya usafiri wa anga inaimarika na kuleta manufaa kwa wananchi kwa kuendeleza ujenzi wa viwanja katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Viwanja hivyo ni pamoja na Kiwanja cha Ndege kule Tabora ambacho kimeshafikia 90%, Kiwanja cha Ndege Mkoani Shinyanga 76%, Kiwanja cha Ndege cha Musoma kilichofikia 57%, Kiwanja cha Ndege Sumbawanga kimefikia 50% na Kiwanja cha Ndege Kigoma 16%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa ambao umefikia 93% ya utekelezaji wake na tayari safari za ndege kwenda Mkoa wa Iringa zimeshaanza. Aidha, kwa upande wa kiwanja cha ndege cha Arusha, ujenzi wa jengo la abiria, ufungaji wa mifumo ya TEHAMA umekamilika; na ufungaji wa taa za kuongozea ndege utakaowezesha kiwanja hicho kutoa huduma kwa saa 24 unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu uimarishaji wa usafiri wa anga, pamoja na ujenzi wa viwanja vya ndege yanapatikana zaidi katika aya ya 140 na 141 kwenye hotuba yangu. Pia tumeweka kwenye vishikwambi vyenu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usafiri wa njia za maji katika maziwa makuu, Serikali imeendelea kufanya maboresho kwa kukamilisha ukarabati wa Bandari ya Kemondo. Vilevile, inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Bandari ya Bukoba ambapo utekelezaji wake umefikia 85%, Bandari ya Mwanza *North,* 48% na Bandari ya Mbambabay 20%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi

wa reli ya kati kwa kiwango cha kimkakati, kuimarisha miundombinu ya bandari, kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania, ukarabati wa meli zilizopo na ujenzi wa meli mpya na kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi ya Mradi wa Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala na maeneo ya uimarishaji wa viwanja vya ndege na bandari, yanapatikana katika aya ya 143 ya hotuba yangu. Pia, tumeweka kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa. Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kutoa taarifa kupitia tafiti za kisayansi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa. Uwepo wa rada katika Mikoa ya Mbeya na Kigoma umewezesha nchi yetu kuwa na jumla ya rada tano za hali ya hewa zinazosaidia kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Serikali katika kukabiliana na kasi ya maendeleo ya mawasiliano na teknolojia, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha nchi yetu inanufaika na maendeleo hayo ya teknolojia. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hadi kufikia Februari, 2025 kilometa 13,820 kati ya 16,280 zimejengwa na kuunganisha wilaya 109 kati ya wilaya 139 pamoja na vituo 111 vya kutolea huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imeanza kuchukua hatua za utekelezaji wa ujenzi wa mkongo wenye urefu wa kilometa 186 kutoka Kigoma Tanzania hadi Kalemie, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* kupitia Ziwa Tanganyika. Aidha, jitihada hizo zimeenda sambamba na kuimarisha utoaji wa huduma za mawasiliano pamoja na ujenzi wa minara. Tayari minara 414 imeshajengwa, sawa na 54.62% ya minara 758 inayotarajiwa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali yetu itaendelea kuweka kipaumbele katika kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali, itaendelea kuboresha na kuhuisha mifumo ya TEHAMA jumuishi, mifumo ya kisekta na mifumo ya kitaasisi inayotumika. Itadhibiti usalama wa Taarifa za Serikali dhidi ya matishio ya kiusalama mtandaoni kwa kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao, itaimarisha tathmini ya hali ya usalama mtandaoni pamoja na upatikanaji huduma za mawasiliano ya simu na posta hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, Seirkali itaweka mazingira wezeshi kwa ajili kukuza na kuimarisha biashara mtandaoni, kuchochea ubunifu, kuimarisha ustawi wa kampuni changa na kuendeleza utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo zaidi juu ya mawasiliano na teknolojia ya habari na kuhusu kuunganisha mifumo ya TEHAMA na kuimarisha mfumo wa anwani za makazi, yanapatikana katika aya ya 148 hadi 150 za hotuba yangu. Pia, tumeweka kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za jamii, nianze na Sekta ya Elimu. Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuimarisha sekta ya elimu hapa nchini kwa kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora yenye tija inayokidhi mahitaji ya soko la ajira inaimarika. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha sera na mitaala, kuongeza fursa za elimu ya amali, msingi, sekondari, ualimu na elimu ya juu, pamoja na kuendeleza utafiti na matumizi ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imeandaa na kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023), pamoja na Mitaala ya Elimu Ngazi ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono haya makubwa yenye lengo la kufanya elimu inayotolewa hapa nchini, iwiane na mahitaji ya sasa Kitaifa, kikanda na Kimataifa na pia, kuendana na mabadiliko na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali, kununua vifaa vya kufundishia kwa vyuo vya *VETA* na vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, kuendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi na kuongeza mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya kati na elimu ya juu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kuimarisha mafunzo kwa walimu, kuongeza uwiano wa vitabu kwa wanafunzi na kuimarisha elimu maalum, kuongeza bajeti ya fedha za mikopo na ufadhili wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi ya kuimarisha utaoji wa elimu ya msingi, sekondari, elimu ya kati, elimu ya juu, yanapatikana katika aya ya 154 hadi 159 ya hotuba yangu. Tumeweka pia kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Maji, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ambayo nimeeleza awali, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Same – Mwanga – Korogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Miradi ya Mugango – Kiabakari – Musoma na kukamilika kwa uchimbaji wa visima 925, ambapo kila Jimbo la Uchaguzi Tanzania Bara limepata wastani wa visima vitano vya maji. Katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kukamilisha miradi mikubwa ya maji, kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika utekelezaji na uendeshaji wa miradi ya maji na kuimarisha utafutaji, ufuatiliaji wa ubora wa maji yanayotumiwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Maji ya kwenye Miji 28 na Bwawa la Kidunda pamoja na miradi mingine ya visima, yanapatikana katika aya ya 162 na 163 za hotuba yangu. Tumeweka pia kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za afya, Serikali imeendelea kutekeleza mipango na mikakati mahsusi ya kusimamia ubora, usalama na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha huduma za

kinga, huduma za afya ya uzazi na mtoto, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya, pamoja na kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi. Vilevile, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya, mifumo ya TEHAMA ambayo itawezesha utoaji wa huduma za afya na matumizi ya takwimu na utawala bora, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026, itaendelea kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa, itaimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya ambazo zinazotolewa hapa nchini na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tutaimarisha mifumo ya ugharimiaji wa huduma za afya nchini, uimarishaji wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, uimarishaji wa huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini na kusimamia tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya, lakini pia, kuendelea na hamasa ya kuanzisha mfuko wa bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo muhimu kuhusu utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa utoaji wa huduma za afya, yanapatikana kwenye aya ya 166 na 167 kwenye hotuba yangu na pia, kwenye vishikwambi tulivyowapa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, watu 1,536,842 kati ya watu 1,690,948 ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) walikuwa wanatambulika na hali zao za maambukizi. Kadhalika, WAVIU 1,545,880 wanatumia dawa za kufubaza makali ya VVU ambapo watu wazima wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ni 96.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha maambukizi mapya ni watu 60,000 kila mwaka, ambapo vijana wanaopata VVU maambukizi ni takribani 34.3% ya maambukizi mapya. Nitoe rai

kwa Watanzania wote kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa UKIMWI bado ni tishio kama takwimu zinavyoonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itaendelea kuratibu shughuli za UKIMWI kwa kutoa huduma endelevu na stahimilivu kwa WAVIU, kuimarisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI, ili uweze kufanikisha malengo ya nchi katika kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030. Pia, tutaweka msukumo katika kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, tutahamasisha mabadiliko ya tabia katika jamii, ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, Serikali inatambua mabadiliko ya kisera kutoka kwa baadhi ya washirika wetu wa muda mrefu wa masuala ya UKIMWI. Kufuatia mabadiliko hayo, Serikali inachukua hatua madhubuti kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha uwekezaji kwenye eneo la utaoji huduma kwa WAVIU.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizo zenye lengo la kuwezesha Taifa letu kujitegemea zitaendelea kuchukuliwa pia, katika maeneo mengine. Niwahakikishie Watanzania wote kuwa, Serikali itaendelea kuhakikisha huduma zinazohusiana na masuala ya UKIMWI zinaendelea kupatikana na hakuna Mtanzania hata mmoja ambaye atakaweza kukosa huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma kwa makundi maalum, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali kwa kushirikiana na wadau wote muhimu imeendelea kuhamasisha ushiriki wa jamii katika maendeleo, kukuza usawa wa kijinsia, kuimarisha huduma za ustawi wa jamii pamoja na kuendeleza makundi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinazofanywa na Serikali ni katika kuhakikisha uwepo wa elimu kuhusu maendeleo ya jamii, ushiriki wa kila mwananchi katika kulinda misingi ya maisha inayozingatia tamaduni sahihi, malezi bora na kutunza amali za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua mojawapo iliyochukuliwa ni kuimarisha mifumo ya kisheria kwa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mtoto Sura ya 13, ili kuboresha mifumo ya haki na ulinzi wa watoto. Aidha, katika kuhakikisha malezi bora, Serikali imeratibu mafunzo kwa maafisa 281 wa mikoa na halmashauri kuhusu sayansi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuimarisha ulinzi wa mtoto na makundi maalum, utoaji wa huduma ya afya kwa wazee na utoaji wa huduma za ustawi wa jamii. Vilevile, itaendelea kuwatambua na kuwaendeleza wafanyabiashara ndogo ndogo na kuboresha mazingira ya kujifunzia katika vyuo vya ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo muhimu kwenye idara hii ya huduma za makundi maalum, usalama wa watoto, uratibu wa makundi maalum na mashirika yasiyo ya Serikali, tumeyaweka kwenye aya ya 175 na 178 kwenye hotuba yangu. Vilevile tumeweka kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hali ya siasa na demokrasia hapa nchini. Hali ya siasa na utekelezaji wa demokrasia hapa nchini imeendelea kuimarika na hii nikutokana na maboresho ya mifumo na jitihada mbalimbali za makusudi zinazofanywa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jitihada hizo ni marekebisho ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utawala wa demokrasia hapa nchini. Aidha, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 1 ya Mwaka 2024, vilevile Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 2 ya Mwaka 2024 na kufanya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Serikali kwa upande wake tayari imeshakamilisha utungaji wa Kanuni za Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeendelea kufanya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa

Mwaka 2025 kwa kuratibu na kusimamia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura. Hadi Machi, 2025 uboreshaji awamu ya kwanza umekamilika katika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar na maandalizi ya awamu ya pili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutoa rai kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza kuhakiki taarifa zao kwenye daftari kabla ya kuhitimishwa kwa awamu ya pili ya uboreshaji inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, hadi kufikia Machi, 2025, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 13.17 kwa vyama vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku. Hatua hiyo, imeendelea kusaidia kuimarisha na kuendeleza uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia Baraza la Vyama vya Siasa imetoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa vyama vya siasa ili kukuza uelewa juu ya uendeshaji wa vyama vya siasa huku tukielekea kwenye uchaguzi ambao utafanyika mwaka huu wa 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uratibu wa shughuli za Serikali hapa Bungeni. Katika mwaka 2024/2024 Ofisi ya Bunge imeendesha mikutano mitatu ya Bunge, yaani Mkutano wa Kumi na Sita, Kumi na Saba na Kumi na Nane; na katika mikutano hiyo jumla ya maswali ya msingi 546 na maswali ya nyongeza 1,725 yaliulizwa Bungeni na kupatiwa majibu na Serikali; na maswali 25 ya papo kwa papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kuhusu miswada, maazimio ya Bunge na aina ya maswali yaliyoulizwa yote yanapatikana kwenye aya ya 184 ya hotuba yangu na tumeweka pia kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulinzi na usalama; sambamba na utulivu wa kisiasa hapa nchini, hali ya usalama na

amani imeendelea kuimaraika nchini kwetu na katika mipaka yote kwa Tanzania imeimarika, na maeneo yote yanayohusu eneo la nchi kavu na eneo la maji nako pia tumeimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, navipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa jitihada zao kubwa wanazoendelea kuchukuwa ili kuhakikisha kwamba hali ya ulinzi na usalama, amani na utulivu ndani ya nchi vinaendelea kuimarika hapa nchini. Jitihada hizo zimechangia kuleta sifa ya kidiplomasia ya nchi yetu na kukuza shughuli za kiuchumi na kijamii ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha jeshi la ulinzi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa pamoja na kushiriki katika misheni za kikanda na Kimataifa katika masuala ya ulinzi na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa wafungwa na mahabusu kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na utekelezaji wa mapendekezo ya tume ya haki jinai, kuendelea kuzuia makosa na jinai na kuimarisha huduma za Jeshi la Polisi, kuendelea kutosheleza vitendea kazi, kujenga na kukarabati miundombinu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kuendelea kuboresha miundombinu ya mfumo wa uhamiaji kwa kuzingatia viwango vya teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kwenye eneo hili kuhusu ushiriki wa vyombo vyetu katika oparesheni za amani na ulinzi, mafunzo ya ukakamavu kwa vijana, usalama wa raia, taadhari dhidi ya moto, huduma za ukazi na utambulisho yanapatikana katika aya ya 186 hadi 198 ya hotuba yangu, na tumeweka pia kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutambua umuhimu wa wafanyakazi katika kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, Serikali imeendelea kuchukuwa hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ushughulikiaji maslahi ya wafanyakazi, kuwajengea uwezo, pamoja na kuwapatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mifumo, Serikali imefanya maboresho ya Sheria za Ajira na Uhusiano Kazini Sura 396, Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300 na Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 ili kukidhi mahitaji ya sasa. Moja ya marekebisho makubwa yaliyofanyika ni pamoja na kuboresha haki ya likizo ya uzazi kwa mama aliyejifungua mtoto njiti. Hivi sasa likizo ya uzazi wa mama atakayejifungua mtoto njiti itaanza baada ya mtoto kufikisha wiki 40 badala ya wiki 36 iliyokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile umeandaliwa mfumo wa kielekroniki *OCMS* unaolenga kuimarisha shughuli za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi unaohusiana na mgogoro ya kikazi kwa njia ya kidijitali. Mfumo huo utarahisisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya kupunguza muda wa gharama na hivyo kuongeza ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 Serikali imepandisha vyeo watumishi 290,625 wa kada mbalimbali. Pia, imelipa fedha, kiasi cha shilingi bilioni 130.4 kwa watumishi wa umma 100,684 waliokuwa na madai mbalimbali Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itafanya kaguzi 350,000 katika maeneo 25,000, kupima afya za wafanyakazi 400,000 na kutoa mafunzo kwa waajiri na wafanyakazi na wajasiriamali wapatao 40,000. Maelezo ya ndani kabisa kuhusu hatua za kupunguza migogoro kazini, kaguzi zilizofanywa, vibali vya ajira kwa wageni na usalama na afya mahali pa kazi yanapatikana katika aya ya 200 hadi 204 kwenye hotuba yangu na kwenye vishikwambi tulivyowapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maendeleo ya vijana, Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, waweze kujipatia pia ajira na kujikwamua kiuchumi. Katika mwaka 2024/2025, Serikali imezindua Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, Toleo la 2024 pamoja na mkakati wake. Sera hiyo imezingatia mazingira na mahitaji ya vijana ikiwemo elimu, ujuzi kwa vijana, uvumbuzi na ubunifu kwa vijana, vijana na mapinduzi

ya kidijitali, ajira kwa vijana nayo imechukuliwa kwa umuhimu wake na ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi nayo imeendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2025/2026, Serikali itatekeleza programu za stadi za maisha, malezi na makuzi na uratibu wa maendeleo ya vijana, na kuendelea kuhamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuweza kujipatia ajira na kuinua kipato chao wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia huduma kwa watu wenye ulemavu. Katika kuboresha utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha jamii ya watu wenye ulemavu inaishi katika mazingira salama na kushiriki katika shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyofahamu, Serikali imezindua Mpangokazi wa Taifa wa Ustawi na Haki kwa Watu Wenye Ualbino kwa Mwaka 2024/2025 – 2028/2029. Mpangokazi huo, unaainisha hatua zinazohitajika katika kuzuia, kukabiliana na kutokomeza kabisa ukatili kwa watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali ilizindua Mkakati wa Taifa wa Teknolojia Saidizi 2024 /2027 ambao unatoa mwongozo wa kimkakati kwa sekta zote kuweka mazingira wezeshi ili kila Mtanzania mwenye uhitaji wa teknolojia saidizi aweze kupata kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ilizindua Kanzidata na Mfumo wa Taarifa za Watu Wenye Ulemavu unaotokana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 utakaowezesha matumizi ya takwimu ya sensa katika kutayarisha programu za kuwawezesha na kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu. Uwezo huo ni wa kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali na wadau wa maendeleo katika kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2025/2026, Serikali yetu itaendelea kuratibu utoaji wa huduma

kwa watu wenye ulemavu na hasa katika kuboresha na kutekeleza sera, sheria, mikakati na mipango mbalimbali ya Kitaifa, kikanda na Kimataifa inayolenga kuwawezesha watu wenye ulemavu kuweza kumudu kufikia malengo yao kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuimarisha ushiriki wao katika nyanja zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie huduma za kinga ya jamii. Huduma ya kinga ya jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Huduma hiyo imekuwa ikitolewa kwa wananchi ambao ni watumishi walioko kazini, waliostaafu na kaya maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2025 huduma imetolewa kwa wananchi wasiopungua milioni 16,506,583 kwa huduma ya kinga ya jamii ya uchangiaji na isiyo ya uchangiaji. Aidha, Serikali imeandaa mfumo wa uratibu wa kinga ya jamii ambao utarahisisha uratibu na utekelezaji wa afua za kinga ya jamii kwa kuwaleta pamoja wadau wanaohusika katika masuala ya kinga ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itaendelea kuboresha na kusimamia programu na mikakati mbalimbali ya kinga ya jamii nchini ikiwemo kulipa mafao ya wastaafu kwa wakati na kutoa elimu ya mpango wa kinga ya jamii kwa wananchi hususan kwenye sekta isiyo rasmi. Maelezo zaidi ya nyongeza ya kima cha pensheni, utendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na Usajili wa Wanachama yanapatikana katika aya ya 213 hadi 216 ya hotuba yangu, na kwenye vishikwambi pia tumeweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, na nikianza na mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa chini ya taasisi yetu ya *TASAF*. Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini awamu ya tatu kwa maeneo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi bilioni 106.3 zimehawilishwa kwa kaya za walengwa 926,054. Vilevile, Serikali imeboresha mfumo wa malipo kwa kaya za walengwa 428,570. Mfumo unaotumika sasa ni wa

malipo ya kielektroniki ambapo baada ya kuzisajili kaya hizo malipo ya fedha hutumwa moja kwa moja kupitia mitandao ya simu na benki ambako wamefungua akaunti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itaendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuzihudumia kaya za walengwa zilizopo kwenye mpango kupitia utoaji wa ruzuku ili ziweze kukidhi mahitaji yao ya msingi; pia kutoa fursa za ajira ya muda kwa kaya za walengwa ili kuongeza kipato kwa kushiriki katika kufanya kazi katika miradi iliyoibuliwa na jamii; na kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupitia Mfuko wa Asilimia Kumi uliopo kwenye majiji, halmashauri za miji na wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu uwezeshaji kaya lengwa, mfumo wa kielekroniki wa utaoji wa mikopo ya 10% thamani ya mikopo iliyotolewa pamoja na manufaa yake tumeyaweka katika aya ya 219 hadi 222 ya hotuba yangu, ambayo pia tumeiweka kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050. Ni ukweli usiopingika kuwa mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu ni muhimu kwa mwelekeo wa nchi. Kwa msingi huo, Serikali iliendelea kufanya maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kufikia mwaka 2050 ambayo itatoa mwongozo wa mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa maandalizi ulihusisha kukusanya maoni ya wadau mbalimbali pamoja na wananchi na hatimaye kukamilisha Rasimu ya Dira 2050 iliyozinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasimu hiyo imezingatia ukuaji wa uchumi utakaofungamanishwa na sekta za uzalishaji, uimarishaji wa sekta binafsi, na kuimarisha uwekezaji na usimamizi katika Mashirika ya umma. Sambamba na dira hiyo, Serikali imeanza maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 ambao utakuwa mpango wa kwanza katika utekelezaji

wa Dira 2050 na Mpango wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mapambano dhidi ya rushwa. Rushwa ni adui wa haki. Kutokana na ukweli huo, Serikali ya imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ili kuhakikisha kunakuwa na usawa katika kutoa na kupokea huduma pamoja na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za Serikali zinalenga kuimarisha eneo la uzuiaji rushwa ili kudhibiti vitendo hivyo kabla na wakati havijafanyika katika maeneo ya kutolea huduma. Hatua za udhibiti zinatekelezwa sambamba na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya rushwa yanaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha 2025/2026, Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi. Kipaumbele kitawekwa katika utoaji wa elimu kwa umma juu ya madhara ya rushwa, kuchambua na kubainisha maeneo yanayohitajika kuimarishwa kwenye mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma, na kuendeleza uchunguzi na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wa makosa ya rushwa. Taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa katika mapambano ya rushwa na taarifa ya '*transparency international*' tumeiweka katika aya ya 227 hadi 228 ya hotuba yangu, na kwenye vishikwambi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie tatizo la matumizi ya biashara ya dawa za kulevya hapa nchini. Tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini na duniani kwa ujumla limekuwa likiongezeka na kusababisha athari nyingi kwa wananchi hususan kwa kundi la vijana. Hivyo basi, udhibiti wa dawa za kulevya ni muhimu ili kulinda vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa inayoathirika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ni muhimu katika kuongeza afya ya jamii kwa kupunguza uraibu na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, kuongeza amani na usalama kwa kupunguza uhalifu, pamoja na kuimarisha sifa za Taifa letu Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 itaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha malengo ya kudhibiti na kutokomeza dawa za kulevya yanafikiwa kwa kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya, kutekeleza afua za kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini, na kuboresha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa. Taarifa kuhusu mafanikio katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya na mashamba ya bangi yaliyotekezwa inapatikana katika aya ya 231 hadi 232 za hotuba yangu ambayo pia tumeiweka kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uratibu wa maafa. Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuhakikisha kuwa shughuli za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali kutokana na maafa zinatekelezwa tena kikamilifu. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya kisera kwa kufanya maboresho yanayolenga kuboresha ufanisi katika usimamizi wa maafa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2004, na kutoa toleo jipya la Sera hiyo la mwaka 2024. Aidha, imeandaa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa pamoja na mikakati ya kupunguza vihatarishi vya maafa kwenye Halmashauri za Kibiti, Monduli, Simanjiro, na Longido. Mipango hiyo, itasaidia halmashauri husika kujiandaa na kukabiliana na maafa pindi yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau, imetekeleza programu ya urejeshaji hali kwa kujenga nyumba 109 katika eneo la Waret, Wilaya ya Hanang kutokana na athari za maporomoko ya udongo yaliyotokea mwaka 2023. Nyumba hizo tayari zimekabidhiwa kwa walengwa. Nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika kukabiliana na kurejesha hali kule Hanang kutokana na maafa yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kukabiliana na maafa kwa kuendelea kutumia tafiti na taarifa za kisayansi

zinazotoa viashiria vya kutokea kwa maafa katika maeneo mbalimbali, kutoa elimu ya utayari wa kukabiliana na maafa kwa wananchi, kuimarisha vitengo vya uokoaji pamoja na Kamati za Uratibu wa Maafa kutoka ngazi za vijiji, kata, halmashauri mpaka mikoa. Maelezo zaidi kuhusu operesheni za maafa zilizofanywa, maandalizi yaliyotokana na tafiti tumeyaweka katika aya ya 235 ya hotuba yangu na kwenye vishkwambi vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uratibu wa masuala ya lishe. Maendeleo ya Taifa lolote pamoja na mambo mengine, yanahitaji uwepo wa watu (nguvu kazi) wenye afya njema na waliopata lishe bora ili kuwawezesha kufanya kazi kwa bidii na tija. Rasilimaliwatu imara ndiyo msingi wa kuzalisha kwa tija na kupunguza umaskini. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026, tutafanya tafiti mbalimbali za kisayansi kuhusu masuala ya lishe, tutaratibu vikao vya majadiliano na kushirikiana na wadau mbalimbali wa lishe, na kuimarisha mazingira wezeshi ili kuwezesha wadau katika ngazi zote kwa nafasi zao kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa afua za lishe. Taarifa kuhusu tafiti za lishe inapatikana katika aya ya 239 ya hotuba yangu na kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kwa kifupi juu ya mazingira. Serikali imeendelea kuweka msisitizo kuhusu suala la uhifadhi na utunzaji wa mazingira kwa kutoa tathmini ya kina ya hali ya mazingira nchini. Tathmini hiyo imefanyika katika maeneo makuu ikiwemo rasilimali za maji, mifumo ikolojia ya ardhi oevu, kilimo, misitu na wanyamapori, na mabadiliko ya tabianchi. Tathmini hiyo imebaini uwepo wa mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na athari zake katika ustawi wa binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira ili kukabiliana na changamoto za hifadhi ya mazingira pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji

wa programu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Taarifa zaidi za mazingira na uhifadhi wake na usimamizi tumeweka kwenye aya ya 242 kwenye hotuba yangu na kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi uchumi wa bluu. Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu ya Mwaka 2024 pamoja na mkakati wake. Hapa lengo ni kuboresha mfumo wa uratibu ili kuwezesha rasilimali na fursa za maji kuwa zinachangia kikamilifu katika pato la Taifa na kuongeza fursa za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka uliopita 2024/2025, mkazo uliwekwa katika ukuaji wa sekta mbalimbali zenye mnasaba na uchumi wa bluu ikiwemo uvuvi, uchukuzi, maji, nishati, madini, maliasili na utalii. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya uvuvi, kukuza uzalishaji wa samaki pamoja na biashara ya mazao ya uvuvi, kufanya marekebisho ya miundombinu ya usafirishaji majini na huduma za bandari katika ukanda wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kufanya utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia, kukuza utafiti na suala la utalii pia kwa bahari pamoja na kuendeleza uchimbaji wa madini baharini pamoja na kilimo cha baharini. Hivyo, kuchochea maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao, 2025/2026, Serikali itaendelea kutekeleza na kuimarisha uratibu wa shughuli za uchumi wa bluu kwa kuhamasisha matumizi ya maeneo ya maji, uwekezaji wa kimkakati na fungamanishi katika matumizi ya rasilimali za uchumi wa bluu, uzingatiaji wa masuala mtambuka katika utekelezaji wa shughuli za uchumi wa bluu, na utafiti katika matumizi ya rasilimali za uchumi wa bluu

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kwa kifupi suala la muungano. Serikali imeendelea kuratibu vikao vya Kamati ya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Muungano. Katika mwaka 2024/2025 vikao viwili vya kujadili masuala ya Muungano vilifanyika. Kupitia vikao hivyo

ilifanyika tathmini ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya pamoja ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba tarehe 26 Aprili, 2025, kwa maana ya mwezi wa nne, nchi yetu itaadhimisha miaka 61 ya Muungano wetu. Maadhimisho haya ya Sherehe za Muungano za Mwaka 2025 yatafanyika katika mikoa yote yakiongozwa na viongozi wakuu wa Serikali. Viongozi hao pamoja na masuala mengine, watajumuika na wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo uzinduzi wa miradi ya maendeleo. Nitoe rai kwa wananchi wote kushiriki katika maadhimisho haya ili kuendelea kuenzi Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali itahakikisha kwamba hoja za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zitashughulikiwa kikamilifu. Vilevile, itaendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kudumisha na kulinda Muungano wetu. Maelezo zaidi juu ya programu za Muungano wetu ambazo zinatekelezwa na pande zote za Muungano yanapatikana katika aya ya 248 kwenye hotuba yetu na pia tumeweka kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na machache yaliyobaki ikiwemo Ushirikiano wa Kikanda na Kikamataifa juu ya uhusiano wa Kimataifa na Kikanda. Uhusiano kati ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na nchi nyingine, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa umeendelea kuimarika. Nchi yetu imeendelea kuwa na ushawishi mkubwa katika kutekeleza majukumu ya kidiplomasia kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeshiriki kikamilifu katika shughuli za Kimataifa ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi Tajiri Duniani wa Kundi la *G20* uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil; Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi *(COP 29);* Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika *New York* nchini Marekani; Mkutano wa 27 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola *(CHOGM 2024);* Mkutano wa 46 wa Kamati ya Urithi wa

Dunia ya *UNESCO* uliofanyika New Delhi, India na Mkutano Mkuu wa 68 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu *(IAEA),* uliofanyika Vienna, Australia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni Mwanadiplomasia Namba Moja Nchini kwa kutoa kipaumbele cha kuifungua nchi kwenye nyanja za diplomasia ya kiuchumi na kisiasa na hasa katika medani za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kuratibu ziara za kimkakati za viongozi wakuu wa Kitaifa nje ya nchi, na ziara za viongozi wakuu wa Mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya Kimataifa kuja hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu eneo hili la mikutano iliyoratibiwa na Serikali pamoja na mapitio ya sera ya mambo ya nje yanapatikana katika aya ya 253 hadi 257 kwenye hotuba yangu na kwenye ya vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie, habari, sanaa, utamaduni michezo; nianze na habari, sekta ya utangazaji ni muhimu sana katika dunia ya sasa na kidijiti ambapo upashanaji wa habari umekuwa ni msingi wa ukuzaji wa uchumi kwa kuwa chachu ya maendeleo ya mtu mmoja na mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo Serikali yetu imedhamiria kuhakikisha kuwa sekta ya habari nchini inaboreshwa ili kuwaongezea wananchi fursa ya kupata habari kwa kuongeza wigo wa upashanaji habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu usikivu wa matangazo ya redio na televisheni, mkakati wa kukuza lugha ya Kiswahili na kazi za sanaa yanapatikana katika aya ya 261 hadi 267 ya hotuba yangu na kwenye vishikwambi vyenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya maandalizi ya mashindano ya *CHAN* yanayotarajiwa kufanyika Agosti, 2025 na mashindano ya *AFCON* yanayotarajia kufanyika mwaka 2027. Hatua za maandalizi zinatekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya michezo, na tayari nimepata nafasi ya kufanya ukaguzi wa viwanja kule Zanzibar na hapa nchini. Hatua tuliyoifikia ni nzuri na inaridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi juu ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo tumeyaweka kwenye hotuba aya ya 269 hadi ya 270 na inapatikana pia kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuendeleza michezo hapa nchini pamoja na kuviwezesha vilabu vyetu kushiriki katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2024, Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.58 kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wa timu zetu katika mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada hizo zimewezesha kuimarika kwa ubora wa michezo hususan ligi ya ndani ya mpira wa miguu ambayo kwa sasa inau bora wa ngazi ya nne Barani Afrika ambapo ushindani mkubwa umeonekana kwa timu zinazowania ubingwa wa ligi hiyo ikiwemo *Dar Young African*, vinara na mabingwa wanaomalizia msimu, *Simba Sports Club*, *Azam Sports Club*, Singida *Big Stars* na *Tabora United*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tumeshuhudia timu ya Simba ikiendelea kuiwakilisha nchi yetu katika michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika hatua ya robo fainali na Timu ya Taifa ikiendelea kuwania nafasi ya kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia kwa Mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuitakia heri timu ya *Simba Sports Club* katika mchezo wake wa marudiano leo hii saa kumi jioni Uwanja wa Taifa wa Mkapa ili iweze kufanya vema na kufuzu hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo le Watanzania tutafurahi, *inshaallah*. Kadhalika, naitakia kila la heri timu yetu ya Taifa almaarufu *Taifa Stars* katika michezo yake

iliyobaki iweze kushinda na kuwa na nafasi ya kufuzu na kushiriki michuano hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa chachu ya mafanikio katika sekta ya michezo hapa nchini. Mheshimiwa Rais wakati wote amekuwa akitoa hamasa kubwa katika sekta ya michezo pamoja na kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia timu zetu ili ziweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio makubwa yamepatikana katika michezo, hasa mpira wa miguu kupitia mpango wa Goli la Mama, hamasa kwenye mchezo wa ndondi ambao nao pia umeanza kuchukua nafasi kubwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa viwanja vya michezo vya Arusha na Dodoma kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya *AFCON* 2027; kuratibu ukuzaji na uendelezaji wa Lugha ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa; na kuratibu Maadhimisho ya Kitaifa na Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani pamoja na Makongamano ya Kiswahili ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie na ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, sasa nitumie fursa hii kutoa msisitizo kwenye maeneo haya yafuatayo: -

(1) Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuhakikisha wananchi na viongozi wanapata muda wa kutoa mchango wao wa kutosha katika kujadili na kutoa maoni pamoja na kuzingatia maoni hayo katika rasimu ya Dira;

(2) Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania waendelee kuimarisha juhudi za ukusanyaji mapato ili kuongeza uwezo wa Taifa kujitegemea, pamoja na kubana matumizi katika maeneo

yasiyokuwa ya lazima katika utoaji wa huduma kwa wananchi;

(3) Nitoe rai kwa wananchi kujitokeza katika zoezi la uandikishaji kwenye Daftari la Mpigakura na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na

(4) Niwasihi Viongozi wa Dini, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Mashirika yasiyo ya Serikali na viongozi wote kuendelea kuhamasisha wananchi wote kuzingatia amani na utulivu wakati wa Uchaguzi Mkuu ujao. Pia, kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi huo ili kuwachagua viongozi walioomba nafasi za uongozi kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu pamoja na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sina shaka nyote mtakubaliana nami kuwa Mheshimiwa, Rais ni kiongozi shupavu, mwenye maono na mpenda haki. Niwaombe Watanzania wote waendelee kumwombea dua ili aweze kuwa na afya njema na aweze kutimiza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, namshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Pia, wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, wakiwemo Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika ushauri wenu umeiwezesha Serikali yetu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na katika kipindi cha uhai wa Bunge hili tumepata ushauri wa kutosha ambao umekuwa chachu katika maendeleo tunayoendelea kuyahudumia na katika kipindi cha Serikali hii ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye eneo muhimu la makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya

Waziri Mkuu na Ofisi hii ya Bunge kwa mwaka 2025/2026. Kwa mwaka 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 595,291,624,000, kati ya fedha hizo, shilingi 183,821,010,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 411,470,614,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 186,793,635,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi 174,960,303,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 11,793,332,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii unaweza kui-*scan* kutoka kwenye *QR code* ambayo inaonekana kwenye *screen* yetu ili uweze kupata hotuba yote na maeneo yote kwa marejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Mfuko wa Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2024/2025 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/2026. Pia, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizopo chini yake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2025/2026.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wenye afya njema tayari kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali ya Awamu ya Sita zilizotekelezwa kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka 2024/2025 na mwelekeo wake kwa mwaka 2025/2026.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwapongeza Waislamu wote kwa kumaliza salama mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikukuu ya Eid el Fitri kwa amani na utulivu. Aidha, niwatakie kila la heri Wakristo wote wanaoelekea kuhitimisha Mfungo wa Kwaresma pamoja na maandalizi mema ya Sikukuu ya Pasaka kwa mwaka 2025. **SALAMU ZA POLE**

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati tukiendelea na utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2024/2025 Bunge lako Tukufu lilipoteza viongozi mashuhuri pamoja na wanasiasa wakongwe ambao wamewahi kutumika katika nafasi mbalimbali zikiwemo za ubunge na nyingine katika Taifa letu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 27 Novemba, 2024, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani ukanda wa Afrika. Ninatoa salamu za pole kwako wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 17 Desemba, 2024 Taifa letu liliondokewa na Mheshimiwa John Tendwa Msajili Mstaafu wa Vyama vya Siasa. Marehemu John Tendwa atakumbukwa kwa kujenga misingi imara kwa vyama vya siasa. Pia, atakumbukwa kwa ukomavu wake hususan katika kusimamia demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, tarehe 27 Desemba, 2024 tuliondokewa na Mheshimiwa Mwanaisha Athumani Kwariko Jaji wa Mahakama ya Rufani na Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi. Marehemu Mwanaisha Kwariko, atakumbukwa kwa utumishi wake ndani ya Mahakama na mchango wake mkubwa katika Tume Huru ya Uchaguzi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 30 Desemba 2024 tuliondokewa na Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema aliyewahi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marehemu Jaji Fredrick Werema, pamoja na kazi nyingine atakumbukwa kwa ushauri na mchango wake wa kisheria katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 20 Februari 2025, nchi ilimpoteza Bibi Sifael Mushi, mwanamke aliyeshiriki katika tukio la kuchanganya udongo wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar. Bibi Sifael Mushi atakumbukwa kwa uzalendo na historia ya Muungano wetu.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, tarehe 5 Machi, 2025 tulimpoteza Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi aliyewahi kutumikia Taifa letu kwa nafasi ya Mbunge, Mkuu wa Mkoa na Waziri katika Wizara mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa marafiki na Watanzania wote walioguswa na msiba huo. Mheshimiwa Profesa Sarungi atakumbukwa kwa utumishi wake uliotukuka, uwajibikaji na uzalendo kwa nchi yake.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, usiku wa kuamkia tarehe 13 Machi, 2025, tulimpoteza mwanasiasa mkongwe Mheshimiwa Tabitha Siwale, aliyewahi kuhudumu katika nafasi ya Mbunge na Waziri katika wizara mbalimbali. Itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 3 Novemba, 1975, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Tabitha Siwale kuwa Mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Waziri.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mchango wake katika jamii, Hayati Mheshimiwa Tabitha Siwale, alitunukiwa Tuzo ya Mwanamke Mahiri wa Karne ya 21 mwaka 2000 na Tuzo ya Mwanamke wa Mwaka katika mwaka 2008. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na kwa Watanzania wote walioguswa na msiba huo.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 28 Machi, 2025 nchi yetu pia iliondokewa na mwanadiplomasia mkongwe Mheshimiwa Balozi Juma Volter Mwapachu. Balozi Mwapachu aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na kwa Watanzania wote walioguswa na msiba huo.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha hivi karibuni, wapo Watanzania wenzetu waliofikwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali ikiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Aidha, ninawaombea majeruhi wote uponyaji wa haraka ili waweze kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa letu.

**Vilevile, tunawaombea marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu ili aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina!**

**PONGEZI**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu kuwa, mwaka huu, Bunge la 12 linahitimisha shughuli zake kwa kipindi cha miaka mitano kilichoanza Novemba, 2020. Kwa msingi huo, hotuba yangu itaeleza kwa muhtasari mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii pia, imeainisha baadhi ya kazi zilizotekelezwa na Serikali kwa kuzingatia mipango na mikakati mbalimbali ya Taifa. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka

2021/2022 hadi 2025/2026 ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Ajenda ya Mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika; na Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati ya moyo wangu nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri tangu alipoanza kuiongoza nchi hii tarehe 19 Machi 2021. Ninampongeza pia kwa mafanikio makubwa aliyoyapata katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020. Kwa hakika ametekeleza kwa vitendo na matokeo yanaonekana.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu; kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii. Pia, kusimamia utawala bora; kuongoza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi; na kuhamasisha uwekezaji, diplomasia ya kiuchumi na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, nimpongeze Mheshimiwa *Dkt*. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuliongoza Taifa letu. Kwa hakika miongozo na maelekezo yake yamekuwa chachu katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa *Dkt*. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuhakikisha kuwa Ilani ya CCM kwa upande wa Zanzibar inatekelezwa kikamilifu na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi na usimamizi wa sekta mbalimbali za maendeleo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kipekee kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Dkt. Hussen Ali

Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika Oktoba, 2025.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** uchaguzi wao ni kielelezo cha ukomavu na imani kubwa waliyonayo wana CCM wote kwa viongozi hawa kutokana na uongozi wao makini na imara unaozingatia maslahi ya wananchi wote. Nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi ni mwanasiasa mkongwe mwenye uzoefu mkubwa ndani ya Chama cha Mapinduzi, Serikali, na jumuiya za kimataifa. Ninampongeza sana Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze Mheshimiwa Steven Masatu Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Bara. Nirudie kauli yangu niliyoitoa katika Mkutano wa 18 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 14 Februari 2025 kuwa Chama kimepata mtu sahihi kwa wakati sahihi kutokana na uzoefu wake na busara zake. Mheshimiwa Wasira ni kiongozi na mwanasiasa mkongwe, ambaye mchango wake unaendelea kuhitajika katika kuimarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu kupitia Chama cha Mapinduzi.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa *Dkt*. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Vilevile, ninampongeza sana kwa kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati, ambapo jitihada zake zimeleta mwelekeo na matokeo chanya ikiwa ni pamoja na kufanikiwa kuunganisha umeme katika vijiji vyote nchini. Vilevile, ninampongeza sana kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nikushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vema Bunge lako Tukufu katika kuisimamia Serikali ili kuhakikisha kuwa inatekeleza wajibu wake wa kuhudumia wananchi. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa na nzuri za kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa maoni na ushauri uliowezesha Serikali kukamilisha maandalizi ya Mipango na Bajeti kwa mwaka 2025/26.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa *Dkt*. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi; Kamati ya Kudumu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Maoni na ushauri wa Kamati hizo yamesaidia sana kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2025/2026.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Mashirika, Wakala na Idara Zinazojitegemea kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Waziri Mkuu.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Hamza Saidi Johari Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushauri wake wakati wote wa mikutano ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, ninamshukuru sana Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, kwa ushirikiano wake wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawashukuru watumishi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa. Jitihada zao, zimechangia tija na ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali. Vilevile, ninawashukuru kwa michango yao, iliyowezesha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2024/2025.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee kabisa, ninamshukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Patrobas Katambi, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu); Makatibu Wakuu *Dkt*. Jim Yonazi (Sera, Bunge na Uratibu) na Bi. Mary Maganga (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Naibu Makatibu Wakuu *Dkt*. James Kilabuko (Sera, Bunge na Uratibu) na Bi. Zuhura Yunus (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Waziri Mkuu.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuwashukuru washirika na wadau wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga uchumi na kuiletea nchi yetu maendeleo. Michango yao imekuwa muhimu katika kuwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa kuzingatia mipango tuliyojiwekea.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kushirikiana nami na kuniunga mkono katika kipindi chote nilipokuwa mbali nao wakati nikitekeleza majukumu ya kiserikali. Hali hii imeonesha ni kwa namna gani wamekuwa wastahimilivu na waungwana kwa Serikali yao katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya pamoja.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushirikiano wao kwa Serikali umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa, ninapenda kumshukuru mke wangu mpendwa Bi. Mary Majaliwa, watoto wangu na familia yangu kwa ujumla kwa upendo, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa. Ninawashukuru sana na ninawapenda.

**MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, katika hotuba yangu ya mwaka huu nitaanza kueleza kwa muhtasari mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Mheshimiwa Rais mara baada ya kushika hatamu ya kuliongoza Taifa letu, aliweka bayana vipaumbele na mwelekeo thabiti unaolenga kuwatumikia wananchi wakati alipolihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais aliahidi kudumisha mazuri yote ya awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuibua mengine mapya. Alisisitiza utekelezaji wa ahadi hizo kupitia salamu ya '***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Kazi Iendelee'.*** Na kwa hakika kazi imefanyika, yaliyoachwa yametekelezwa, mapya yameibuliwa kwa mafanikio na tunasonga mbele.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mheshimiwa Rais alielekeza Serikali anayoingoza kutekeleza majukumu kwa kuzingatia ***falsafa ya 4Rs*** ambayo inasisitiza umuhimu wa ***Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga Upya.*** Falsafa hiyo inalenga kulileta taifa pamoja, kujenga hali ya kuvumiliana, kuwa na makubaliano ya pamoja na kulijenga upya Taifa letu.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia mwelekeo na maono ya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha uongozi wake, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Shughuli hizo ni pamoja na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya uchumi, kuongeza fursa za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kupitia sekta za uzalishaji, kuboresha huduma za kijamii ikiwemo afya, elimu na maji, kutekeleza mikakati thabiti ya kuvutia uwekezaji nchini na kukuza uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya kiuchumi.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana yamewezesha kukua kwa uchumi wa nchi yetu pamoja na kuboresha maisha ya wananchi. Ninaomba sasa nilitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi wote baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uongozi wa Awamu ya Sita:

**a. Uzalishaji wa Ajira**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuzalisha fursa za ajira nchini kupitia uwekezaji na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki, reli ya kisasa, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato. Vilevile, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kupanua wigo wa uzalishaji wa ajira nchini. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Februari, 2025 jumla ya ajira 8,084,204 zimezalishwa katika sekta ya umma na sekta binafsi.

**b. Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyo azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kukamilisha kwa ufanisi mkubwa miradi yote ya kimkakati ili kuleta maendeleo endelevu ya nchi yetu, tarehe 01 Agosti, 2024, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua huduma za usafiri wa reli kati ya Dar es Salaam - Morogoro – Dodoma. Hadi kufikia Februari, 2025, abiria 1,809,983 wamesafirishwa na jumla ya shilingi bilioni 54.9 zimekusanywa. Uwepo wa huduma hiyo ya treni, umepunguza muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kutoka wastani wa saa 10 kwa basi hadi kati ya saa tatu na nne na kuchagiza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, ujenzi wa kipande cha kutoka Mwanza - Isaka (km 341) umefikia asilimia 62.37; Makutupora – Tabora (km 368) umefikia asilimia 14.53; Tabora – Isaka (km 165) umefikia asilimia 6.33; na Tabora – Kigoma (km 506) umefikia asilimia 7.34. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa kipande cha Uvinza - Malagarasi - Musongati (Km 282) yameanza ambapo Serikali za Tanzania na Burundi zilisaini mkataba wa ujenzi wa kipande hicho tarehe 29 Januari, 2025.

**c. Uimarishaji wa Huduma za Bandari ya Dar es Salaam**

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia ushindani wa kibiashara uliopo katika ukanda wa Bahari ya Hindi, nchi yetu imechukua hatua mahsusi ili kunufaika na fursa ya kijiografia tuliyonayo ya kuwa lango kuu la kibiashara kwa nchi jirani. Hatua hizo ni pamoja na uboreshaji wa bandari zetu zilizo katika Bahari na uwekezaji wa sekta binafsi katika kutoa baadhi ya huduma bandarini.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya makasha yanayohudumiwa yameongezeka na kufikia 686,515 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 ikilinganishwa na makasha 670,724 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Ongezeko hilo lilichangiwa na uwekezaji uliofanyika katika gati 0 - 7 ambapo idadi ya makasha yaliyohudumiwa katika eneo hilo yaliongezeka kutoka 122,339 hadi 160,286 katika kipindi hicho. Aidha, muda wa meli za makasha kusubiri nangani umeondolewa kabisa. Hivi sasa, meli huenda moja kwa moja gatini mara zinapowasili katika Bandari ya Dar es Salaam. Hali hiyo imepunguza wastani wa muda wa meli kusubiri nangani kutoka siku 46 za awali hadi siku saba.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kupungua kwa idadi ya meli zinazosubiria nangani kutoka meli 30 hadi tatu muda wa kuhudumia meli za mafuta umepungua kutoka siku 10 hadi siku tatu. Kuimarika kwa utoaji wa huduma hizo kumepunguza tozo ya meli kusubiri nangani na hivyo kuchangia kupunguza gharama za bidhaa kwa Watanzania.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mapato ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa mwezi yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 mwaka 2023/2024 hadi kufikia wastani wa

shilingi trilioni moja mwaka 2024/2025. Aidha, mapato yanayokusanywa kutokana na ushuru wa forodha yameongezeka kutoka shilingi trilioni 9.35 mwaka 2023/2024 hadi shilingi trillioni 9.86 kufikia Februari 2025.

**d. Kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania- ATCL**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania ili kutoa huduma bora za usafiri wa anga kwa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi. Serikali katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Februari, 2025, ilitumia shilingi trilioni 1.49 kununua ndege saba ambapo ndege sita ni za abiria na ndege moja ni ya mizigo. Ununuzi wa ndege hizo umelifanya Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 ambazo zimeimarisha na kuongeza safari za ndege za ndani na nje ya nchi.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** hivi sasa Shirika la Ndege Tanzania limeongeza safari za ndege kwenda nchi za nje ambapo ndege zake zinasafiri kwenda Johanesburg (Afrika Kusini), Guangzhou (China), Mumbai (India), Lubumbashi (DRC), Lusaka na Ndola (Zambia), Harare (Zimbabwe), Dubai (Falme za Kiarabu), Nairobi (Kenya), Entebbe (Uganda), Bujumbura (Burundi), Moroni (Comoro). Hivi karibuni, litaanza safari za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la ndege limechangia pia kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaohudumiwa kutoka abiria 822,232 mwaka 2021 hadi abiria 3,818,567 Februari, 2025; mizigo kutoka tani 2,567 mwaka 2021 hadi tani 5,730.48 Februari, 2025. Kadhalika, mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 254 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.5 Februari, 2025.

**e. Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa ikiwemo Tanzanite (Dar es Salaam) lenye urefu wa kilometa 1.03 na Wami (Pwani) lenye urefu wa mita 510. Aidha, inaendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo — Busisi (Mwanza) lenye urefu wa km 3.2 ambao umefikia asilimia 98. Lengo la ujenzi wa madaraja hayo ni kurahisisha shughuli za kiuchumi na ufikiwaji wa huduma za kijamii kwa haraka kwa kupunguza foleni na muda wa usafiri.

**f. Ujenzi na Ukarabati wa Meli Katika Maziwa Makuu**

**52.** ***Mheshimiwa* Spika,** utoaji wa huduma za usafiri katika maziwa makuu umeendelea kuimarishwa ili kuhakikisha wananchi wetu wanapiga hatua za kiuchumi. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa meli ya MV Mwanza ambao umefikia asilimia 98. Aidha, meli hiyo itakayogharimu shilingi bilioni 109, itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo, na magari 23.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea na ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika ambazo ni: MT Sangara kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 3.60 ambao umefikia asilimia 98, mradi huu utakapokamilika utawezesha kubeba shehena ya mafuta kiasi cha lita 410,000; na MV Liemba kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 13.19 ambao umefikia asilimia 15, mradi huu utakapokamilika utawezesha kubeba abiria 600 na tani 200 za mizigo.

**g. Ukamilishaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115)**

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme katika Bwawa la Julius Nyerere kwa gharama ya shilingi trilioni 6.6. Ujenzi wa mradi huo wenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 kwa siku umekamilika. Hadi Machi 2025, jumla ya megawati 2,115 zimeunganishwa kwenye gridi ya taifa na hivyo kuongeza kiwango cha umeme katika gridi ya taifa kufikia megawati 4,031.7. Kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika mradi huo kumeongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuwa chachu ya kasi ya maendeleo ya nchi.

**h. Uunganishaji wa Umeme Vijijini**

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Februari, 2025, Serikali imeunganisha umeme katika vijiji 4,071 kwa gharama ya shilingi bilioni 1,593 na hivyo kuwezesha vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kuunganishwa na umeme. Hatua inayofuata baada ya kukamilisha mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vyote, ni kupeleka umeme kwenye vitongoji ambapo jumla ya vitongoji 33,657 kati ya 64,359, sawa na asilimia 52.3 vimeunganishwa na huduma ya umeme. Usambazaji wa umeme katika vijiji na vitongoji utawezesha wananchi kushiriki kikamilifu

katika shughuli za kiuchumi hususan zinazohitaji nishati ya umeme zikiwemo kuchomelea vyuma, useremala, kuchakata nafaka na kuchenjua madini.

**i. Ujenzi wa Bomba la Mafuta Kutoka Hoima (Uganda) Hadi Tanga (Tanzania)**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda inatekeleza ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lenye urefu wa kilometa 1,443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 55 ambapo kilometa 1,115 za bomba hilo zinapita hapa nchini. Serikali tayari imeshachangia mtaji wa Dola za Marekani milioni 376 sawa na asilimia 15 ya hisa. Kupitia mradi huo, jumla ya ajira 6,610 za muda na ajira 114 za kudumu zimezalishwa.

**j. Ujenzi wa Shule za Sayansi za Wasichana katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama mnavyokumbuka, wakati anaingia madarakani Mheshimiwa Rais alieleza azma yake ya kumsaidia mwanamke. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita imejenga shule za wasichana katika mikoa 26 zenye michepuo ya masomo ya sayansi. Hadi sasa, ujenzi wa shule hizo umegharimu shilingi bilioni 121.55 na tayari wanafunzi 10,274 wameshadahiliwa.

**k. Uwezeshaji wa Wanafunzi wa Vyuo vya Kati na Elimu ya Juu**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Serikali ya Awamu ya Sita imeanzisha programu ya ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu (*Samia Scholarship Program)* kwenye fani za sayansi, teknolojia, ubunifu, uhandisi, hisabati na tiba wenye ufaulu wa kiwango cha juu. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 6.63 kimetolewa tangu kuanza kwa programu hiyo na kunufaisha wanafunzi 1,313.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile Serikali inatoa ufadhili wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya vyuo vya kati wanaosoma stashahada za fani za ufundi. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo shilingi bilioni 20.08 zimetolewa na kunufaisha wanafunzi 7,732. Pia, imeanzisha Mfuko wa Wabunifu unaojulikana kama *Samia*

*Innovation Fund* ili kusaidia wabunifu kuchochea biashara za ubunifu na kuongeza fursa za ajira.

**l. Ujenzi wa Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma za afya nchini umeendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 8,458 mwaka 2020 hadi 9,826 Februari, 2025.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, idadi ya hospitali zinazotoa huduma ya magonjwa ya dharura zimeongezeka kutoka saba mwaka 2020 hadi 116 mwaka 2025. Pia, vituo vya kutolea huduma za afya vyenye majengo ya mama na mtoto vimeongezeka kutoka 6,081 mwaka 2020 hadi 7,397 Februari, 2025. Kutokana na jitihada hizo vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000 Februari, 2025; na vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 67 mwaka 2020 hadi 43 Februari, 2025.

**m. Huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi na Hali ya Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zimeendelea kuimarika. Hivi sasa huduma hizo zinapatikana katika hospitali za rufaa za mikoa zinatoa huduma nane za kibingwa ambazo hapo awali zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya kanda. Huduma hizo ni pamoja na afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, afya ya watoto, magonjwa ya ndani, upasuaji, upasuaji mifupa, huduma za dharura, huduma za mionzi, huduma za ganzi na dawa za usingizi.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya kisasa na bidhaa za afya imeimarika kutoka asilimia 73 mwaka 2020 hadi asilimia 89.3 Februari, 2025. Mafanikio hayo makubwa yameendelea kuwavutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na kuimarisha Tiba Utalii ambapo hadi Februari, 2025 wagonjwa 7,843 kutoka nje ya nchi wametibiwa ikilinganishwa na wagonjwa 5,705 mwaka 2020.

**n. Kuongeza Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini**

**64. *Mheshimiwa Spika,*** hali ya upatikanaji wa maji imeendelea kuimarika kutokana na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma ya maji vijijini na mijini. Jumla ya miradi 1,633 imetekelezwa, kati ya hiyo, miradi 1,335 ni ya vijijini na miradi 298 ya mijini. Miradi hiyo imeongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asimilia 79.6 mwaka 2025. Kwa upande wa mijini, kiwango hicho kimeongezeka kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2020 hadi asilimia 90 mwaka 2025. Kutokana na ongezeko hilo wananchi 12,547,526 wamenufaika na huduma ya maji safi na salama.

**o. Kuongezeka kwa Idadi ya Watalii**

**65. *Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mchango mkubwa wa sekta ya utalii katika kuingiza fedha za kigeni nchini, kukuza uchumi na maendeleo. Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi ili kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Kutokana na umuhimu huo, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua kufanya jitihada binafsi za kutangaza vivutio vya utalii nchini kupitia filamu ya Tanzania "*The Royal Tour*" na "*Amazing Tanzania*". Jitihada hizo zimechangia kuongeza idadi ya watalii kutoka 1,711,625 mwaka 2021 hadi 5,360,247 mwaka 2024. Kati yao, watalii wa kimataifa waliongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 2,141,895 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 132.24 na idadi ya watalii wa ndani iliongezeka kwa asilimia 307.94 kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 3,218,352 mwaka 2024.

**p. Ujenzi wa Mji wa Serikali – Mtumba**

**66. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa uendelezaji wa Mji wa Serikali ambao hadi Machi, 2025 unajumuisha jumla ya majengo 34. Kati ya hayo, majengo 24 ni ya wizara na 10 ni ya taasisi. Pamoja na majengo hayo, Serikali imejenga Jengo la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika eneo la Kikombo. Aidha, wastani wa ujenzi wa majengo ya wizara umefikia asilimia 89.7 na kutumia jumla ya shilingi bilioni 534.4. Vilevile, ujenzi wa majengo matatu umekamilika na kuanza kutumika. Kukamilika kwa majengo hayo kutawezesha wananchi

kupata huduma kwa urahisi na kupendezesha Jiji na hivyo kuwa moja ya vivutio vya utalii Mkoani Dodoma.

***q.* Kuimarisha Diplomasia *ya Kiuchumi***

***67.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Machi 2025, Serikali imeimarisha ushiriki wake katika nyanja ya kidiplomasia kwa kujumuisha ushirikiano wa kikanda, kimataifa na diplomasia inayozingatia maslahi ya kiuchumi. Katika kipindi hicho, nchi yetu imeshiriki katika mikutano 312 ya Kikanda na Kimataifa na mikutano 42 ya Tume za Kudumu za Pamoja (JPC) ambayo imewezesha kusainiwa kwa hati za Makubaliano 229.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuimarika kwa uhusiano wa kimataifa, Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika tarehe 15 Februari 2025 Jijini Addis Ababa, Ethiopia uliichagua Tanzania kuwa Mjumbe wa Kamati ya Uongozi wa Umoja wa Afrika kwa mwaka 2025. Kuchaguliwa kwa Tanzania katika nafasi hiyo kutawezesha nchi kunufaika na nafasi za ajira zinazotolewa kwa kuzingatia uwiano wa wakilishi kwa nchi wanachama pamoja na kujenga mtangamano imara na wenye maslahi kwa pande zote.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Agosti, 2024 Serikali iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 44 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika Harare, Zimbabwe. Katika mkutano huo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya SADC ya Siasa, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Mwaka mmoja kuanzia Agosti, 2024.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikutano na ziara hizo pamoja na jitihada kubwa za kidiplomasia zinazofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimeleta mafanikio makubwa kwa nchi yetu. Mafanikio hayo ni pamoja na upatikanaji wa fursa za masoko nje ya nchi; wawekezaji kutoka nje; misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo; ongezeko la fursa za ajira na ufadhili wa masomo nje ya nchi.

**UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kuainisha baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Jemedari wetu, Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ninaomba nieleze utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2024/2025.

**UKUAJI WA UCHUMI**

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, mwenendo wa viashiria vya uchumi na bajeti katika mwaka 2024/2025 umeendelea kuwa wa kuridhisha. Katika mwaka 2024, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme; uimarishaji wa huduma za jamii; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji; na kuimarika kwa sekta ya uchukuzi. Aidha, sekta zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji katika kipindi cha marejeo ni pamoja na shughuli za sanaa na burudani asilimia 17.1, fedha na bima asilimia 16.3 na habari na mawasiliano asilimia 14.3.

**MFUMUKO WA BEI**

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumuko wa bei kwa mwaka 2024 umepungua hadi kufikia wastani wa asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi na Jumuiya za kikanda la wigo wa asilimia 3.0 hadi 5.0 katika muda wa kati. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti; uwepo wa utoshelevu wa chakula nchini; na uboreshaji wa miundombinu ya uchukuzi iliyorahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka maeneo ya uzalishaji hadi kwenye masoko.

**AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI**

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2024, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani bilioni 5.50 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 5.45 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.5, ikiwa ni juu ya lengo la

nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi cha miezi minne. Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa programu ya Benki Kuu ya Tanzania ya ununuzi wa dhahabu nchini; kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yaliyotokana na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia; mauzo ya mazao ya biashara ikiwemo korosho na tumbaku; na kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini.

**MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MAPATO**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa ukusanyaji wa mapato nchini umeendelea kukua ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025, mapato ya ndani yalifikia shilingi trilioni 22.58 sawa na asilimia 99.9 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 22.60 ambao ni ukuaji wa asilimia 16.6 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Ufanisi huo umetokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA inayosimamia shughuli za ukusanyaji wa mapato katika taasisi; kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarika kwa shughuli za ufuatiliaji na usimamizi; na uwepo wa ushirikiano mzuri kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mapato yote ya ndani yaliyokusanywa, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya shilingi trilioni 19.62 sawa na asilimia 101.4 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 17.18; Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali zilikusanya shilingi trilioni 2.05 sawa na asilimia 87.1 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.36; na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya shilingi bilioni 903.89 ikiwa ni asilimia 101.3 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 892.38.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuimarisha utekelezaji wa mpango na bajeti. Aidha, Serikali itaendelea kutumia namba ya ankara *(control number)* ya malipo jumuishi katika kufanya malipo ya kodi, tozo au ada; kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA ikiwemo mifumo ya ardhi, TAUSI na forodha; kuendelea kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari na matumizi ya mashine za kielektroniki; na kuendelea kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vilivyopo na kubuni vyanzo vipya.

**UWEKEZAJI NA UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Hatua hizo ni pamoja na kufanya maboresho ya Sheria 12 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2024 na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeanza maandalizi ya Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini unaolenga kuvutia uwekezaji wa nje na ndani, kuongeza fursa za ajira, uboreshaji wa miundombinu, upatikanaji wa soko la kimataifa kwa bidhaa za ndani na kukuza ushindaji na ubora wa bidhaa.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la uwezeshaji kiuchumi na maendeleo ya sekta binafsi, Serikali imezindua Mwongozo wa Uratibu wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa mifuko na programu za uwezeshaji na kuainisha taratibu mahususi zitakazofuatwa kabla na baada ya kuanzisha mfuko na programu za uwezeshaji. Vilevile, Serikali imeanza utekelezaji wa Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia inayolenga kuwezesha wanawake, vijana na makundi maalum kunufaika na fursa za uwezeshaji. Aidha, Serikali iliratibu Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara ili pamoja na masuala mengine kutoa fursa ya majadiliano kuhusu maboresho ya mfumo wa usimamizi wa kodi.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha na kuboresha uwekezaji ni pamoja na kupungua kwa muda wa kupata vibali vya uwekezaji kutoka wastani wa siku 14 hadi siku 3; kupungua kwa muda wa usajili wa hospitali binafsi kutoka miezi 12 hadi miezi 3; kupungua kwa muda wa kupata cheti cha usajili wa sehemu za kazi kutoka siku 14 hadi siku 1; kupungua kwa muda wa kutoa leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi kutoka siku 28 hadi siku 3; na kupungua kwa muda wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka siku zaidi 14 hadi wastani wa siku 3 hadi siku 7.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji nchini umeongeza usajili wa miradi kwenye sekta binafsi kutoka 416 hadi 615. Miradi hiyo yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 4.49 ilizalisha ajira mpya 119,717 katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 ikilinganishwa miradi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 7.95 iliyozalisha ajira mpya 187,355 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025.

**83.** ***Mheshimiwa*** **Spika,** Serikali imeendelea kuboresha na kuwezesha taasisi za umma kuongeza mitaji iliyochangia kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji kwa asilimia 12.6 kutoka shilingi trilioni 75.8 mwaka 2022/2023 mpaka shillingi trilioni 85.4 mwaka 2023/2024. Aidha, uwekezaji wa Serikali katika taasisi za nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 9 kutoka shilingi bilioni 778.95 mwaka 2022/2023 na kufikia shilingi bilioni 846.22 mwaka 2023/2024.

**UTAWALA WA SHERIA**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusimamia utawala wa sheria unaozingatia misingi ya utawala bora na haki za binadamu, Serikali imefanya marekebisho ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuinua ustawi wa wa wananchi. Katika mwaka 2024/2025, Sheria 19, Kanuni 65, Amri 116, Notisi 313, Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa 76, Matamko mawili na Hati Idhini moja zilitungwa na kufanyiwa marekebisho. Vilevile, imekamilisha maandalizi ya Sheria Ndogo Kifani 40 ili kuziongoza Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uandaaji wa Sheria Ndogo.

**85.** ***Mheshimiwa*** **Spika,** vilevile, katika kuharakisha upatikanaji wa haki, Serikali imeendelea kutenganisha shughuli za mashtaka na upelelezi ili kuendelea kuimarisha huduma za haki jinai na kusogeza huduma za kisheria na kimahakama karibu na wananchi. Katika mwaka 2024/2025, jumla ya wilaya 16 za mashtaka zimefunguliwa na kufanya uwepo wa jumla ya ofisi 78 za mashtaka za wilaya hapa nchini.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizo zimeenda sambamba na utekelezaji Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia. Kampeni hiyo, inatekelezwa kwa lengo la kuongeza wigo wa

upatikanaji haki kwa wananchi, hususan wale wasio na uwezo wa kumudu gharama za huduma za kisheria ambapo wananchi 1,373,099 wamefikiwa na huduma hiyo. Itakumbukwa kuwa Tarehe 18 Februari, 2025 nikiwa Wilayani Ruangwa, nilizindua kampeni hiyo kimkoa na hivyo kuongeza idadi ya mikoa iliyofikiwa na kampeni hiyo kufikia mikoa 19.

**87.** ***Mheshimiwa Spika:*** kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini iliyoundwa na Mheshimiwa Rais. Mafanikio ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume hiyo, yameanza kuonekana. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na: kupungua kwa msongamano wa mahabusu na wafungwa gerezani; kurekebishwa kwa sheria zinazohusu utoaji wa haki jinai; kuiwezesha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kutekeleza mpango wa kutenganisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka; kuzijengea uwezo taasisi za utoaji wa haki jinai ikiwa ni pamoja na kuongeza rasilimali watu na vitendea kazi.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha Sekta ya Sheria kwa kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini; kujenga na kukarabati miundombinu ya Mahakama; kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa watu wenye uhitaji; na kuboresha mifumo ya haki za binadamu na utawala bora.

## SEKTA ZA UZALISHAJI KILIMO

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, sekta ya kilimo ni muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini kutokana na mchango wake katika uzalishaji wa ajira na mazao ya chakula, biashara na malighafi za viwandani. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuendeleza sekta hii muhimu kwa uchumi wa taifa letu. Moja ya hatua hizo ni utekelezaji wa Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo (ASDP). Tayari Serikali imekamilisha mapitio na uhuishaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II) kwa muhula wa mwisho utakaokamilika mwaka 2030.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mapitio hayo baadhi ya masuala yaliyobainika ni pamoja na kufikiwa kwa malengo ya awali kwa asilimia 66 na kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa programu hiyo na mikakati inayolenga kuitekeleza ili kuimarisha sekta ya kilimo. Hii ni pamoja na kuimarisha uratibu wa programu, kuweka mkazo kwenye masuala ya uhifadhi na usimamizi rasilimali za misitu, kuongeza nguvu katika utekelezaji wa afua za kuongeza usalama wa chakula na lishe na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta hiyo.

**Usalama wa Chakula**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati madhubuti ya kuendeleza kilimo. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa mbegu na pembejeo za kilimo, kutoa mikopo ya kilimo kwa wananchi, kuanzisha skimu za umwagiliaji na kuimarisha ushirika.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 128. Utoshelevu huo unatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 20.4 katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 hadi tani milioni 22.8 msimu wa mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limetokana na ongezeko la matumizi ya mbolea iliyotolewa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku, kuongezeka kwa mtandao wa kilimo cha umwagiliaji, kuimarika kwa huduma za ugani na matumizi ya mbegu bora.

**Upatikanaji wa Mbolea**

**93.** ***Mheshimiwa Spika*,** hali ya upatikanaji wa mbolea nchini imeendelea kuimarika ambapo hadi tarehe 31 Januari, 2025 kulikuwa na jumla ya tani milioni 1.21 sawa na asilimia 80.9 ya makisio ya mahitaji ya tani milioni 1.5 za mbolea kwa msimu wa mwaka 2024/2025. Aidha, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2024/2025, tani 388,619.87 za mbolea yenye ruzuku ya thamani shilingi bilioni 131.66 imesambazwa kwa wakulima 4,223,278.

**Upatikanaji wa Huduma za Ugani**
**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa huduma za ugani katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao nchini, Serikali imenunua na kusambaza pikipiki 555 kwa maafisa ugani, vishikwambi 3,500, magari 40, visanduku vya ugani 1,000 na kuanza ujenzi wa nyumba 50 za maafisa ugani. Niwatake maafisa ugani wote kuvitunza vitendea kazi walivyopatiwa na kuendelea kuvitumia kwa lengo lililokusudiwa ili kupata tija na manufaa yanayotarajiwa.

**Kilimo cha Umwagiliaji**
**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ambapo eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta 694,715 mwaka 2023/2024 hadi hekta 727,280.6 mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo limechangiwa na kukamilika kwa ujenzi wa skimu tatu za umwagiliaji za Tlawi (Manyara) kwa awamu ya kwanza, Magurukenda na Sukuma (Buchosa) na mabwawa matatu ya Tlawi (Manyara), Ulyanyama na Goweko (Tabora) pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa skimu sita za umwagiliaji. Aidha, ujenzi wa skimu 50, mabwawa 16 na ukarabati wa skimu 42 unaendelea.

**Utoaji wa Mikopo ya Kilimo**
**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza tija katika sekta ya uzalishaji, Serikali imeendelea kuboresha utoaji wa huduma wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa lengo la kuimarisha na kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima. Katika mwaka 2024, mikopo iliyodhaminiwa na Benki hiyo ilifikia shilingi bilioni 131 zilizotolewa kwa wakulima 5,865 kwa ajili ya utekelezaji miradi iliyo katika mnyororo wa thamani wa kilimo ikiwemo ununuzi wa mazao na uchakataji, usambazaji wa pembejeo za kilimo na ununuzi wa zana za kilimo kama matrekta na mitambo ya kuvuna mazao.

**Maendeleo ya Ushirika**
**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ushirika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirika nchini kwa kujenga Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU). Mfumo huo umesajili vyama vya ushirika 6,570 na kuhakiki taarifa za wanachama na wasio wanachama 2,216,282 wanao hudumiwa

na vyama vya ushirika. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia mauzo ya mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika ambapo hadi Februari, 2025, jumla ya tani milioni 2.22 za mazao zenye thamani ya shilingi trilioni 4.23 zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa ushirika ikilinganishwa na tani milioni 1.64 zilizouzwa kwa thamani ya shilingi trilioni 1.98 mwaka 2023/2024.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake kupata mitaji na pembejeo; kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, sukari na chai; kujenga na kukarabati ghala za kuhifadhi mbolea na kuendelea na mpango wa utoaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima nchini.

**Mifugo**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya mifugo imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Serikali kwa kutambua umuhimu huo imeendelea kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za mifugo, kuimarisha huduma za ugani na kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayovuka mipaka. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Januari 2025, Serikali imenunua chanjo zenye thamani ya shilingi bilioni 10.1 kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo. Pia, imetoa chanjo kwa mifugo zaidi ya milioni 370 dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ikiwemo kimeta na homa ya mapafu. Uchanjaji wa mifugo unaifanya Tanzania kukidhi matakwa ya viwango vya kimataifa katika biashara ya mifugo na mazao.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatambua umuhimu wa ufugaji wa kisasa unaozingatia malisho bora na idadi ya mifugo inayoweza kuleta tija kwa mfugaji. Hivyo, imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ambapo ujenzi wa mabwawa manne ya Bukabwa (Butiama), Kihumbu (Bunda), Isulamilomo (Nsimbo) na Kwenkikwembe (Kilindi). Mabwawa hayo yana uwezo wa kuhifadhi wastani wa lita za maji milioni 120 kila moja.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na Kampeni ya Tutunzane Mvomero iliyozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 3 Agosti, 2024, uzalishaji wa mbegu za malisho umeongezeka kutoka tani 127.8 mwaka 2023/ 2024 hadi tani 152.67 mwaka 2024/2025; na uzalishaji wa malisho yaliyosindikwa umeongezeka kutoka tani 728.6 hadi tani 2,669.84.

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na jitahada zilizofanyika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025, uzalishaji wa mifugo umeongezeka hadi milioni 189.8 kutoka mifugo milioni 181.8 mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limechangia kuongeza uzalishaji wa nyama kutoka tani 963,856.55 mwaka 2023/2024 hadi tani 1,054,114.03 Februari, 2025; na thamani ya nyama iliyozalishwa imeongezeka kutoka shilingi trilioni 7.71 mwaka 2023/2024 hadi shilingi trilioni 8.43 Februari, 2025.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu na huduma za chanjo ya mifugo; kujenga na kukarabati minada ya mifugo; kujenga machinjio za kisasa; na kujenga mashamba darasa ya malisho.

**Uvuvi**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuweka mkazo katika ukuaji wa sekta ya uvuvi kwa kuboresha miundombinu, kuweka mazingira wezeshi katika uzalishaji wa samaki na biashara ya mazao ya uvuvi na kuimarisha kilimo cha mwani. Kutokana na jitihada hizo, kati ya Julai, 2024 hadi Februari, 2025, jumla ya tani 352,004.55 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.36 zilivunwa ikilinganishwa na tani za samaki 323,856.83, zenye thamani ya shilingi trilioni 1.92, zilizovunwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa mikopo nafuu kwa wananchi ili kuwekeza katika ufugaji samaki kwa njia ya vizimba ambapo mikopo ya shilingi bilioni 36.64 imetolewa kwa wanufaika 7,130. Kupitia mikopo hiyo, ajira 3,000 za moja kwa moja, na zaidi ya 1,000 katika mnyororo wa thamani zimezalishwa.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa-Masoko. Ujenzi wa bandari hiyo utakaohusisha gati lenye urefu wa mita za mraba 315, jengo la utawala na vyumba baridi vya kuhifadhia samaki kwa gharama ya shilingi bilioni 289.5 umefikia asilimia 79. Ujenzi huo utakapokamilika, unakadiriwa kuhudumia tani 60,000 za mazao ya uvuvi kwa mwaka na kutoa fursa za ajira takriban 30,000.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko-Lindi; kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Bagamoyo; na kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na ugani.

**Maliasili na Utalii**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kukuza utalii na kuendeleza maliasili zilizopo nchini ili kuiwezesha nchi kupata mapato na kukuza ustawi wa wananchi. Katika mwaka 2024/2025, tumeshuhudia ukuaji wa utalii wa mikutano na matukio ambapo mikutano mbalimbali ya kimataifa ilifanyika nchini ikiwemo Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika Januari, 2025. Kadhalika, Jukwaa la Pili la Utalii wa Chakula Duniani kwa Kanda ya Afrika linaloandaliwa na Shirika la Utalii Duniani linatarajiwa kufanyika hapa nchini katika mwezi huu wa Aprili 2025.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) yaliyopangwa kufanyika Agosti, 2025 ni fursa nyingine adhimu ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii ikizingatiwa kuwa michezo huhusisha mashabiki wengi kutoka nchi mbalimbali. Niwatake Watanzania wote kutumia vema fursa hii adhimu kwa Taifa letu

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, utangazaji wa utalii na vivutio vilivyoko nchini umewezesha Taasisi ya *World Travel Awards* kuitambua na kutoa Tuzo kwa Tanzania kama eneo linalovutia zaidi kiutalii mwaka 2024. Vilevile, eneo linaloongoza kwa utalii wa safari Dunia kwa mwaka 2024; Hifadhi ya Taifa Serengeti kuendelea kuwa bora duniani kwa miaka sita (6) mfululizo; na Mlima

Kilimanjaro kuwa kivutio bora cha utalii barani Afrika kwa mwaka 2024.

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kutangaza utalii wa ndani na nje ya nchi; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati na kuimarisha usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na uhifadhi.

**Madini**

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya madini imeendelea kukua na kuimarika kutokana na mikakati mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ambayo imechagiza kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na Pato la Taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na ugunduzi wa maeneo mapya ya uchimbaji, kuendeleza madini muhimu na ya mkakati; kuhamasisha uwekezaji, uanzishaji minada na maonesho ya madini ya vito; uongezaji thamani madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo; na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli.

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari 2025, Serikali imetoa leseni 39 za utafiti wa madini mkakati, leseni 170 za uchimbaji mdogo wa madini mkakati yakiwemo madini ya Kinywe (graphite), *Nickel, Cobalt, Lithium, Heavy Mineral Sand* na *Rear Earth Elements*, leseni 01 ya uchimbaji wa kati na leseni 02 za uchenjuaji madini mkakati. Vilevile, imetoa leseni 7,076 kwa ajili ya shughuli za madini ambazo ni uchimbaji wa kati na mdogo, utafutaji, ufanyaji biashara ndogo na kubwa na uchenjuaji.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuimarika kwa ukusanyaji wa maduhuli, Serikali ilikusanya shilingi bilioni 80.52. Fedha hizo ni mrabaha na ada ya ukaguzi kutoka katika masoko ya madini 44 na vituo 106 vya ununuzi wa madini.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuhamasisha uwekezaji; kuongeza thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini; na kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

**NISHATI Umeme**

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa uhakika na unaokidhi mahitaji ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Hadi Machi 2025, kiwango cha umeme uliounganishwa katika Gridi ya Taifa ni Megawati 4,031.7 ikilinganishwa na Megawati 1,889.84 za Februari, 2024. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (megawati 2,115) na Rusumo – Nyakanazi (megawati 26.6).

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme na kuwafikia wananchi, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Hadi Februari, 2025, njia ya kusafirishia umeme imeongezeka na kufikia urefu wa kilometa 8,025.38 kutoka kilometa 7,745.38 zilizokuwepo mwaka 2024. Vilevile, njia za kusambaza umeme zimeongezeka na kufikia urefu wa kilometa 198,215.17 ikilinganishwa na kilometa 176,334.14 zilizokuwepo.

**Mafuta na Gesi**

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali iliendelea na utekelezaji wa shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi asilia ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2025 wastani wa kiasi cha gesi asilia kilichozalishwa nchini kilikuwa futi za ujazo milioni 177.18 kwa siku. Kiasi cha gesi hiyo kilitoka katika vitalu vya Songosongo (futi za ujazo 87.78) na Mnazi bay (futi za ujazo 89.4). Aidha, kasi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma ya gesi asilia unaoendelea nchini unatarajiwa kuchochea zaidi matumizi ya gesi asilia nchini.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea kuimarisha matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya magari, viwanda, taasisi, migahawa na majumbani. Jumla ya vibali 14 vimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za gesi asilia iliyogandamizwa. Kati ya vibali hivyo, vibali sita ni vya ujenzi wa vituo vya gesi asilia iliyogandamizwa ikiwemo kituo kinachomilikiwa na Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania kinachojengwa eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vibali nane ni vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye vituo vinavyojengwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Tangi

Bovu – Mbezi Beach, Ubungo na Kipawa, na kupeleka gesi asilia kwa watumiaji wenye viwanda, taasisi, migahawa na majumbani.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; mradi wa kupeleka nishati ya umeme katika vitongoji vyote Tanzania Bara; na miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini pamoja na upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini.

**ARDHI**

**121.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuhakikisha matumizi bora ya ardhi, Serikali inaendelea kusimamia mpango wa kupima, kupanga na kumilikisha ardhi nchini. Lengo ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, kuipa thamani ardhi kuwa mtaji kwa wananchi kuweza kukopesheka na kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha imepima viwanja 7,550 katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma na Njombe. Kuhusu upangaji wa miji, michoro ya mipangomiji yenye viwanja 126,935 iliidhinishwa na hati miliki za viwanja 3,569,994 kubadilishwa kuwa za kidijitali.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya miundombinu na huduma za jamii hususan kwa maeneo ambayo yameendelezwa bila kupangwa, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Programu ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Makazi yasiyopangwa maeneo ya mijini. Vilevile, imeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 4,346 na kupima mipaka ya vijiji 10,744 kati ya 12,318.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha Mfumo wa kielektroniki wa e-Ardhi wa utunzaji taarifa za ardhi. Mfumo huo unatumika katika mikoa 7 ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Shinyanga, Tabora, Pwani na Mtwara na Halmashauri 20. Kupitia mfumo huo, jumla ya hatimiliki 863 zimesajiliwa.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za makazi. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ujenzi wa nyumba 5,000 za gharama ya kati na chini kupitia mradi wa *Samia Housing Scheme* ambapo Dar es Salaam zitajengwa nyumba 2,500 na tayari ujenzi wa nyumba 560 unaendelea na umefikia asilimia 80, Dodoma nyumba 1,000 na mikoa mingine nyumba 1,500.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuandaa na kukamilisha mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vilivyosalia; na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi wa kazi ikiwa ni pamoja na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali za ardhi.

**Maendeleo ya Viwanda na Biashara**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje ya nchi, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya uanzishaji wa viwanda nchini. Jumla ya leseni za viwanda 225 na vyeti vya usajili wa viwanda 29 vimetolewa.

**Ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na sukari inayotosheleza mahitaji ya wananchi kwa kufanya jitihada mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Kiwanda hicho, kilichozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 7 Agosti 2024-kina uwezo wa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka. Tayari kiwanda hicho kimeshazalisha tani 19,124 za sukari ya majumbani tangu kuanza rasmi uzalishaji Julai 2024 na kimetoa ajira rasmi 2,172 na zisizo rasmi zaidi ya 8,000.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imewezesha uanzishaji wa kiwanda cha kuunganisha magari aina ya HOWO cha Saturn kilichopo Mkoa wa Dar es Salaam; Kiwanda cha kuzalisha mafuta ya alizeti cha *Wild Flower and Grains LTD* kilichopo Mkoani Singida chenye uwezo kuzalisha tani 75 za mafuta kwa siku; na upanuzi wa kiwanda cha Maweni *Limestone* cha kuzalisha saruji aina ya

Huaxin kilichopo Mkoa wa Tanga. Viwanda hivyo vinatoa ajira 800 za muda na ajira 1,200 za kudumu.

**Ujenzi wa Kongani ya Viwanda Kwala**

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa mradi wa kongani ya viwanda ya Kwala wenye ukubwa wa ekari 2,500 na mtaji wa uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 327. Mradi huo unatekelezwa kwa awamu tano, ambapo awamu ya kwanza imefikia asilimia 80. Kongani hiyo inatarajiwa kuwa na jumla ya viwanda vikubwa na vya kati 200 na viwanda vidogo 300 vitavyohusika na usindikaji wa vyakula; na utengenezaji wa vifaa vya ujenzi, dawa, ngozi, nguo na kemikali.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, kukamilika kwa kongani ya viwanda kunatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja 100,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 500,000. Kukamilika kwa Kongani ya Kwala, kunatarajiwa kuzalisha bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 6 na kuchangia shilingi trilioni 1.2 kwa mwaka kwenye mapato ya kodi na ushuru.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imekamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Soko Huru la Afrika. Kukamilika kwa Mkakati huo kumehamasisha wafanyabiashara kusafirisha shehena ya bidhaa tofauti 21 katika nchi 18 za Afrika yenye uzito wa tani 1,000 na thamani ya Dola za Marekani milioni 9.36. Bidhaa zilizouzwa ni pamoja na nyuzi za katani, kahawa, viungo, parachichi, ngozi za mbuzi, ngozi za kondoo, tumbaku, mchele na vioo.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya kimkakati; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi; utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; kuhamasisha uzalishaji unaozingatia viwango vya kimataifa; kuongeza uwezo wa mifumo ya masoko nchini ikiwa ni pamoja mfumo wa stakabadhi za ghala; na kutumia fursa za diplomasia ya uchumi kupata masoko katika nchi mbalimbali.

**USAFIRI NA USAFIRISHAJI**

**133.** ***Mheshimiwa* Spika,** Serikali imeendelea kufanya utanuzi wa mtandao wa barabara ambapo katika mwaka 2024/2025, barabara zenye urefu wa kilometa 246 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 1,494.62 kwa kiwango cha changarawe. Aidha, imefanya matengenezo ya barabara kilometa 3,107.38 kwa kiwango cha lami na kilometa 5,193.09 kwa kiwango cha changarawe.

**134.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kutatua changamoto ya msongamano wa magari na kuboresha mfumo wa huduma za usafiri na usafirishaji katika majiji yenye msongamano ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mbeya. Kwa upande wa Dar es Salaam, awamu ya tatu ya ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka kutoka Posta hadi Gongolamboto yenye kilometa 23.3 umefikia asilimia 80 na awamu ya nne ya ujenzi wa barabara ya Kivukoni hadi Tegeta ya urefu wa kilometa 30.1 umefikia asilimia 22.2.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Jiji la Dodoma, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje yenye urefu wa kilometa 112.3. Ujenzi wa sehemu ya kwanza kutoka Nala — Veyula — Mtumba — Ihumwa Bandari Kavu (km 52.3) umefikia asilimia 84.72, na kwa sehemu ya pili kutoka Ihumwa Bandari Kavu — Mtumba — Matumbulu — Nala (km 60) umefikia asilimia 81.5. Kwa Jiji la Mbeya, ujenzi wa njia nne za barabara kutoka Nsalaga (Uyole) mpaka Ifisi (Kiwanja cha Ndege cha Songwe) yenye urefu wa kilometa 29 umefikia asilimia 22.

**Miradi ya Dharura**

**136.** ***Mheshimiwa* Spika,** kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kufanya ukarabati wa barabara na miundombinu iliyoathirika kufuatia mvua za EL-NINO zilizonyesha nchini kuanzia Septemba, 2023 hadi Mei, 2024 pamoja na kimbunga Hidaya. Jumla ya kilometa 520, makalavati na madaraja 189 katika barabara 342 kwenye mikoa 26 ziliathirika na hivyo kuathiri huduma za usafiri na usafirishaji.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kurejesha hali, Serikali ilitoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 72.15 kwa ajili ya kurejesha miundombinu hiyo kwa dharura. Pia, imetoa fedha nyingine kiasi cha shilingi bilioni 868.56 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kudumu katika maeneo yaliyoathirika.

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, nchi jirani pamoja na barabara za ulinzi kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo miundombinu ya vivuko na madaraja ili kuunganisha maeneo ya nchi kavu ambayo yametenganishwa na maji katika maeneo ya bahari, maziwa na mito.

**UCHUKUZI Viwanja vya Ndege**

**139.** ***Mheshimiwa*** **Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuhakikisha huduma ya usafiri wa anga inaimarika na kuleta manufaa kwa wananchi. Ili kufikia azma hiyo, inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja katika mikoa mbalimbali hapa nchi. Viwanja hivyo ni pamoja na Kiwanja cha Ndege Tabora asilimia 90, Kiwanja cha Ndege Shinyanga asilimia 76, Kiwanja cha Ndege cha Musoma kilichofikia asilimia 57, Kiwanja cha Ndege Sumbawanga asilimia 50 na Kiwanja cha Ndege Kigoma asilimia 16. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa ambao umefikia asilimia 93 na safari za ndege zimeanza. Aidha, kwa upande kiwanja cha ndege cha Arusha, ujenzi wa jengo la abiria na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA umekamilika na ufungaji wa taa za kuongezea ndege utakaowezesha kiwanja hicho kutoa huduma kwa masaa 24 unaendelea.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, hatua nyingine ni kuimarisha huduma za usafiri wa anga kwa kufunga mitambo ya mawasiliano ya sauti ya baina ya waongoza ndege na marubani katika viwanja vya ndege 12 pamoja na vituo 18. Mitambo hiyo imeongeza ufanisi baina ya waongoza ndege na marubani.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Cha Msalato, Dodoma**

**141. *Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Jijini Dodoma unaotekelezwa kwa awamu mbili unaendelea. Hadi Februari 2025, ujenzi wa awamu ya kwanza unaohusisha barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara za maungio na kuingia na kutoka uwanjani, maegesho ya ndege na magari, uzio wa usalama, na usimikaji wa taa za kuongozea ndege umefikia asilimia 85.4. Aidha, awamu ya pili inayohusisha jengo la abiria na majengo mengine ya kiwanja umefikia asilimia 51.4. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hicho kutaboresha usafirishaji wa watu na bidhaa ndani na nje ya nchi; kuunganisha makao makuu ya nchi na maeneo mengine ya ndani na nje ya nchi; na kuchochea ukuaji na uimarishaji wa shughuli za kiuchumi, kijamii na kiutawala.

**Usafiri kwa Njia ya Maji**

**142. *Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa usafiri wa njia za maji katika maziwa makuu, Serikali imeendelea kufanya maboresho kwa kukamilisha ukarabati wa Bandari ya Kemondo. Vilevile inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa Bandari ya Bukoba ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 85, Bandari ya Mwanza North asilimia 48, na Bandari ya Mbambabay asilimia 20.

**Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala**

**143. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari kavu ya Kwala kwa lengo la kupunguza msongamano wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam, msongamano wa meli kusubiri kushusha shehena, na foleni katikati ya Jiji la Dar es Salaam.Ujenzi huo unatekelezwa kwa awamu mbili kwa gharama ya shilingi bilioni 83.246. Tayari awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi huo imekamilika na imeshapokea makasha 700.

**144. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa; kuimarisha miundombinu ya bandari; kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania; ukarabati wa meli zilizopo na ujenzi wa meli mpya; na kuendelea na ujenzi wa bandari kavu ya Kwala.

**Huduma za Hali ya Hewa**

**145. *Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa. Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji na kutoa taarifa kupitia tafiti za kisayansi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa. Uwepo wa rada katika Mikoa ya Mbeya na Kigoma umewezesha nchi yetu kuwa na jumla ya rada tano za hali ya hewa zinazosaidia kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

**MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**146. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kukabiliana na kasi ya maendeleo ya mawasiliano na teknolojia, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha nchi yetu inanufaika na maendeleo hayo ya teknolojia. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hadi kufikia Februari, 2025 kilometa 13,820 kati ya 16,280 zimejengwa na kuunganisha wilaya 109 kati ya 139 pamoja na vituo 111 vya kutolea huduma za Mawasiliano.

**147. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeanza kuchukua hatua za utekelezaji wa ujenzi wa Mkongo wenye urefu wa Kilometa 186 kutoka Kigoma Tanzania hadi Kalemie, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kupitia Ziwa Tanganyika. Aidha, jitihada hizo zimeenda sambamba na kuimarisha utoaji wa huduma za mawasiliano pamoja na ujenzi wa minara. Tayari minara 414 imeshajengwa sawa na asilimia 54.62 ya minara 758 inayotarajiwa kujengwa.

**148. *Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, imeunganisha mifumo 898 ili kuhakikisha lengo la mifumo ya TEHAMA kubadilishana taarifa linafikiwa. Kati ya mifumo hiyo, 514 ni mifumo ya Serikali na 384 ni mifumo ya sekta binafsi. Ukamilishwaji wa zoezi hili utawezesha kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

**149. *Mheshimiwa Spika,*** jitihada zinazofanyika ni sehemu ya utekelezaji wa vitendo wa maelekezo ya Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliagiza ifikapo Desemba 2024, mifumo ya TEHAMA

Serikalini iwezeshwe kubadilishana taarifa. Hadi sasa, jumla ya mifumo 202 ya Taasisi za Umma 179 imeunganishwa na inabadilishana taarifa kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini. Mojawapo ya mifumo inayobadilishana taarifa ni mifumo ya Taasisi za Sekta ya Haki Jinai zinazojumuisha Mahakama, TAKUKURU, Polisi na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya hayo, Serikali inaendelea kuimarisha mfumo wa anwani za makazi kwa kuhakiki na kusajili taarifa za maeneo ya makazi. Hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya anwani 3,057,295 zimehakikiwa na anwani 535,276 zimesajiliwa na kufanya idadi ya anwani zilizohakikiwa kufikia 12,853,077. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha usalama wa mfumo wa kidijitali wa anwani za makazi pamoja na moduli ya kukusanya taarifa za anwani za makazi ili kujumuisha mahitaji ya wadau.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali; itaendelea kuboresha na kuhuisha mifumo ya TEHAMA jumuishi, mifumo ya kisekta na mifumo ya kitaasisi inayotumika, itadhibiti usalama wa taarifa za Serikali dhidi ya matishio ya kiusalama mtandaoni kwa kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao, itaimarisha tathmini ya hali ya usalama mtandaoni pamoja na upatikaji huduma za mawasiliano ya simu na posta nchini. Kadhalika, itaweka mazingira wezeshi kwa ajili kukuza na kuimarisha biashara mtandaoni; kuchochea ubunifu; kuimarisha ustawi wa kampuni changa na kuendeleza utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA.

**HUDUMA ZA JAMII Elimu**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuimarisha sekta ya elimu nchini kwa kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora yenye tija inayokidhi mahitaji ya soko la ajira. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha sera na mitaala, kuongeza fursa za elimu ya amali, msingi, sekondari, ualimu na elimu ya juu, pamoja na kuendeleza utafiti, matumizi ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya viwanda.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeandaa na kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023), pamoja

na Mitaala ya Elimu ngazi ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono haya makubwa yenye lengo la kufanya elimu inayotolewa hapa nchini iwiane na mahitaji ya sasa kitaifa, kikanda na kimataifa lakini pia, kuendana na mabadiliko na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

***Elimu ya Msingi na Sekondari***

**154. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatinakaji wa elimu ya msingi na sekondari, na kuboresha mazingira ya kufujifunzia na kufundishia, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu muhimu ya shule za msingi na sekondari. Hadi Februari, 2025 jumla ya shilingi bilioni 24.92 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya, umaliziaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na miradi viporo katika shule za msingi na sekondari.

**155. *Mheshimiwa Spika,*** kadhalika inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa shule 103 za sekondari za amali ambapo shule 29 ni za kihandisi na 74 za kawaida. Aidha, inaendelea kukamilisha ujenzi wa madarasa 1,897, mabwalo 241 na mabweni 126.

**156. *Mheshimiwa Spika***, sambamba na utekelezaji wa miradi ya ujenzi, Serikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia vikiwemo vitabu. Jumla ya nakala 12,047,829 za vitabu vya kiada na nakala 9,902,102 za vitabu vya sekondari vimesambazwa kwa wanafunzi. Idadi hiyo ni pamoja na vitabu vya maandishi yaliyokuzwa na breli kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

***Elimu ya Kati na Elimu ya Juu***

**157. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha elimu ya kati nchini kwa kuboresha miundombinu ya vyuo vya elimu hiyo. Tayari imekamilisha ujenzi wa vyuo vipya 29 vya ufundi stadi ambavyo vimechangia kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi wa ufundi stadi kutoka 415,131 mwaka 2023/2024 hadi 425,509 mwaka 2024/2025.

**158. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyuo 65 vya mafunzo ya ufundi stadi ambao upo hatua

mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo, inatekelezwa kwa lengo la kuwaandaa wahitimu kumudu mahitaji ya soko la ajira.

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa elimu ya juu, Serikali imeongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 738.7 mwaka 2023/2024 hadi shilingi bilioni 787 mwaka 2024/2025. Aidha, wanufaika wa mikopo wameongezeka kutoka wanafunzi 224,056 mwaka 2023/2024 hadi wanafunzi 245,799 mwaka 2024/2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali, kununua vifaa vya kufundishia kwa vyuo vya VETA na vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, kuendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi, kuongeza mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya kati na elimu ya juu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kuimarisha mafunzo kwa walimu, kuongeza uwiano wa vitabu kwa wanafunzi na kuimarisha elimu maalum, na kuongeza bajeti ya fedha za mikopo na ufadhili wa wanafunzi.

**Maji**

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ambayo nimeeleza awali, katika mwaka 2024/2025, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa Same – Mwanga – Korogwe. Vilevile, miradi ya Mugango – Kiabakari – Musoma na kukamilika kwa uchimbaji wa visima 925, ambapo kila jimbo la uchaguzi Tanzania Bara limepata wastani wa visima vitano vya maji.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Miji 28 ya Tanzania Bara ambao umefikia kati ya asilimia 14 na asilimia 68.95 za utekelezaji. Mradi huo ukikamilika utanufaisha wananchi wapatao 5,985,500.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji wa mradi huo, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda lililopo Mkoani Morogoro. Bwawa hilo litakuwa na uwezo wa kutunza lita

bilioni 190 za maji. Utekelezaji wa mradi huo uliofikia asilimia 28, utagharimu shilingi bilioni 329.46. Mradi huo utakapokamilika unatarajiwa kupunguza athari za kimazingira kwa kuimarisha utiririshaji wa maji katika mkondo wa Mto Ruvu kwa kipindi chote cha mwaka ili kulisha mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Chini na kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kukamilishaji miradi mikubwa ya maji, kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika utekelezaji na uendeshaji wa miradi ya maji na kuimarisha ufuatiliaji wa ubora wa maji yanayotumiwa na wananchi.

**Afya**

**165.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa huduma za afya, Serikali imeendelea kutekeleza mipango na mikakati mahsusi ya kusimamia ubora, usalama na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha huduma za kinga; huduma za afya ya uzazi na mtoto; kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya; pamoja na kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi. Vilevile, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya; Mifumo ya TEHAMA inayowezesha utoaji wa huduma za afya na matumizi ya takwimu; na utawala bora na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote.

**166.** ***Mheshimiwa Spika*****,** hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya shilingi bilioni 74.85 zimetolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati 7, vituo vya afya 41 na hospitali 89 za halmashauri. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo, kutasaidia kusogeza huduma za afya ya msingi karibu na wananchi na hivyo kuwapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya. Vilevile, Serikali imetoa shilingi bilioni 45.13 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye zahanati 356, vituo vya afya 41 na hospitali za halmashauri 119.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hatua hizo, Serikali imeendelea kuboresha na kuweka mfumo wa uendeshaji na

usimamizi wa utoaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya vituo 4,813, sawa na asilimia 67 ya vituo vya umma ngazi ya afya msingi vinatumia mfumo huo. Kati ya vituo hivyo, hospitali za wilaya ni 185, vituo vya afya 836, zahanati 3,778, kliniki 7 na hospitali teule za wilaya 7 ambapo wagonjwa zaidi ya milioni 6 wamepata huduma kupitia mfumo huu na rufaa 10,264 zilitolewa kwa wagonjwa. Matumizi ya mfumo huo yamesaidia kudhibiti upotevu wa dawa na vifaa tiba, kudhibiti na kuongeza makusanyo ya ada za kuchangia huduma na ubadilishanaji na utoaji wa taarifa kwa wakati.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2025/2026, itaendelea kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa; kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi taifa; kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini; kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto; kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini; na kusimamia tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa takwimu zilizopo watu 1,690,948 wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU). Kadhalika, WAVIU 1,545,880 wanatumia dawa za kufubaza makali ya VVU ambapo watu wazima wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ni asilimia 96.4.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** kiwango cha maambukizi mapya ni watu 60,000 kila mwaka ambapo vijana wanaopata VVU maambukizi ni takribani asilimia 34.3 ya maambukizi mapya. Nitoe rai kwa Watanzania wote kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa UKIMWI bado ni tishio kama takwimu zinavyoonesha.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuratibu shughuli za UKIMWI kwa kutoa huduma endelevu na stahimilivu kwa WAVIU; kuimarisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ili uweze kufanikisha malengo ya nchi katika kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030; kuweka msukumo katika

kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; kuhamasisha mabadiliko ya tabia katika jamii ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, Serikali inatambua mabadiliko ya sera za misaada kutoka kwa baadhi ya wafadhili wetu wa muda mrefu wa masuala ya UKIMWI. Kufuatia mabadiliko hayo, Serikali inachukua hatua madhubuti kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha uwekezaji kwenye eneo la utaoji huduma kwa WAVIU. Hatua hizo zenye lengo la kuwezesha Taifa letu kujitegemea zitaendelea kuchukuliwa pia katika maeneo mengine. Niwahakikishie Watanzania wote, kuwa, Serikali itaendelea kuhakikisha huduma zinazohusiana na masuala ya UKIMWI zinaendelea kupatikana na hakuna Mtanzania atakayekosa huduma hizo.

**Huduma kwa Makundi Maalum**

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali kwa kushirikiana na wadau wote muhimu, imeendelea kuhamasisha ushiriki wa jamii katika maendeleo, kukuza usawa wa kijinsia, kuimarisha huduma za ustawi wa jamii pamoja na kuendeleza makundi maalum. Jitihada zinazofanywa na Serikali ni katika kuhakikisha uwepo wa elimu kuhusu maendeleo ya jamii, ushiriki wa kila mwananchi katika kulinda misingi ya maisha inayozingatia tamaduni sahihi, malezi bora na kutunza amali za Taifa.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua mojawapo iliyochukuliwa ni kuimarisha mifumo ya kisheria kwa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mtoto Sura ya 13 ili kuboresha mifumo ya haki na ulinzi wa watoto. Aidha, katika kuhakikisha malezi bora, Serikali imeratibu mafunzo kwa maafisa 281 wa mikoa na halmashauri kuhusu sayansi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, imetoa mafunzo kuhusu usalama wa watoto kwa walimu 3,500 na kusajili vituo 552 vya kulelea watoto wadogo mchana hivyo kufikia vituo 4,193 nchi nzima na kutoa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Vilevile, Serikali imeanzisha madawati 1,039 ya ulinzi na usalama wa mtoto,

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuyafikia makundi mbalimbali katika jamii, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa kuwatambua, kuwasajili na kuwaendeleza wafanyabiashara ndogondogo. Hadi Februari 2025, tayari wafanyabiashara 63,222 wamesajiliwa. Aidha, shilingi bilioni 8 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo. Hadi kufikia Februari, 2025 wafanyabiashara ndogondogo 1,008 wamepata mikopo hiyo.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua umuhimu na inathamini mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kutokana na umuhimu huo, imeendelea kuimarisha usimamizi na uratibu wa mashirika hayo ili yaweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

**178. 178.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi kuanzia Julai 2024 hadi Februari 2025, Serikali imesajili mashirika 939. Mashirika hayo yametelekeza jumla ya miradi 405 iliyochangia upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo afya, elimu, utunzaji wa mazingira, haki za binadamu na utawala bora kwa gharama ya shilingi bilioni 342.07. Aidha, kulingana na tathmini ya mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali kwa mwaka 2023, jumla ya shilingi trilioni 2.6 zilitumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuimarisha ulinzi wa mtoto na makundi maalum, utoaji wa huduma ya afya kwa wazee, utoaji wa huduma za ustawi wa jamii. Vilevile, itaendelea kuwatambua na kuwaendeleza wafanyabiashara ndogondogo na kuboresha mazingira ya kujifunzia katika vyuo vya ustawi wa jamii.

**HALI YA SIASA NA DEMOKRASIA NCHINI**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya siasa na utekelezaji wa demokrasia hapa nchini imeendelea kuimarika kutokana na maboresho ya mifumo na jitihada mbalimbali za makusudi zinazofanywa na Serikali. Moja ya jitihada hizo ni marekebisho ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utawala wa demokrasia hapa nchini. Aidha, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 1 ya Mwaka 2024; Sheria

ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 2 ya Mwaka 2024 na kufanya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258. Serikali kwa upande wake tayari imeshakamilisha utungaji wa Kanuni za Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeendelea kufanya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa kuratibu na kusimamia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura. Hadi Machi, 2025 uboreshaji awamu ya kwanza umekamilika katika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar na maandalizi ya awamu ya Pili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura yanaendelea. Nitumie nafasi hii kutoa rai kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza kuhakiki taarifa zao kwenye daftari kabla kuhitimishwa kwa awamu ya pili ya uboreshaji.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, hadi kufikia Machi, 2025, Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 13.17 kwa vyama vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku. Hatua hiyo, imeendelea kusaidia kuimarisha na kuendeleza uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa nchini. Sambamba na hilo, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia Baraza la Vyama vya Siasa imetoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa vyama vya Siasa ili kukuza uelewa juu ya uendeshaji wa shughuli za vyama.

**URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI BUNGENI**

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Ofisi ya Bunge imeendesha mikutano mitatu ya Bunge yaani Mkutano wa 16, 17 na 18. Katika mikutano hiyo, jumla ya maswali ya msingi 546 na maswali ya nyongeza 1,725 yaliulizwa Bungeni na kupatiwa majibu na Serikali na maswali 25 ya papo kwa papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Miswada 15 ya sheria ilijadiliwa na kupitishwa na Miswada 9 ilisomwa kwa mara ya kwanza. Pia, Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la Bunge la tarehe 31 Januari, 2025 la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika (Mission 300) kwa mwaka 2025.

**ULINZI NA USALAMA**

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utulivu wa kisiasa, hali ya usalama na amani imeendelea kuimarika nchini na katika mipaka yote ya nchi yetu inayohusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji. Ninavipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa jitihada kubwa inazoendelea kuzichukua ili kuhakikisha hali ya ulinzi, usalama, amani na utulivu vinaendelea kuimarika hapa nchini. Jitihada hizo zimechangia kuiletea sifa za kidiplomasia nchi yetu na kukuza shughuli za kiuchumi na kijamii.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika hatua nyingine, imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika kuhakikisha ulinzi wa amani. Kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania nchi yetu imeendelea kushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya misheni za Umoja wa Mataifa katika Mataifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Afrika ya Kati na Lebanon. Vilevile, imeshiriki kupitia misheni ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya kuimarisha amani katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, maafisa wanadhimu na makamanda wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wameendelea kushiriki kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan, Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na DRC. Ushiriki wa vyombo vyetu mbalimbali katika operesheni hizo, umeiwezesha nchi yetu kuimarisha diplomasia ya ulinzi, uhusiano, ushirikiano na kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda ya kushiriki katika ulinzi wa amani kimataifa na kikanda.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine,_Serikali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) imeendelea kuwapatia vijana mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Kuanzia Julai 2024 hadi Februari 2025 vijana 23,540 wa kujitolea walipatiwa mafunzo hayo ambapo wavulana ni 15,514 na wasichana ni 8,026.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao utendaji wa makosa ya jinai umeendelea kupungua hapa nchini. Aidha, idadi ya makosa makubwa

yaliyoripotiwa imepungua kutoka makosa 28,785 ikilinganishwa na makosa 30,112 yaliyoripotiwa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Februari, 2024. Hii inaonesha kuwa uhalifu umepungua kwa asilimia 5.6.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kupunguza idadi ya wafungwa magerezani kwa utaratibu wa kutoa adhabu mbadala. Hadi kufikia mwezi Februari 2025, jumla ya wafungwa 1,415 walinufaika na utaratibu wa kifungo cha nje na wafungwa 112 waliachiliwa kupitia huduma za Parole. Aidha, jumla ya wafungwa 1,548 waliachiwa huru kupitia msamaha wa Rais.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutekeleza majukumu yake yakuokoa maisha ya watu na mali zao. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari, 2025, Jeshi limefanikiwa kuzima moto kwenye matukio 1,734 na kufanya uokoaji katika matukio 620. Vilevile, Jeshi limefanya ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto na majanga mengine katika maeneo 44,555.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji imeendelea kuimarisha shughuli za kutoa huduma za nyaraka mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari, 2025 jumla ya pasi za kusafiria 94,672; visa 793,028; hati za ukazi 15,035 zimetolewa ikilinganishwa na pasi za kusafiria 114,482; visa 669,998; hati za ukazi 15,368 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeendelea kusajili na kutambua watu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Februari, 2025, imesajili watu 545,065 na kufanya watu waliosajiliwa tangu mwaka 2012 kufikia 25,555,038, sawa na asilimia 81.2 ya watu 31,477,938 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari, 2025, NIDA imeunganisha taasisi 16 katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi na kufanya taasisi zilizounganishwa kufikia 124. Uunganishaji wa taasisi umewezesha taasisi hizo kufanya uhakiki wa taarifa za wateja kabla ya kutoa huduma na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi, kijamii na kuimarisha usalama.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kuliimarisha Jeshi la Ulinzi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa pamoja na kushiriki katika misheni za kikanda na kimataifa katika masuala ya ulinzi wa amani. Pia, itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa wafungwa na mahabusu kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na utekekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai; kuendelea kuzuia makosa ya jinai kwa kuimarisha huduma za Jeshi la Polisi; kuendelea kutoa vitendea kazi, kujenga na kukarabati miundombinu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; na kuendelea kuboresha miundombinu na Mfumo wa Uhamiaji kwa kuzingatia viwango vya teknolojia ya kisasa.

**MASUALA YA KAZI NA WAFANYAKAZI**

**196.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutambua umuhimu wa wafanyakazi katika kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ushughulikiaji maslahi ya wafanyakazi, kuwajengea uwezo, pamoja na kuwapatia vitendea kazi.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mifumo, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Sura 366, Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300, na Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 ili kukidhi mahitaji ya sasa. Moja ya marekebisho makubwa yaliyofanyika ni pamoja na kuboresha haki ya likizo ya uzazi kwa mama atayejifungua mtoto njiti. Hivi sasa, likizo ya uzazi ya mama atakayejifungua mtoto njiti itaanza baada ya mtoto kufikisha wiki 40 badala ya wiki 36.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imeandaa mfumo wa kielekroniki (oCMS) unaolenga kuimarisha shughuli za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inayohusika na migogoro ya kikazi kwa njia ya kidijitali. Mfumo huo utarahisisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri kwa kupunguza muda na gharama na hivyo kuongeza ufanisi.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari, 2025, Serikali imepandisha vyeo watumishi 290,625 wa kada mbalimbali. Pia, imelipa fedha, kiasi cha shilingi bilioni

130.4 kwa watumishi wa umma 100,684 waliokuwa na madai mbalimbali.

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchua hatua mahsusi ili kuongeza ufanisi na tija katika sehemu za kazi na kupunguza migogoro na migongano ya mara kwa mara baina ya Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, lakini pia kwa Vyama vya Wafanyakazi vyenyewe. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Majadiliano baina ya Serikali, Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri. Mwongozo huo umeandaliwa ili kuweka misingi bora ya majadiliano kwa lengo la kujenga uelewa na mtazamo wa pamoja kuhusu masuala muhimu ya maendeleo yanayohusu Serikali, Wafanyakazi na Waajiri.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia sheria za kazi kwa kufanya kaguzi 5,809 na kutoa elimu kuhusu masuala ya kazi kwa waajiri 3,802 na wafanyakazi 14,291. Kaguzi hizo zimesaidia kuimarisha uzingatiaji wa sheria za kazi na kuimarisha mazingira ya kazi.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imetoa vibali 10,754 vya kazi kwa wageni vilivyowezesha kuongeza fursa za ajira kwa wazawa. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya wageni 10,498 na wazawa 224,147 walipata ajira.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2025/2026, itaendelea kuweka mazingira bora ya kufanya kazi, kushughulikia changamoto mbalimbali ili wafanyakazi wote wafanye kazi kwa weledi, uzalendo, juhudi, uadilifu na uwajibikaji.

**USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa taratibu zilizowekwa kuhusu kulinda afya na usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi zinafuatwa na kuzingatiwa wakati wote wanapokuwa mahali pa kazi. Katika kipindi cha mwaka 2024/2025, Serikali kupitia OSHA imefanya kaguzi maalum 211,906 katika maeneo 13,003. Maeneo hayo ni pamoja na viwanda, migodi na sekta ya usafirishaji. Pia imefanya uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi 283,083 na kutoa ushauri stahiki. Kati ya hao

wafanyakazi 122,023 walibainika kuwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na usikivu mdogo, uzito uliokithiri, uzito usiofikia kiwango pamoja na uoni hafifu.

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Serikali itafanya kaguzi 350,000 katika maeneo 25,000, kupima afya za wafanyakazi 400,000 na kutoa mafunzo kwa waajiri na wafanyakazi na wajasiriamali wapatao 40,000.

**MAENDELEO YA VIJANA**

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa maendeleo ya vijana, Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, kujipatia ajira na kujikwamua kiuchumi. Katika mwaka 2024/2025 Serikali imezindua Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007, Toleo la 2024 pamoja na mkakati wake. Sera hiyo imezingatia mazingira na mahitaji ya vijana ikiwemo elimu na ujuzi kwa vijana; uvumbuzi na ubunifu kwa vijana; vijana na mapinduzi ya kidijitali; ajira kwa vijana; na ushiriki wa vijana katika sekta za kijamii na kiuchumi.

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/2026, Serikali itatekeleza programu za stadi za maisha, malezi na makuzi na uratibu wa maendeleo ya vijana; na kuendelea kuhamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuweza kujipatia ajira na kuinua kipato chao.

**HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU**

**208.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha utoaji wa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha jamii ya Watu Wenye Ulemavu inaishi katika mazingira salama na kushiriki katika shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu, Serikali imezindua Mpangokazi wa Taifa wa Ustawi na Haki kwa Watu Wenye Ualbino kwa Mwaka 2024/2025 – 2028/2029. Mpangokazi huo, unaainisha hatua zinazohitajika katika kuzuia, kukabiliana na kutokomeza ukatili kwa Watu Wenye Ualbino.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali ilizindua Mkakati wa Taifa wa Teknolojia Saidizi 2024 – 2027 ambao unatoa mwongozo wa kimkakati kwa sekta zote kuweka mazingira wezeshi ili kila Mtanzania mwenye uhitaji wa teknolojia saidizi aweze kupata kwa wakati na kwa gharama nafuu. Aidha, Serikali ilizindua kanzidata na Mfumo wa Taarifa za Watu Wenye Ulemavu unaotokana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 utakaowezesha matumizi ya Takwimu ya Sensa katika kutayarisha programu za kuwawezesha na kuwajengea uwezo Watu Wenye Ulemavu kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali na wadau wa maendeleo kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kimazingira.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuratibu utoaji wa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu kwa kuboresha na kutekeleza Sera, Sheria, mikakati na mipango mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuimarisha ushiriki wao katika nyanja zote.

**HUDUMA ZA KINGA YA JAMII**

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya kinga ya jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Huduma hiyo imekuwa ikitolewa kwa wananchi ambao ni watumishi walioko kazini, waliostaafu na kaya maskini.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Februari, 2025 huduma imetolewa kwa wananchi wasiopungua milioni 16,506,583 kwa huduma ya kinga ya jamii ya uchangiaji na isiyo ya uchangiaji. Aidha, Serikali imeandaa mfumo wa uratibu wa kinga ya jamii ambao utarahisisha uratibu na utekelezaji wa afua za kinga ya jamii kwa kuwaleta pamoja wadau wanaohusika katika masuala ya kinga ya jamii.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za kinga ya jamii nchini kwa kuboresha mafao kwa kuongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000 hadi Shilingi 150,000 kwa mwezi na kuhuisha

pensheni ya kila mwezi kwa kiwango cha asilimia 2 kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) imelipa mafao kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika 23,187 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.17 na pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 175,806 kwa wastani wa shilingi bilioni 72.49 kila mwezi. Vilevile, kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) imelipa mafao ya shilingi bilioni 539.52 kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika 110,080. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 79.8 zililipwa kama pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 33,840 ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni 12 kila mwezi.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)* umelipa mafao ya fidia jumla ya shilingi bilioni 7.66 kwa wanufaika wa Mfuko. Kiasi cha fidia kilicholipwa kinajumuisha malipo ya pensheni ya kila mwezi kwa wanufaika 2,237, kati ya hao wanufaika 516, ni wenye ulemavu, wanufaika 1,692 ni wategemezi na wanufaika 29 ni wanaohudumia wagonjwa wasiojiweza. Aidha, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi umeandaa Kanuni za utoaji fao la utengemao ambapo wafanyakazi waliopata ulemavu wakiwa kazini watapatiwa mafunzo ya ujuzi mbadala yatakayowawezesha kuendelea kufanya kazi na kupata kipato.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** mifuko ya hifadhi ya jamii imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kusajili wanachama wapya na kukusanya mapato. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umesajili wanachama wapya 28,498 na kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 1.46. Vilevile, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umesajili wanachama wapya 242,031 kutoka sekta rasmi na sekta isiyo rasmi na kukusanya kiasi cha ya shilingi trilioni 1.48 kutoka kwa waajiri na wanachama wake. Aidha, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umesajili waajiri wapya 2,875 na kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 47.05 kutoka kwa waajiri.

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuboresha na kusimamia programu na mikakati mbalimbali ya kinga ya jamii nchini ikiwemo kulipa mafao ya

wastaafu kwa wakati na kutoa elimu ya mpango wa kinga ya jamii kwa wananchi hususan sekta isiyo rasmi.

## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

### Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF)

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini awamu ya tatu kwa maeneo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka 2024/2025 jumla ya shilingi bilioni 106.3 zimehawilishwa kwa kaya za walengwa 926,054. Vilevile, Serikali imeboresha mfumo wa malipo kwa kaya za walengwa 428,570. Mfumo unaotumika sasa ni wa malipo ya kielektroniki ambapo baada ya kuzisajili kaya hizo malipo ya fedha hutumwa moja kwa moja kupitia mitandao ya simu na benki.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuwezesha kaya za walengwa kutekeleza miradi ya kijamii ili kuongeza kipato chao. Jumla ya miradi ya maendeleo 181 ilitekelezwa na kuwezesha kaya hizo kulipwa jumla ya shilingi bilioni 18.88. Kutokana na jitihada hizo, walengwa 394,505 waliimarika kiuchumi na hivyo kuwa tayari kutolewa kwenye mpango kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari 2025.

### Utoaji wa Mikopo ya asilimia 10 kwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfuko wa asilimia 10 wa uwezeshaji wananchi kiuchumi umeboreshwa kwa kuanzishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa Wezesha Portal. Mfumo huo, umewezesha kuondoa changamoto zilizokuwepo awali ikiwa ni pamoja kuondoa vikundi hewa, watu kujisajili katika kikundi zaidi ya kimoja na wakopaji hewa. Vilevile, matumizi ya Mfumo huo yamewezesha kuongeza idadi ya wanufaika kwa asilimia 50, kupungua kwa muda wa kuchakata maombi kwa asilimia 85 sambamba na kuhakikisha urejeshaji wa mikopo kwa wakati.

**221.** ***Mheshimiwa*** **Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 82.84 kwa vikundi 8,275 vya wanawake, vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 40.71 zimetolewa kwa

vikundi 4,557 vya wanawake, shilingi bilioni 36.64 kwa vikundi 2,827 vya vijana na shilingi bilioni 5.48 kwa vikundi 891 vya Watu Wenye Ulemavu kwa kuzingatia utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo hiyo wa Wezesha Portal uliooboreshwa.

**222. *Mheshimiwa Spika,*** sina shaka nyote mtakubaliana nami kwamba maboresho yaliyofanyika yametokana na jitihada za makusudi za Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwezesha kufanyika kwa maboresho ya Mfuko wa Asilimia 10 ambao umewezesha vijana wa Kitanzania kunufaika na mikopo hiyo kwa kuanzisha miradi mbalimbali ikiwemo usafirishaji wa bodaboda, mama na baba lishe na kuwawezesha wafanyabiashara ndogondogo (wamachinga) kujiajiri. Aidha, nitoe rai kwa vijana hao kuhakikisha wanatumia fedha za mikopo hiyo kwa shughuli zilizokusudiwa na kuzirejesha ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na mikopo hiyo.

**223. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuzihudumia kaya za walengwa zilizopo kwenye mpango kupitia utoaji wa ruzuku ili ziweze kukidhi mahitaji ya msingi; kutoa fursa za ajira ya muda kwa kaya za walengwa ili kuongeza kipato kwa kushiriki katika kufanya kazi katika miradi iliyoibuliwa na jamii; na kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi ya vijana, wanawake na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Asilimia 10.

**Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050**

**224. *Mheshimiwa Spika,*** ni ukweli usiopingika kuwa mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu ni muhimu kwa mwelekeo wa nchi. Kwa msingi huo, Serikali iliendelea kufanya maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo itatoa mwongozo wa mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. Mchakato wa maandalizi ulihusisha kukusanya maoni ya wadau mbalimbali pamoja na wananchi na hatimaye kukamilisha rasimu ya Dira 2050 iliyozinduliwa rasmi na Mheshimiwa *Dkt*. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**225. *Mheshimiwa Spika,*** rasimu hiyo imezingatia ukuaji wa uchumi utakaofungamanishwa na sekta za uzalishaji; uimarishaji wa sekta binafsi; na kuimarisha uwekezaji na usimamizi katika Mashirika ya umma. Sambamba na dira hiyo, Serikali imeanza maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027 ambao utakuwa mpango wa kwanza katika utekelezaji wa Dira 2050 na Mpango wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031.

**Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**226. *Mheshimiwa Spika,*** rushwa ni adui wa haki. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ili kuhakikisha kunakuwa na usawa katika kutoa na kupokea huduma pamoja na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hatua za Serikali zinalenga kuimarisha eneo la uzuiaji rushwa ili kudhibiti vitendo hivyo kabla na wakati havijafanyika katika maeneo ya kutolea huduma. Hatua za udhibiti zinatekelezwa sambamba na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya rushwa.

**227. *Mheshimiwa Spika,*** kiasi cha shilingi bilioni 3.35 na Dola za Marekani 620,000 ziliokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi uliofanyika nchini. Hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na rushwa zimeleta nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Jumla ya kesi 760 zimeendeshwa mahakamani katika mwaka 2024/2025 zikiwemo kesi mpya 357. Kati ya kesi hizo, kesi 345 ziliamuliwa ambapo Jamhuri ilishinda kesi 268.

**228. *Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada zilizofanyika, nchi yetu imeendelea kupata sifa nzuri kikanda na kimataifa. Kwa mujibu wa Taarifa ya '*Transparency International*' ya mwaka 2024, Tanzania kupitia kiashiria cha "*Corruption Perception Index*" imefanya vizuri kwa kupata alama 41 na kushika nafasi ya 82 kati ya nchi 180 ikilinganishwa na alama 40 na nafasi ya 87 ya mwaka 2023/2024. Matokeo hayo yameipandisha Tanzania kwa nafasi tano.

**229. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi. Kipaumbele kitawekwa katika utoaji wa elimu kwa umma juu ya madhara ya

rushwa; kuchambua na kubainisha maeneo yanayohitajika kuimarishwa kwenye mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma; na kuendeleza uchunguzi na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wa rushwa.

**Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya**

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini na duniani kwa ujumla limekuwa likiongezeka na kusababisha athari nyingi kwa wananchi hususan kundi la vijana. Hivyo basi, udhibiti wa dawa za kulevya ni muhimu ili kulinda vijana ambao ni nguvukazi ya taifa inayoathirika zaidi. Pia, ni muhimu katika kuongeza afya ya jamii kwa kupunguza uraibu na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, kuongeza amani na usalama kwa kupunguza uhalifu, pamoja na kuimarisha sifa za Taifa letu kimataifa.

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali hiyo imeilazimu Serikali kuendelea kubuni mikakati mbalimbali ya kukabiliana na tatizo hilo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Hadi kufikia Februari 2025, Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola ilifanikisha ukamataji wa dawa za kulevya aina ya bangi kilogramu 2,303,120.58, methamphetamine kilogramu 1,728.8, mirungi kilogramu 18,449.5, skanka kilogramu 4,168.1, heroin kilogramu 433.02, cocaine gramu 854.7, na dawa tiba zenye asili ya kulevya kilogramu 56.78 na mililita 200.

**232. 232.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ekari 4,721 za mashamba ya bangi ziliteketezwa. Idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na ekari 2,389 zilizoteketezwa mwaka 2023. Pia, mbegu za bangi kilogramu 704.7 ziliteketezwa ikilinganishwa na kilogramu 2,500 zilizoteketezwa katika mwaka 2023. Aidha, Serikali ilifanikiwa kukamata kemikali bashirifu zenye ujazo wa lita 22,682.4 pamoja na watuhumiwa 9,543 wanaohusika na dawa hizo.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha malengo ya kudhibiti na kutokomeza dawa za kulevya yanafikiwa kwa kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya; kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya; kutekeleza

afua za kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini; na kuboresha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.

**Uratibu wa Maafa**

**234.** ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuhakikisha kuwa shughuli za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali kutokana na maafa zinatekelezwa kikamilifu. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya kisera kwa kufanya maboresho yanayolenga kuboresha ufanisi katika usimamizi wa maafa nchini. Tayari Serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2004, na kutoa toleo jipya la Sera hiyo la mwaka 2024. Aidha, imeandaa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa pamoja na mikakati ya kupunguza vihatarishi vya maafa kwenye Halmashauri za Kibiti, Monduli, Simanjiro, na Longido. Mipango hiyo, itasadia halmashauri husika kujiandaa na kukabiliana na maafa pindi yanapotokea.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeratibu, kusimamia na kutekeleza operesheni mbalimbali za kukabili maafa yaliyotokea katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo maafa ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa nne la Kariakoo Jijini Dar es Salaam, maafa ya moto uliozuka katika hifadhi ya misitu ya SAO Hill, huko Mafinga Mkoani Iringa pamoja na maafa ya maporomoko ya ardhi yaliyotokea Same Mkoani Kilimanjaro.

**236.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau, imetekeleza programu ya urejeshaji hali kwa kujenga nyumba 109 katika eneo la Waret, Wilaya ya Hanang kutokana na athari za maporomoko ya udongo yaliyotokea mwaka 2023. Nyumba hizo tayari zimekabidhiwa kwa walengwa. Nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika kukabiliana na kurejesha hali kutokana na maafa hayo.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kukabiliana na maafa kwa kuendelea kutumia tafiti na taarifa za kisayansi zinazotoa viashiria vya kutokea kwa maafa katika maeneo mbalimbali, kutoa elimu ya utayari wa kukabiliana na maafa kwa wananchi, kuimarisha

vitengo vya uokoaji pamoja na kamati za uratibu wa maafa katika ngazi za mikoa na wilaya.

**Uratibu wa Masuala ya Lishe**

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** maendeleo ya taifa lolote pamoja na mambo mengine, yanahitaji uwepo wa watu (nguvu kazi) wenye afya njema na lishe bora ili kuwawezesha kufanya kazi kwa bidii na tija. Rasilimaliwatu imara ndio msingi wa kuzalisha kwa tija na kupunguza umaskini. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** tafiti zinaonesha kuwa uwekezaji katika lishe unasaidia kuinua Pato la Taifa kwa asilimia 2 hadi 3 kila mwaka. Aidha, wataalam kutoka Benki ya Dunia wamebainisha kuwa kwa kila Dola moja ya Marekani inayowekezwa katika afua za kimkakati za lishe, faida yake ni Dola 18 za Marekani. Kiwango hicho ni kikubwa katika uwekezaji wa aina yoyote. Kutokana na ukweli huo, nchi yetu imedhamiria kuwekeza kwenye suala la lishe kwa kuhakikisha Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga fedha na kuzitumia kwa ajili ya utekelezaji wa afua za lishe.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026; kufanya tafiti mbalimbali za kisayansi kuhusu masuala ya lishe; kuratibu vikao vya majadiliano na mashirikiano na wadau wa lishe; na kuimarisha mazingira wezeshi ili kuwezesha wadau katika ngazi zote kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa afua za lishe.

**Mazingira**

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuweka msisitizo kuhusu suala la uhifadhi na utunzaji wa mazingira kwa kutoa tathmini ya kina ya hali ya mazingira nchini. Tathmini hiyo imefanyika katika maeneo makuu ikiwemo rasilimali za maji; mifumo ikolojia ya ardhioevu, kilimo, misitu na wanyamapori; na mabadiliko ya tabianchi. Tathmini hiyo imebaini uwepo wa mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na athari zake katika ustawi wa binadamu na mazingira.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari hizo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwemo upandaji na utunzaji wa miti ambapo kwa mwaka 2024/2025 miti 150,159,594 imepandwa katika halmashauri mbalimbali nchini. Vilevile, inaendelea na uratibu wa biashara ya kaboni nchini. Kupitia biashara hiyo jumla ya miradi 70 imesajiliwa ikijumuisha: miradi ya utunzaji wa misitu ya asili na ya kupandwa; utunzaji wa nyanda za malisho; na utunzaji wa taka. Utekelezaji wa miradi hiyo utachangia kuongeza Pato la Taifa kwa wastani wa Dola za Marekani bilioni moja kupitia mauzo ya viwango vya kaboni kutoka kwenye miradi husika.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira ili kukabiliana na changamoto za hifadhi ya mazingira pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

**Uchumi wa Buluu**

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 pamoja na mkakati wake. Lengo ni kuboresha mfumo wa uratibu ili kuwezesha rasilimali na fursa za maji kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa na kuongeza fursa za ajira.

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, mkazo uliwekwa katika ukuaji wa sekta mbalimbali zenye mnasaba na uchumi wa buluu ikiwemo uvuvi, uchukuzi, maji, nishati, madini, maliasili na utalii. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya uvuvi, kukuza uzalishaji wa samaki pamoja na biashara ya mazao ya uvuvi; kufanya maboresho ya miundombinu ya usafirishaji majini na huduma za bandari katika ukanda wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu. Vilevile, kufanya utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; kukuza utalii wa bahari pamoja na kuendeleza uchimbaji wa madini baharini pamoja na kilimo cha baharini, hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi wa Taifa.

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2025/2026, Serikali itaendelea kutekeleza na kuimarisha uratibu wa shughuli za

uchumi wa buluu kwa kuhamasisha: matumizi ya maeneo ya maji; uwekezaji wa kimkakati na fungamanishi katika matumizi ya rasilimali za uchumi wa buluu; uzingatiaji wa masuala mtambuka katika utekelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu; na utafiti katika matumizi ya rasilimali za uchumi wa buluu.

**MUUNGANO**

**247.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuratibu vikao vya kamati ya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Muungano. Katika mwaka 2024/2025 vikao viwili vya kujadili masuala ya Muungano vilifanyika. Kupitia vikao hivyo ilifanyika tathmini ya utekelezaji wa maagizo ya kamati ya pamoja ya kushughulikia masuala ya Muungano.

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo. Programu na miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III); Miradi ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha Bahari ya Hindi-Sipwese Pemba; na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika pamoja na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania. Miradi na programu hizo zimechangia kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuboresha maisha.

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** maadhimisho ya sherehe za Muungano za mwaka huu yatafanyika katika mikoa yote yakiongozwa na viongozi wakuu wa Serikali. Viongozi hao pamoja na masuala mengine, watajumuika na wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo uzinduzi wa miradi ya maendeleo. Nitoe rai kwa Wananchi wote kushiriki katika maadhimisho hayo ili kuendelea kuenzi Muungano wetu.

**250.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2025/2026 Serikali itahakikisha kwamba hoja za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zitashughulikiwa kikamilifu. Vilevile, itaendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuudumisha na kuulinda Muungano wetu.

**USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA Uhusiano ya Kimataifa na Kikanda**

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** uhusiano kati ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na kimataifa umeendelea kuimarika. Nchi yetu imeendelea kuwa na ushawishi mkubwa katika kutekeleza majukumu ya kidiplomasia kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali imeshiriki kikamilifu katika shughuli za kimataifa ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi Tajiri Duniani za Kundi la G20 uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil; Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP 29); Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika New York nchini Marekani; Mkutano wa 27 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola (CHOGM 2024); Mkutano wa 46 wa Kamati ya Urithi wa Dunia ya UNESCO uliofanyika New Delhi, India na Mkutano Mkuu wa 68 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu (IAEA), uliofanyika Vienna, Austria.

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali iliratibu ziara za viongozi wakuu na wawakilishi kutoka mataifa mengine ikiwemo kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati (Mission 300) uliolenga kuendeleza nishati endelevu, uhifadhi na ufanisi. Kupitia mkutano huo yalisainiwa maazimio ya kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika pamoja na kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati.

**254.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, iliratibu Mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Arusha uliojadili masuala mbalimbali ya kimkakati ikiwemo juhudi za kutafuta amani mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali iliratibu na kushiriki Mkutano wa Tano wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kiislam ya Iran uliofanyika Jijini Dar es Salaam uliopelekea kusainiwa kwa Hati za Makubaliano 11; na Mkutano wa Kwanza

wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Comoro uliofanyika tarehe 22 hadi 24 Julai 2024 Jijini Dar es Salaam.

**256.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia majukwaa na mikutano hiyo ya kimataifa, Tanzania iliainisha vipaumbele vyake na kutoa msimamo kuhusu ajenda mbalimbali zilizojadiliwa kama hatua muhimu ya kutatua changamoto zinazoikabili dunia kwa pamoja. Masuala hayo ni pamoja na umuhimu wa nishati safi ya kupikia barani Afrika ambapo kinara wake ni Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 Toleo la mwaka 2024. Sera hiyo imeweka msisitizo wa diplomasia ya uchumi na ushirikiano unaozingatia maslahi ya kiuchumi. Lengo ni kuimarisha ushiriki nchi katika nyanja ya kidiplomasia pamoja na kupata fursa mbalimbali. Fursa hizo ni pamoja na zile za uchumi wa buluu, diaspora, mazingira na mabadiliko ya tabia-nchi, jinsia na vijana. Aidha, Sera hiyo imeweka msingi wa ziada wa kusimamia mila desturi na tamaduni za Tanzania.

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mwanadiplomasia namba moja nchini kwa kutoa kipaumbele cha kuifungua nchi kwenye nyanja za diplomasia ya kiuchumi na kisiasa katika medani za kimataifa.

**259.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kuratibu ziara za kimkakati za viongozi wakuu wa kitaifa nje ya nchi, na ziara za viongozi wakuu wa mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa hapa nchini.

**HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO Habari**

**260.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utangazaji ni muhimu sana katika dunia ya sasa ya kidijitali ambapo upashanaji wa habari umekuwa ni msingi wa ukuaji wa uchumi na kuwa chachu ya maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kutokana

na ukweli huo Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa sekta ya habari inaboreshwa ili kuwaongezea wananchi fursa ya kupata habari kwa kuongeza wigo wa upashanaji wa habari.

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2024/2025 kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania imeongeza usikivu wa matangazo ya redio na televisheni sambamba na ujenzi wa majengo na ufungaji wa mitambo ya kurushia matangazo ya redio katika wilaya nane. Ujenzi huo umefikia asilimia 80 ya utekelezaji. Aidha, uendelezaji wa upanuzi wa mitambo ya kurushia matangazo ya redio kwa wilaya 12 umekamilika na unatumika.

**Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kukuza na kuitangaza Lugha ya Kiswahili. Jitihada hizo ni pamoja na kufungua vituo vya utamaduni katika balozi zetu ughaibuni kwa lengo la kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni, kuingia makubaliano ya kuanzisha somo la Lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya mataifa ya nje, kuandaa machapisho na kushiriki katika makongamano ya kimataifa.

**263.** ***Mheshimiwa Spika***, kama Waheshimiwa Wabunge mtakavyokumbuka, Tanzania ilishiriki katika Kongamano la kwanza la Kimataifa la Kiswahili lililofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Havana nchini Cuba kwa lengo la kupeleka Kiswahili katika nchi zenye watu wengi wenye asili ya Afrika na kuwafahamisha lugha ambayo inatokana na chimbuko lao. Kongamano hilo liliwahusisha takribani washiriki 400 kutoka mataifa mbalimbali.

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya kukuza Lugha ya Kiswahili, Serikali imeendelea kuhakikisha utamaduni wa Taifa letu unaendelea kulindwa na kurithishwa kwa vizazi vyetu. ***"Utamaduni Wetu ni Utu Wetu; Tuuenzi na Kuuendeleza"*** hii ni kaulimbiu iliyotumika wakati wa Tamasha la Tatu la Utamaduni la Kitaifa lililofanyika Mkoani Ruvuma. Lengo kuu la Tamasha hili ilikuwa ni kutoa fursa kwa Watanzania kutambua, kuenzi, kujivunia na kutangaza utajiri wa Urithi wa Utamaduni wa Watanzania uliopo katika Taifa letu.

**265. *Mheshimiwa Spika,*** jitihada za kuendeleza sanaa na utamaduni zinatekelezwa sambamba na kuwaendeleza wasanii, kuimarisha na kusimamia maslahi ya wasanii ili kuhakikisha uwepo wa tija katika kazi zao za sanaa. Moja ya hatua iliyochukuliwa ni kutoa mikopo kwa ajili ya kuendeleza kazi za sanaa ambapo shilingi bilioni 7.96 zimetolewa na Serikali. Fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza kazi za sanaa ikiwemo filamu, ufundi, maonesho, vikundi mbalimbali na muziki.

**266. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza na kuhamasisha kazi za sanaa nchini, Serikali kwa kushirikiana na "*The Hollywood and African Prestigious Awards (HAPAWARDS)"* kutoka Marekani iliratibu utoaji wa Tuzo za *Hollywood and African Prestigious Awards* ambapo tuzo 55 zilitolewa kwa wasanii waliofanya vizuri kitaifa na kimataifa kwenye muziki, filamu na ubunifu wa mavazi. Aidha, tuzo 61 zilitolewa katika matamasha ya sanaa mbalimbali yaliyowahusisha wanafunzi na wanafilamu.

**267. *Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu kuwa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akiweka kipaumbele katika kukuza, na kuendeleza wasanii wa Tanzania kwa kuwapa fursa ya kujifunza, kuongeza ujuzi na kutanua soko la kazi zao ndani na nje ya nchi. Hivi karibuni tumeshuhudia Rais wetu akiliwezesha kundi la wasanii wa filamu nchini kwenda kupata uzoefu kwenye nchi ya Korea Kusini ambayo imepiga hatua kubwa kwenye uzalishaji wa kazi za sanaa hasa filamu na tamthilia.

**268. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kufanya maandalizi ya mashindano ya CHAN yanayotarajiwa kufanyika Agosti, 2025 na mashindano ya AFCON yanayotarajia kufanyika mwaka 2027. Hatua za maandalizi zinazotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya michezo.

**269. *Mheshimiwa Spika***, miradi hiyo ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu imefikia hatua mbalimbali ambapo ukarabati wa miundombinu ya Uwanja wa Benjamini Mkapa umefikia asilimia 75; na ujenzi wa Uwanja wa Arusha umefikia asilimia 26. Pia, mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Dodoma uko katika hatua za awali

baada ya Serikali na mkandarasi kutia saini mkataba Februari 2025.

**270.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, inaendelea kufanya maandalizi ya viwanja vya mazoezi 11 katika maeneo ya Dar es Salaam na Arusha. Kati ya viwanja hivyo uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo na Gymkhana maandalizi yamefikia asilimia 60 na uwanja wa *Leaders Club*, uwanja wa Shule ya Sheria, uwanja wa TIRDO na uwanja wa Farasi maandalizi yanaendelea kwa hatua za awali za utekelezaji.

**271.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuendeleza michezo hapa nchini pamoja na kuviwezesha vilabu vyetu kushiriki katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2024, Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.58 kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wa timu zetu katika mashindano mbalimbali.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo zimewezesha kuimarika kwa ubora wa michezo hususan ligi ya ndani ya mpira wa miguu ambapo ushindani mkubwa umeonekana kwa timu zinazowania ubingwa wa ligi hiyo ikiwemo Yanga vinara wa ligi, Simba, Azam, Singida Big Stars na Tabora United. Vilevile, tumeshuhudia timu ya Simba ikiendelea kuiwakilisha nchi yetu katika michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika hatua ya robo fainali na Timu ya Taifa ikiendelea kuwania nafasi ya kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia kwa Mwaka 2026.

**273.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuitakia heri timu ya Simba katika mchezo wake wa marudiano ili iweze kufanya vema na kufuzu hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo. Kadhalika, ninaitakia kila la heri timu yetu ya Taifa almaarufu Taifa Stars katika michezo yake iliyobaki iweze kushinda na kuwa na nafasi ya kufuzu na kushiriki michuano hiyo.

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa chachu ya mafanikio katika sekta ya michezo. Mheshimiwa Rais wakati wote amekuwa akitoa hamasa kubwa katika sekta ya michezo pamoja

na kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia timu zetu ili ziweze kufanya vizuri. Kutokana na jitihada hizo mafanikio makubwa yamepatikana katika michezo mbalimbali ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu kupitia "***Goli la Mama***".

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa viwanja vya michezo vya Arusha na Dodoma kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027; kuratibu ukuzaji na uendelezaji wa Lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa; na kuratibu Maadhimisho ya Kitaifa na Kikanda ya Siku ya Kiswahili Duniani pamoja na Makongamano ya Kiswahili ya wadau.

**HITIMISHO**

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu ninaomba sasa nitumie fursa hii kutoa msisitizo kwenye maeneo mahsusi kama ifuatavyo:

**Mosi:** Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuhakikisha wananchi na viongozi wanapata muda wa kutosha kujadili na kutoa maoni pamoja na kuzingatia maoni hayo katika rasimu ya Dira.

**Pili:** Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania waendelee kuimarisha juhudi za ukusanyaji mapato ili kuongeza uwezo wa Taifa kujitegemea, pamoja na kubana matumizi katika maeneo yasiyokuwa na tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Tatu:** Nitoe rai kwa wananchi kujitokeza katika zoezi la uandikishaji kwenye Daftari la Mpigakura na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

**Nne:** Niwasihi Viongozi wa Dini, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Mashirika yasiyo ya Serikali na viongozi wote kuendelea kuhamasisha wananchi wote kuzingatia amani na utulivu wakati wa uchaguzi lakini pia kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi ili kuwachagua viongozi.

**277.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimalizie kwa kuwashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu pamoja na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Sina shaka nyote mtakubaliana nami kuwa Mheshimiwa, Rais ni kiongozi shupavu, mwenye maono na mpenda haki. Niwaombe Watanzania wote waendelee kumwombea dua ili awe na afya njema na aweze kutimiza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu.

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nikushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, wasaidizi wako wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote. Hakika ushauri wenu umewezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kipindi cha uhai wa Bunge la 12 ambao umekuwa chachu kubwa ya maendeleo tunayoendelea kuyashuhudia katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2025/2026**

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/2026, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 595,291,624,000** kati ya fedha hizo, **shilingi 183,821,010,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 411,470,614,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo**.**

**280.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 186,793,635,000** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **shilingi 174,960,303,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 11,793,332,000** ni kwa ajili ajili ya matumizi ya maendeleo.

**281.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YAUTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante umetoa hoja na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, hotuba hii imesomwa kwa muda wa masaa mawili. Ni mambo mengi na mambo yamefanywa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusoma vizuri na kutupa imani kuwa nchi yetu iko salama na tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulivyoipongeza Simba, nilikuwa natazama baadhi ya watu wanapiga makofi au hawapigi. Nimewa-*note,* lakini wameniomba nisiwataje, nami sitawataja. Najua ni wazalendo, walipitiwa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria na Wenyeviti wengine watatu wajiandae. Mwenyekiti nenda kwenye mambo muhimu. Maoni na ushauri kwa dakika 10, mambo yote kayamaliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2024/2025

pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118(9) ya Kanuni ya Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: Sehemu ya kwanza, inatoa maelezo ya jumla ya kuonyesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi; Sehemu ya pili, inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati; Sehemu ya tatu, inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Sehemu ya nne, inahusu majumuisho ya maoni ya ushauri wa Kamati; na sehemu ya mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kifungu cha 6 (2)(c) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati kufanya uchambuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi huo Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano ambayo ni: Fungu namba 25, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu; Fungu namba 37, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Fungu namba 27, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Fungu namba 61, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na Fungu namba 91, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umenipa dakika 10 tutaenda kwa uchambuzi katika maeneo ambayo ni mahususi.

Kwanza, tuangalie uchambuzi wa tathmini ya ufafanuzi. Katika matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho, hili naomba kubainisha mambo makuu manne yaliyochambuliwa kama ifuatavyo: -

(i) Makusanyo ya Maduhuli;

(ii) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida;

(iii) Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; na

(iv) Uzingatiaji wa maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili uchambuzi umefanyika katika kukusanya maduhuli kama yalivyowasilishwa, na katika mafungu mbalimbali kama nilivyosema Fungu namba 61; 37; na 27. Pia, katika eneo hili, nitajielekeza katika kutoa pongezi katika Fungu namba 61 na Fungu namba 31 ambayo yamevuka malengo ya makadirio ya makusanyo ya maduhuli katika kipindi cha Julai, 2024 na Februari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ina maoni kuwa kutokuwepo na makusanyo ya maduhuli kwa kupitia Fungu namba 27 ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo haikuonyesha kukusanya kiasi chochote inatafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa na uhalisia na vyanzo vya maduhuli vilivyoainishwa havikuwa na uhakika na sio endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa kila mwaka. Mchanganuo upo katika jedwali namba moja, katika jedwali lililoambatanishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa matumizi ya bajeti ni kama yalivyoelezwa. Naomba nijielekeze moja kwa moja kwenda kwenye eneo la makadirio ya mapato na matumizi katika mafungu haya, ambayo taarifa yangu kuanzia ukurasa wa kwanza naomba iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Nami nijielekeze katika sehemu ya tatu ambayo ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu inaomba kukusanya shilingi 12,100,000,000/= ikilinganisha na shilingi 12,056,000,000/= katika mwaka wa fedha ulioisha kama ambavyo imeainishwa katika jedwali namba tano. Hii ni sawa na ongezeko la 0.3% ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha. Aidha, mchanganuo pia umeambatanishwa katika jedwali namba tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kwamba ongezeko la makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa Fungu 61 inaakisi azma ya Serikali kuongeza wigo wa mapato yake. Aidha, ongezeko hilo litachangiwa na makusanyo yanayotarajiwa kutoka Fungu namba 61 ambayo ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ambayo yanatokana na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 514,828,552,000 ikiwa ni sehemu ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo, shilingi 21,344,130,000 ni mishahara; shilingi 17,563,000,000 ni ruzuku kwa Vyama vya Siasa; shilingi 116,479,938,000 ni matumizi mengineyo na shilingi 377,004,484,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali namba tano lililoko katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa 23% ukilinganisha na mwaka wa fedha ulioisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wake wa bajeti ilikuwa ni shilingi 112,183,433,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba moja kati ya sababu za ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi na ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 377,004,484,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 370,237,705,000 ni fedha za ndani na shilingi 6,766,779,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa takribani shilingi 1,319,946,000 sawa na 16.77% ukilinganisha na bajeti ya mwaka unaoisha. Sababu ya ongezeko hilo imechangiwa na ongezeko la bajeti ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji wa Nyaraka za Serikali Dodoma, kwa fedha za ndani kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali namba sita kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi kwa kutumia fedha za ndani jambo ambalo limekuwa likisisitizwa na Kamati na Bunge lako kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ni maoni na ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(i) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji wa maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato; na

(ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati fedha za maendeleo na matumizi mengineyo ili kuwezesha Wizara hii na taasisi na idara zilizo chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mahususi kuhusu Fungu namba 37 ambalo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu:-

(i) Serikali ihakikishe kwamba, mradi namba 44:29 programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi unatekelezwa kikamilifu ili kuwa na tija Kitaifa;

(ii) Serikali ihakikishe kwamba, ujenzi wa Kiwanda cha Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali unakamilika kwa wakati na mashine za uchapishaji zinasimikwa kwa wakati ili kuwezesha kiwanda kutekeleza majukumu yake; na

(iii) Serikali ihakikishe kwamba, Kiwanda cha Kupiga Chapa kinakamilika na nyaraka zote muhimu za Serikali zinachapwa katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, kukushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu kutupatia nafasi ya kuwasilisha hii taarifa. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa shughuli za Serikali

Bungeni na kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake katika Ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao, naomba niwatambue ambao ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dkt. Jim Yonazi; Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa; Mheshimiwa Jaji Jacobs Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; Ndugu Ramadhani Kailima, Mtendaji Mkuu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na Ndugu Aretas James Lymo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Mahakama, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nchini kwa kukamata dawa za kulevya kiasi cha tani 2,327.98 kwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la 19% ya kiasi cha dawa za kulevya kilichokamatwa mwaka 2023. Hali hii inadhihirisha namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kupambana na uingizaji wa matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Sekretarieti ya Kamati hii kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa niliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1. Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

## 1.2. Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

## 1.3. Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano (5) ambayo ni: -

a) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
b) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu,
c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa,
d) **Fungu 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,
e) **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu manne yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 12,056,000,000.00**, kati ya fedha hizo **Fungu Na. 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya **Sh. 12,000,000,000.00**, **Fungu Na. 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ililenga kukusanya **20,000,000.00** na **Fungu Na. 27** - Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa ililenga kukusanya **36,000,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo: -

(a) **Fungu 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi hadi kufika Mwezi Februari, 2025 imekusanya kiasi cha Sh. **34,400,876.33** sawa na **asilimia 172** ya lengo la Makusanyo. Fungu 61 limevuka

malengo ya makusanyo ya maduhuli kutokana na bakaa ya fedha kutoka Halmashauri kufuatia chaguzi ndogo zilizofanyika

(b) **Fungu 37**-Ofisi ya waziri Mkuu hadi kufikia Mwezi Februari,2025 imekusanya kiasi cha **Shilingi 2,979,053,075.09** sawa na **asilimia 25** ya lengo. Aidha Kamati ilitaarifiwa kwamba mpka kufika mWisho wa mwezi Machi Fungu hili litakuwa limeweza kufikia lengo la ukusanyaji kutokana na malipo yanayotarajiwa kupokelewa kutokana na kazi mbalimbali za uchapaji ikiwemo uchapaji wa nyaraka za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika** naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba hadi ilipofika Aprili 2024 Fungu hili limekusanya jumla **Sh. 16,218,550,475.09** sawa na **asilimia 135.1** ya lengo ambayo ilikua ni **Sh. 12,000,000,000.00**

(c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haijafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufika Februari 2025 hakukua na chama kilichokuwa kimesajiliwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kutotimiza masharti ya kupata usajili. Na kwakuwa chanzo cha maduhuli kwa fungu hili ni usajili wa vyama vya siasa na tozo za uvunjaji wa sheria za gharama za uchaguzi, Hivyo hadi kufikia Februari 2025 hakuna ada ya usajili wa vyama iliyolipwa wala Tozo iliyolipwa na chama chochote cha siasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia **Fungu 61** na **Fungu 37** ambayo yamevuka makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Februari 2025. Aidha Kamati ina maoni kuwa, kutokuwepo na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha kupitia Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa inaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa kila mwaka.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1: MAKUSANYO YA MADUHULI 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu | 12,000,000,000.00 | 16,218,550,475.09 | 135.1 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 20,000,000.00 | 34,400,876.33 | 172 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 36,000,000.00 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **12,056,000,000.00** | **16,252,951,351.42** | **134.8** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

### 2.3.1 Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 33,853,979,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 33,568,723,595.66** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 6,932,937,000.00** ni Mishahara na **Sh. 26,921,042,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, **Sh. 6,504,205,000.000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 1,235,635,000.00** ni fedha za ndani kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa cha Serikali Dodoma na **Sh. 5,358,184,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya uratibu wa Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 33,853,979,000.00** Kati ya fedha hizo, **Sh. 33,568,723,598.00** sawa na **asilimia 99** zilipokelewa kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida na **Sh. 4,134,688,614.00** sawa na **asilimia 63.5 na Sh. 9,581,746,252.98** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo **Sh. 2,899,053,614.00** zilizopokelewa kwa ajili ya kuendeleza programu ya kilimo na Uvuvi na **Sh. 6,681,692,638.98** zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa kiwanda kati ya **Sh. 5,268,570,000.00** zilipokelewa nje ya bajeti kwa ajili ya ununuzi wa mashine na malighafi zitakazotumika katika shughuli za uchapaji.

**2.3.2 Fungu Na. 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 26,191,548,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; kati ya fedha hizo **Sh. 1,687,420,000.00** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 24,504,128,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu ilipokea jumla ya **Sh. 18,283,632,333.36** sawa na **asilimia 70** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Kati ya fedha hizo, **Sh. 17,265,333,333.36** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 1.018,299,000.00** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara.

**2.3.3 Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 28,039,773,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 17,563,000,000.00** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 1,181,418,000.00** ni Mishahara na **Sh. 9,295,355,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 17,563,000,000** ilitengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa. Aidha, **Sh. 940,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilipokea jumla ya **Sh. 20,076,947,904.32** kati ya fedha hizo, **Sh. 11,708,666,664.00** sawa na **asilimia 66** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya Kawaida, Kati ya fedha hizo**, Sh. 7,655,003.512.32** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 713,277,728.00** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara.

Aidha Sh. na **Sh. 940,000,000** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

### 2.3.4 Fungu Na. 91 - Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 17,377,232,000.00**, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; kati ya fedha hizo **Sh. 4,657,413,000.00** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 12,719,819,000.00** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, **Sh. 1,314,506,000.00** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi hiyo ilipokea jumla ya **Sh. 13,747,017,156.69** sawa na **asilimia 79**, Kati ya fedha hizo, **Sh. 11,016,051,326.69** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 2,730,965,830.00** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara.

### 2.3.5 Fungu Na. 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 9,720,901,000.00**, kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; kati ya fedha hizo **Sh. 5,576,181,000.00** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **Sh. 4,144,720,000.00** ni Mishahara. Aidha, **Sh. 167,617,818,000.00** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya **Sh. 5,392,409,539.01** sawa na **asilimia 55** ya fedha iliyoidhinishwa, Kati ya fedha hizo, **Sh. 2,901,339,464.00** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 2,491,070,075.01** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na Jumla ya **Sh. 195,264,401,151** zilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Aidha **Sh. 27,646,583,151** zilipokelewa nje ya ukomo wa bajeti ya maendeleo kwa ajili ya uratibu na na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura. Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na

Uratibu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 na Jedwali Na. 3.

**JEDWALI NA. 2: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 33,853,979,000 | 33,568,723,598 | 70 |
| **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 26,191,548,000 | 18,283,632,333 | 80 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 25,039,773,000 | 20,076,947,904 | 99 |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 17,377,232,000 | 13,747,017,156 | 55 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 9,720,901,000 | 5,392,409,539 | 79 |
| **JUMLA KUU** | 112,183,433,000 | 91,068,730,527.00 | **81** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3: MCHANGANUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 6,504,205,000 | 9,580,746,252 | 147.3 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 940,000,000 | 0 | 0 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 167,617,818,000 | 195,264,401,151 | 116.5 |
| **Fungu 91 –** Mamlaka ya Kudhibiti naKupambana na Dawa za Kulevya | 1,314,506,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **176,376,529,000** | **204,845,147,403.00** | **116** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ni wa kuridhisha, isipokuwa katika **Mradi Na. 5510: Programu ya Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao** ambapo hadi kufikia Februari, 2025 mradi huu ulikua haujapokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa changamoto ya mradi kutopokea fedha inatokana na kutokukamilika kwa taratibu za umiliki wa eneo la mradi huo lililopo eneo la Itega, jijini Dodoma.

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri Mkuu alipowasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 aliidhinishiwa jumla ya **Sh 176,376,529,000** kwa Miradi ya Maendeleo katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika Jedwali Na. 4

**JEDWALI NA. 4: MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2024/2025**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4429** Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi | 4,108,560,000 |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4937** Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali | 1,880,000,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | **NA. 6389** Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma | 940,000,000 |
| **Fungu 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi | **NA. 6583** Program ya kusaidia Uchaguzi Tanzania | 167,617,818,000 |
| **Fungu 91 –** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | **NA. 5510** Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha utengamao | 1,314,506,000 |
| **JUMLA KUU** | | **176,376,529,000** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi mitatu (3) kati ya mitano (5) inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

**2.4.1 Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili lenye jumla ya ghorofa sita (06) wenye thamani ya **shilingi 20,431,828,643.50** ulianza tarehe 05/02/2022 na Ulitarajiwa kukamilika tarehe 25/05/2023.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kuchelewa kwa upatikanaji wa kibali cha ujenzi, kuchelewa kwa michoro ya ujenzi na kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi kulipelekea ujenzi kuchelewa na hivyo kusogezwa mbele hadi tarehe 31/03/2025. Aidha Kamati ilielezwa kuwa uwezekano wa mradi kukamilika tarehe 31/03/2025 ni mdogo kutokana n na uhaba wa malighafi za ujenzi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na hivyo Mkandarasi ameomba kuongezewa miezi sita kukamilisha ujenzi wa mradi.

**2.4.2 Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali, Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa kiwanda hiki kwa awamu ya kwanza unahusisha ujenzi wa jengo kiwanda cha uchapishaji wa nyaraka, jengo la utawala, uzio na kazi za nje ambao ulianza tarehe 25 Machi, 2022 na ulitarajiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na mbili(12) kwa gharama ya **shilingi 2,292,745,444.82**.

**Mheshimiwa Spika,** Awamu ya pili ya mradi ni kuendelea kwa ujenzi wa Jengo la Utawala na kazi za nje(Hard and Soft Scaping) ambao ulianza tarehe 1/03/2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 29 Machi 2024 kwa gharama ya **Sh. 5,015,000,000.00;** Kamati ilielezwa kwamba sababu za kuchelewa kukamilika kwa mradi kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo ucheleweshwaji wa malipo ya Mkandarasi hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika** sambamba na Ujenzi Hadi kufikia Machi 2025 Serikali imeshanunua mashine nane (8) za uchapaji na kukatia karatasi na hadi Kamati inatembelea mradi huo tarahe 17 Machi 2025 ilikuta tayari Mashine moja ya kukatia karatasi kuwa

imeshasimikwa na Serikali iliahidi kwamba hadi kufika Aprili 2025 mashine saba (7) zilizobaki zitakuwa zimekamilika kusimikwa na itakuwa ni baada ya kukamilika kwa mfumo wa umeme ambao unaendelea kuwekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kujengwa kwa kiwanda hiki kutawezesha nyaraka za Serikali za siri na za wazi kuchapishwa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ubora na kwa wakati. Jambo hili litachochea kuongezeka kwa usiri na ubora wa nyaraka za Serikali. Aidha, pindi kiwanda kitakapoanza kazi, kitaongeza maduhuli ya Serikali kupitia Idara ya Mpiga chapa Mkuu wa Serikali kutoka wastani **Sh. 2,000,000** kwa mwaka hadi kufikia **Sh. 2,000,000,000** kwa mwaka.

### 2.4.3 Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Utengamao, Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mkataba wa mradi wa Ujenzi Kituo cha Taifa cha Utengamao unatarajiwa kugharimu **Shilingi 5,666,515,760.00** ambao unatarajiwa kukamilika 15 Septemba 2025.

**Mheshimiwa Spika** hadi kamati inatembelea mradi huu mnamo yatehe 17 machi 2025 tayari Mkandarasi na Mshauri elekezi walikuwa wameshakabidiwa mradi na kazi za awali ikiwemo kusafisha eneo la mradi zilikua zimekwisha kuanza**.**

**Mheshimiwa Spika** Kujengwa kwa Kituo hiki cha Utengamao kutapunguza matumizi ya Serikali katika kutibu waraibu wa dawa za kulevya kwakuwa kila mwaka serikali inatumia **Shilingi 517,000,000,000.00** kwa ajili ya ununuzi wa dawa za methadone zinazotumiwa na waraibu wa dawa za kulevya.Hivyo ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inapeleka fedha za mradi kwa wakati ili kuwezesha Kituo hiki kuanza kutoa huduma kwa wananchi na pia kupunguza gharama kwa serikali kuhudumia waraibu.

**2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**3.1 Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 12,100,000,000** ikilinganishwa na **Sh. 12,056,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali Na. 5. Hii ni na sawa na ongezeko la **asilimia 0.3** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

**JEDWALI NA. 5: MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 |
|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 12,000,000,000 | 12,000,000,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 36,000,000 | 0 |
| **Fungu 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi | 20,000,000 | 100,000,000 |
| **JUMLA KUU** | **12,056,000,000** | **12,100,000,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kwamba, ongezeko la makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Fungu 61 inaakisi azma ya Serikali kuongeza wigo wa mapato yake. Aidha, Ongezeko hilo litachangiwa na makusanyo yanayotarajiwa kutoka Fungu 61- Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ambayo yatatokana na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 514,828,552,000.00** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 21,344,130,000** ni mishahara, **Sh. 17,563,000,000** ni ruzuku kwa vyama vya Siasa na **Sh. 116,479,938,000** ni matumizi mengineyo, na **Sh. 377,004,484,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 5

**JEDWALI NA. 5 – Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 8,369,915,000 | 34,594,068,000 | 0 | 42,963,983,000 |
| **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 1,630,183,000 | 28,116,731,000 | 0 | 29,746,914,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 1,321,730,000 | 30,015,739,000 | 17,563,000,000 | 48,900,469,000 |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 5,073,567,000 | 18,037,814,000 | 0 | 23,111,381,000 |
| **Fungu 61** – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi | 4,948,735,000 | 5,715,586,000 | 0 | 10,664,321,000 |
| **JUMLA KUU** | **21,344,130,000** | **116,479,938,000** | **17,563,000,000** | **145,787,068,000** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 23** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 112,183,433,000.00**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 377,004,484,000**kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 370,237,705,000.00** ni fedha za ndani, na **Sh. 6,766,779,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Sh. 1,319,946,000** sawa na **asilimia 16.77** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya ongezeko hilo imechangiwa na ongezeko la bajeti ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali Dodoma kwa fedha za ndani, Kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6.**

**JEDWALI NA. 6 – Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026**

**JEDWALI NA. 6: MCHANGAUO WA BAJETI YA MAENDELEO 2025/2026**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu** | **NA. 6575** Mradi wa Kuimarisha uwezo wa nchi wa kujiandaa na maafa | | 200,600,000. |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4937** Ujenzi wa Kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali Dodoma | 741,381,000 | 0 |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4429** Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi | | 6,566,179,000. |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | **NA. 6389** Ujenzi wa jingo la Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa Zanzibar | 564,000,000 | |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | **NA. 6583** Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania | 367,617,818,000 | 0 |
| **Fungu 91 –** Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za kulevya | **NA. 6583** Ujenzi wa Kituo cha taifa cha Utengamao | 1,314,506,000 | |
| **Jumla Ndogo** | | **370,237,705,000** | **6,766,779,000** |
| **JUMLA KUU** | | **377,004,484,000** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani jambo ambalo limekua likisisitizwa na Kamati na Bunge lako kwa ujumla.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

i) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na idara zilizo chini yake zinatekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

### 4.2 Ushauri Mahsusi Fungu kwa Fungu

#### 4.2.1 Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

i) Serikali ihakikishe kwamba, fedha za Mradi Na. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi unatekelezwa kikamilifu ili kuwa na Tija kwa Taifa

ii) Serikali ihakikishe kwamba Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali unakamilika kwa wakati na Mashine za uchapaji zinasimikwa kwa wakati ili kuwezesha Kiwanda kutekeleza majukumu yake.

iii) Serikali ihakikishe kwamba Kiwanda cha kupiga Chapa kinakamilika na nyaraka zote muhimu za Serikali zinachapwa na kiwanda hiko.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Aziza SleyumAlly, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
22. Mhe.Dkt. Oscar Ishengoma kikoyo, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi Mkubwa. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majumu yake katika ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. William Vangingembe Lukuvi, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

2. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi, Mhe. Jaji Francis S. Mutungi - Msajili wa vyama vya Siasa, Mhe. Jaji Jacobs Mwambegele – Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Pamoja na Mkurugenzi Ndg.Ramadhani Kailima ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Ndg. Aretas James Lyimo – Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, na kwa namna ya kipekee Kamati inaipongeza Wizara kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya nchini kwa kukamata dawa za kulevya kiasi cha **tani 2327.98** kwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la **Asilimia 19** ya kiasi cha dawa za kulevya kilichokamatwa mwaka 2023, hali hii inadhihirisha namna ambavyo Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. **Dkt. Samia Suluhu Hassan** Rais Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imedhamiria kupambana na uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Sekretarieti ya Kamati hii kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
9 Aprili, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, dakika 10.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge, Fungu namba 42 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Mmakadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Bunge, Fungu namba 42 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 62 na Ibara ya 63 (2) na (3) imeainisha majukumu ya Ofisi ya Bunge ambayo ni kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza masharti hayo ya kikatiba, Mfuko wa Bunge ulianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, sura namba 115.

Kifungu hiki pia kinatoa maelekezo ya namna mfuko huo utakavyosimamiwa na kuendeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji ya bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ofisi ya Bunge inatekeleza bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti sura namba 439; Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma sura namba 348; Sheria ya Manunuzi sura namba 410; Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/2025; Mpango Mkakati wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026; pamoja na Mpango wa Muda wa Kati wa Mwaka 2023/2024 – 2024/2025. Utekelezaji wa bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika kulingana na mahitaji halisi kwa lengo la kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kiasi cha shilingi 181,106,233,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 23,870,762,000 ni mishahara, shilingi 148,253,651,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi 9,680,110,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi 8,976,470,000 ni fedha za ndani na shilingi 704,340,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025, Mfuko wa Bunge ulipokea jumla ya shilingi 126,433,726,143.70 sawa na 69.81% ya bajeti nzima. Kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi 15,786,018,968, matumizi mengineyo ni shilingi 107,856,778,272 na shilingi 2,790,928,907.70 zilipelekwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo zilizopokelewa, shilingi 2,156,188,903.70 ni fedha za ndani na shilingi 634,740,000 ni fedha za nje. Jedwali namba moja lililopo katika taarifa ya Kamati linaonesha mchanganuo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya fedha za maduhuli kiasi cha shilingi 147,939,000. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025 kiasi cha shilingi milioni 86,717,520,000 zilikuwa zimekusanywa sawa na 58.6% ya bajeti. Fedha zilizokusanywa zimetokana na kodi ya pango katika jengo la utawala *(Annex)* Dodoma pamoja na kukodisha kumbi za mikutano katika Ofisi ya

Bunge Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar. Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti mwaka 2024/2025 ni kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge, Fungu Namba 42 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yamezingatia masuala yafuatayo: -

(i) Dira na Dhima ya Ofisi ya Bunge;

(ii) Majukumu ya Idara na Vitengo;

(iii) Mahitaji ya Shughuli za Bunge ikiwa ni pamoja na vikao vya Bunge na Kamati zake;

(iv) Maelekezo yaliyotolewa katika mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(v) Mpango wa maendeleo wa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni sehemu ya rasilimali ya kutekeleza mpango mkakati wa ofisi wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 unaotekelezeka kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Mfuko wa Bunge umepewa ukomo wa shilingi 186,753,635,000 sawa na ongezeko la 2.7% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/2025 ya shilingi 181,805,233,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 25,632,628,000 ni mishahara; shilingi 149,327,675,000 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi 11,763,332,000, ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za maendeleo zilizotengwa, shilingi 11,385,882,000 ni fedha za ndani na shilingi 407,450,000 ni fedha za nje. Mchanganuo wa mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama unavyoonekana katika jedwali namba mbili kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maduhuli, Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 147,936,000 kutokana na ukodishaji wa kumbi za mikutano, kodi za pango katika jengo la mgahawa wa Dodoma na sehemu ya jengo la utawala *(Annex)*. Vipaumbele vya bajeti vya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama vinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati. Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuhamisha taasisi za umma ambazo bado ziko kwenye eneo lililotwaliwa na Bunge. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kwa ajili ya kuhamisha taasisi za umma zilizopisha maeneo yaliyotwaliwa na Bunge ili Ofisi ya Bunge ianze mchakato wa uendeshaji wa maeneo hayo. Hatua hii itawezesha taasisi hizo kuhamia maeneo mengine ili kupisha eneo lililotwaliwa na Bunge kwa ajili ya kuendeleza Ofisi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani; pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba majina yao yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu

yake ipasavyo. Baada ya maelekezo haya, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato ya matumizi ya mfuko wa Bunge Fungu Namba 42 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya shilingili bilioni 186,753,635.000 ambapo kiasi cha bilioni 25,632,628.000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 149,327,675,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 11,793,332,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

**TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/26.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 62 na Ibara ya 63 (2) na (3) imeainisha majukumu ya Ofisi ya Bunge ambayo ni kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake. Katika kutekeleza masharti hayo ya Kikatiba, Mfuko wa Bunge ulianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge Sura ya 115. Kifungu hichi pia kinatoa maelekezo ya namna Mfuko huo utakavyosimamiwa na kuendeshwa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele cha (c) cha Sheria ya Bajeti, Kamati ilikutana na Mheshimiwa

William Lukuvi (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Ndugu, Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge, ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Februari, 2025, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango na Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348, Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura ya 410, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25, Mpango Mkakati wa mwaka 2021/22-2025/26 pamoja na Mpango wa Muda wa Kati wa mwaka 2023/24 – 2024/25. Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika kulingana na mahitaji halisi kwa lengo la kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao wa kikatiba.

### 2.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge ya mwaka 2024/25 hadi Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 181,106,233,000.** Kati ya Fedha hizo **shilingi 23,870,772,000** ni Mishahara, **shilingi 148,253,651,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 9,680,810,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, **shilingi 8,976,470,000** ni fedha za ndani na **shilingi 704,340,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025 Mfuko wa Bunge ulipokea jumla ya **shilingi 126,433,726,143.70** sawa na

**asilimia 69.81** ya bajeti nzima. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **shilingi 15,786,018,968,** matumizi mengineyo ni **shilingi 107,856,778,272 na shilingi 2,790,928,903.70** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa **shilingi 2,156,188,903.70 ni fedha za ndani na** shilingi **634,740,000** ni fedha za nje.

**Jedwali Na. 1** linaonyesha mchanganuo wa fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 28 Februari 2025.

**Jedwali Na. 1. Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge Hadi Februari 2025**

| MAELEZO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ZILIZOPOKELEWA | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 23,870,772,000 | 15,786,018,968 | 66.13 |
| Matumizi Mengineyo | 148,253,651,000 | 107,856,778,272 | 72.75 |
| Maendeleo | 9,680,810,000 | 2,677,478,903.70 | 28.83 |
| **JUMLA** | **181,805,233,000** | **126,433,726,143.70** | **69.81** |

**Chanzo:** *Randama ya Mfuko wa Bunge*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kupitia hazina kwa kutoa fedha kwa wakati na kulingana na mahitaji ya Mfuko wa Bunge ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

## 2.2. Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya fedha za maduhuli kiasi cha **shilingi 147,966,000**. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2025 kiasi cha

**shilingi 86,717,520** kilikuwa kimekusanywa sawa na **asilimia 58.6** ya bajeti. Fedha zilizokusanywa zimetokana na kodi ya pango katika Jengo la Utawala *Annex* Dodoma pamoja na kukodisha kumbi za Mikutano katika Ofisi ya Bunge Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

**2.3. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/25**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Bunge umefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu Mikutano ya Bunge Mitatu (3) na Kamati zake;

ii. Kulipa stahili za Wabunge na watumishi pamoja na kushiriki Mikutano ya vyama vya Kibunge ndani na nje ya nchi ambayo Bunge ni mwanachama;

iii. Kuwezesha Ushiriki wa michezo kwa Wabunge na watumishi;

iv. Kuajiri Watumishi wapya 8;

v. Kutekeleza pendekezo la Tume ya Utumishi wa Bunge na Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi, ambapo Ofisi imefanikiwa kununua Magari 16 kwa ajili ya kuhudumia Viongozi na Watumishi wa Bunge;

vi. Kuboresha Muundo wa Ofisi kwa kuanzisha Vitengo vitatu (3) vipya ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza shughuli za Bunge;

vii. Kukamilisha shughuli za ujenzi wa nyumba mbili (2) za Viongozi;

viii. Kusimika mitambo ya ulinzi na usalama katika maeneo ya Ofisi ya Bunge Dodoma;

ix. Ukarabati wa Majengo ya Bunge Dodoma, Dar es salaam na Zanzibar; na

x. Kukamilisha malipo ya mwisho ya Mfumo wa kupooza hewa kwenye ukumbi wa Bunge.

## 3.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 yamezingatia masuala yafuatayo:-

i. Dira na Dhima ya Ofisi ya Bunge;

ii. Majukumu ya Idara na Vitengo;

iii. Mahitaji ya Shughuli za Bunge ikiwa ni pamoja na Vikao vya Bunge na Kamati zake;

iv. Maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25; na

v. Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2025/26 ni sehemu ya rasilimali ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Ofisi wa Mwaka 2021/22 - 2025/26 unaotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja mmoja.

### 3.1. Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Mfuko wa Bunge umepewa ukomo wa **shilingi 186,753,635,000** sawa na ongezeko la **asilimia 2.7** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/25 ya **shilingi 181,805,233,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 25,632,628,000** ni mishahara, **shilingi 149,327,675,000** ni fedha za matumizi mengineyo na **shilingi 11,793,332,000 ni** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zilizotengwa **shilingi 11,385,882,000** ni fedha za ndani na **shilingi 407,450,000** ni fedha za nje. Mchanganuo wa Mapendekezo ya Bajeti kwa mwaka fedha 2025/26 ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

*Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na 2025/26*

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2024/25 | MAPENDEKEZO YA BAJETI YA MWAKA 2025/26 | ONGEZOKO /PUNGUZO |
|---|---|---|---|
| A: Matumizi ya Kawaida | 172,124,423,000 | 174,960,303,000 | 2,835,880,000 |
| Mishahara | 23,870,772,000 | 25,632,628,000 | 1,761,856,000 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 148,253,651,000 | 149,327,675,000 | 1,074,024,000 |
| B: Maendeleo | 9,680,810,000 | 11,793,332,000 | 2,112,522,000 |
| Fedha za Ndani | 8,976,470,000 | 11,385,882,000 | 2,409,412,000 |
| Fedha za Nje | 704,340,000 | 407,450,000 | 296,890,000 |
| **JUMLA KUU A+B** | **181,805,233,000** | **186,753,635,000** | **4,948,402,000** |

**Chanzo:** *Randama Mfuko wa Bunge*

**3.2. Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maduhuli, Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **shilingi 147,966,000** kutokana na ukodishaji wa kumbi za mikutano, kodi ya pango katika Jengo la Mgahawa Dodoma na sehemu ya Jengo la Utawala *Annex*.

**4.0. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kugharamia Mikutano mitatu (3) ya Bunge na Mikutano miwili (2) ya Kamati;

ii. Kugharamia Posho ya Jimbo na Usafiri wa Wabunge na stahiki nyingine kwa Wabunge na Watumishi;

iii. Kulipa Mishahara kwa Watumishi na Wabunge, Ajira mpya 28, pamoja na kupanda madaraja kwa Watumishi 58; kubadilishwa kada kwa Watumishi wanne (4);

iv. Kugharamia matibabu ya Wabunge na Watumishi kwa utaratibu wa Bima ya Afya;

v. Kugharamia mahitaji ya Bunge Jipya la 13 hususan mafunzo elekezi ya uendeshaji wa Shughuli za Bunge kwa Wabunge wote pamoja na Watumishi;

vi. Kuhudumia Viongozi Wastaafu wa Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya kustaafu ya Viongozi wa Kisiasa;

vii. Ununuzi wa magari manne (4) kwa Viongozi wa Bunge pamoja na gari moja (1) la Wagonjwa la Kituo cha Afya cha Bunge;

viii. Ununuzi wa Samani za Ofisi kwa ajili ya Viongozi na Watumishi;

ix. Ununuzi wa vitendea kazi vya Ofisi;

x. Mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi kwa Watumishi pamoja na kuwawezesha kushiriki makongamano ya kitaaluma;

xi. Kutenga bajeti kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Kiongozi wa walio wachache Bungeni;

xii. Ushiriki katika mikutano ya kimataifa, hususan mikutano ya vyama vya Kibunge ambavyo Bunge letu ni mwanachama;

xiii. Marekebisho ya Miundombinu na Mifumo ya TEHAMA katika Majengo ya Ofisi;

xiv. Ununuzi wa mtambo wa simu kwa Ofisi ya Dar es Salaam, pamoja na ununuzi wa server kwa ajili ya kuhifadhi picha za video (media storage) za vikao vya Bunge;

xiv. Kugharamia urushaji wa matangazo ya Bunge mubashara kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) pamoja na Bunge la Vijana na mikutano ya Elimu kwa Umma;

xv. Kugharamia gharama nyingine za uendeshaji wa Ofisi;

xvi. Kufanya ukarabati wa Ukumbi wa Bunge, Ukumbi wa Msekwa na Ofisi ya Dar es Salaam;

xvii. Kuboresha Mfumo wa Sauti (DCN) katika Ukumbi wa Bunge;

xviii. Kusimika Mitambo ya Usalama katika maeneo ya Bunge Ofisi ya Dodoma na Dar es Salaam; na

xix. Ujenzi wa uzio kuzunguka eneo jipya la Ofisi ya Bunge ya Dodoma.

## 5.0. MAONI YA KAMATI

### 5.1. Serikali Kutenga Fedha kwa ajili kuhamisha Taasisi za Umma ambazo bado ziko kwenye eneo lililotwaliwa na Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha kwa ajili ya kuhamisha Taasisi za Umma zilizopisha maeneo yaliyotwaliwa na Bunge ili Ofisi ya Bunge ianze mchakato wa uendelezaji wa maeneo hayo. Hatua hii itawezesha Taasisi hizo kuhamia maeneo mengine ili kupisha eneo lililotwaliwa kwa ajili ya kuendelezwa na Ofisi ya Bunge.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Akson, (Mb) Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani pamoja na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) Naibu Spika kwa miongozo yenu katika kuendesha shughuli za

Bunge. Aidha nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha, Mhe. William Lukuvi (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, na Uratibu na Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati Kamati inajadili bajeti ya Mfuko wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 10.Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 11.Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12.Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13.Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 14.Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 15.Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb | Mjumbe |
| 16.Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 17.Mhe. Zaytun Seif Swai,Mb | Mjumbe |
| 18.Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 19.Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 20.Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 21.Mhe. Yahya Ally Mhata, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Baraka I. Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha

2025/26 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya **shilingi 186,753,635,000** ambapo kiasi cha **shilingi 25,632,628,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **shilingi 149,327,675,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 11,793,332,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza, (Mb)
*MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI*
09 Aprili, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Namwita sasa Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa mpaka tutakapomaliza shughuli yetu. Mheshimiwa dakika 10. *(Makofi)*

**MHE. JACQULINE K. ANDREA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI naomba kuwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi huo wa kina, naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makuu matatu na naomba mambo ambayo nitakayoyaruka yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *Hansard*. Mambo hayo ni kama yafuatavyo:-

(a) Utekelezaji wa mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(b) Makadirio ya matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(c) Maoni ya ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, mambo mbalimbali yalizingatiwa ikiwemo uhusiano wa makadirio hayo na mpango wa tatu wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025. Aidha, vipaumbele vya mpango na bajeti katika makadirio ya mwaka wa fedha 2025/2026 vimezingatia miongozo iliyowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizoombwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Mwaka wa Fedha 2025/2026, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania – Fungu 92 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 8,280,832,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2,787,579,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 5,493,253,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 20,867,978,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ya fedha hizo, shilingi 5,280,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 15,587,978,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa

utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – Fungu 92, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

a) Mwenendo mdogo wa utoaji wa fedha za ndani za maendeleo zilizotengwa mwaka 2024/2025. Kutokana na kutolewa kwa kiwango kidogo cha fedha za ndani za maendeleo, kiwango cha 50% tu, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji wa fedha zote za ndani zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

b) Utegemezi mkubwa wa fedha za nje za maendeleo kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo kwa utegemezi mkubwa wa fedha za nje kutoka kwa wafadhili katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

a) Iongeze kiwango cha fedha za ndani za maendeleo zinazotengwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI *(Aids Trust Fund)* ili kuhakikisha afua za 16 UKIMWI zinatekelezwa bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi;

b) Itekeleze kikamilifu mpango wa uendelevu wa mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini *(HIV Response Sustainability Roadmap)* ili kupata rasilimali endelevu za ndani katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo usioridhisha wa huduma ya upimaji wa Virusi vya UKIMWI (VVU). Kutokana na mwenendo usioridhisha wa huduma ya upimaji wa Virusi vya UKIMWI (VVU), Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupima ili kujua hali zao za maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na dawa kinga za maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Imebainika kuwa Serikali ina utaratibu wa kuagiza dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI na dawa kinga za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kutoka nje ya nchi, utaratibu huo unasababisha nchi kutumia gharama kubwa kuagiza bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ili kupunguza gharama na kuhakikisha kunawepo na uhakika wa upatikanaji wa dawa, Kamati inaishauri Serikali iwekeze kwenye viwanda vya ndani kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya kuzalisha dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI na dawa kinga za maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, uundaji na utekelezaji wa mpango mkakati wa kudhibiti UKIMWI. Ili kufikia malengo ya kidunia ya kutokomeza UKIMWI, ifikapo mwaka 2030, zinahitajika jitihada madhubuti kwa kila sekta na taasisi za umma nchini kushiriki mapambano dhidi ya UKIMWI. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba kila sekta na taasisi za umma zinaunda na kutekeleza mpango mkakati wa kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa afua za virusi vya UKIMWI gerezani. Afua za Virusi vya UKIMWI zinatekelezwa gerezani kwa lengo la kutoa huduma kwa WAVIU waliopo gerezani na kuzuia maambukizi ya VVU gerezani. Katika kuboresha na kuimarisha mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI gerezani, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuna upatikanaji wa uhakika wa dawa gerezani kwa ajili ya kutibu wafungwa na mahabusu wanapopatwa na maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuendesha Bunge lake kwa umahiri mkubwa, vile vile napenda kukushukuru kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vile vile Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa

Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza Uongozi wake wa shughuli za Serikali Bungeni na kuwasilisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge na Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga Mbunge kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu yao ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dkt. Jim James Yonazi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Catherine Joachim na watendaji wote wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2025/2026 naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU (TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA –*TACAIDS*) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya majukumu ya Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI ni kushughulikia Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Jukumu hilo lilitekelezwa tarehe 24 Machi, 2025, ambapo Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi huo wa kina, naomba kutoa Taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makuu matatu (3) ambayo ni yafuatayo: -

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(b) Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*;* na

(c) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*- **Fungu 92**.

**SEHEMU YA PILI**

**UCHAMBUZI WA MASUALA YA KIBAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi kwa ajili ya kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kushauri inavyofaa kuhusu makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Uchambuzi wa wasilisho la Serikali ulijikita katika mambo makuu matatu (3) ambayo ni: -

(a) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(c) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ulizingatia mambo makuu yafuatayo: -

(a) Uzingatiaji na Utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu; **Fungu 92** - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(b) Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2025; na

(c) Utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango na Bajeti vilivyowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha Bajeti husika.

**Uchambuzi kuhusu Uzingatiaji na Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha dhana ya usimamizi wa Serikali inatekelezwa kikamilifu, Kamati ilijadili na kuchambua uzingatiaji na utekelezaji wa ushauri ilioutoa kwa Serikali katika Bunge wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa jumla ya maeneo tisa (9) yalitolewa ushauri ili kuboresha utendaji wa Serikali. Kati ya maeneo hayo yaliyotolewa ushauri, maeneo matano (5) yametekelezwa kikamilifu na maeneo manne (4) yapo katika hatua ya utekelezaji. Kwa muktadha huo nguvu zaidi inahitajika katika maeneo ambayo utekelezaji wake unaendelea ili yakamilishwe kwa wakati.

**Uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa Ziara ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge inaipa mamlaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

iliyotengewa Fedha kwa mwaka 2024/2025. Kamati ilifanya ziara kati ya tarehe 12 hadi 18 Machi, 2025 kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa afua za Virusi vya UKIMWI na UKIMWI katika mkoa wa Shinyanga na Singida.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mkoa wa Shinyanga, Kamati ilitembelea mgodi wa Bulyanhulu ili kupata taarifa kuhusu utekelezaji wa afua za Virusi vya UKIMWI na UKIMWI katika mgodi huo. Aidha, Katika mkoa wa Singida, gereza la Mkoa huo lilitembelewa kwa ajili ya kupata taarifa na kukagua utekelezaji wa afua za Virusi vya UKIMWI na UKIMWI katika gereza hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini uwepo wa mafanikio na changamoto kadhaa na hivyo kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na changamoto zilizobainika. Mafanikio yaliyobainika ni kama ifuatavyo; -

i) Upatikanaji wa uhakika wa huduma za upimaji wa Virusi vya UKIMWI na utoaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs) kwa WAVIU katika gereza na mahabusu. Mfano, katika Gereza Singida kuna WAVIU 14 wanaotumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI; na

ii) Utoaji wa elimu kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI ndani ya mgodi na gerezani.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania, imebainika kuwepo kwa changamoto kadhaa katika maeneo hayo. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

i) Uhaba wa dawa za kutibu wafungwa na mahabusu; na

ii) Uwepo wa unyanyapaa miongoni mwa watumishi wa jeshi la magereza ambapo husababisha mwitikio mdogo wa watumishi kupima afya zao.

**Uchambuzi kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa Fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha ilichambuliwa ambapo katika mwaka wa fedha 2024/ 2025 Tume iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 17,808,981,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 4,542,483,000.00** ni Matumizi ya Kawaida yenye kujumuisha Mishahara **shilingi bilioni 1,817,358,000.00** na **shilingi bilioni 2,725,125,000.00** za Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo ni **shilingi bilioni 13,266,498,000.00** ambapo kati yake fedha za ndani ni **shilingi bilioni 1,880,000,000.00** na fedha za nje ni **shilingi billioni 11,386,498,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kwamba, hadi kufika mwezi Februari, 2025, Tume ilipokea kiasi cha **shilingi bilioni 12,912,102,293.43** sawa na asilimia 73 ya Bajeti yake yote. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa fedha za Matumizi ya Kawaida ni **shilingi bilioni 2,382,976,777.00** sawa na asilimia 52.46 ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida fedha zilizotolewa kwa ajili ya Mishahara ni **shilingi milioni 997,151,027.00** sawa na asilimia 54.87 ya fedha zote za Mishahara zilizoidhinishwa. Fedha za Matumizi Mengineyo zimetolewa **shilingi bilioni 1,385,825,750.00** sawa na asilimia 50.85 ya fedha zote za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Fedha za Maendeleo, imebainika kuwa hadi mwezi Februari 2025, kiasi cha **shilingi bilioni 10,529,125,516.43** kimepokelewa sawa na asilimia 79.37 ya fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa. Fedha hizi za Maendeleo zilizotolewa zinajumuisha Fedha za Ndani **shilingi milioni 940,000,000.00** sawa na asilimia 50 ya Fedha za Ndani zilizoidhinishwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)* pamoja na Fedha za Nje **shilingi bilioni 9,589,125,516.43** sawa na asilimia 84.21 ya Fedha zote za Nje za Maendeleo zilizoidhinishwa.

**KIELELEZO NA 1: Mchanganuo wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizopokelewa kuanzia Julai, 2024 hadi Februari, 2025**

| MAELEZO | ZILIZOIDHINISHWA | ZILIZOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,817,358,000.00 | 997,151,027.00 | **54.87** |
| Matumizi Mengineyo | 2,725,125,000.00 | 1,385,825,750.00 | **50.85** |
| **Jumla (Fedha za Matumizi ya Kawaida)** | **4,542,483,000.00** | **2,382,976,777.00** | **52.46** |
| Maendeleo Ndani | 1,880,000,000.00 | 940,000,000.00 | **50.00** |
| Maendeleo Nje | 11,386,498,000.00 | 9,589,125,516.43 | **84.21** |
| **Jumla (Fedha za Maendeleo)** | **13,266,498,000.00** | **10,529,125,516.43** | **79.37** |
| **Jumla Kuu** | **17,808,981,000.00** | **12,912,102,293,43** | **73.00** |

***Chanzo: Taarifa ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha ambao ni wastani wa asilimia 73 ni wa kuridhisha. Hata hivyo kwa muda mchache uliobaki kumaliza Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inasisitiza kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa vipaumbele mbalimbali vilivyowekwa kwa kipindi husika.

**UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**


**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, mambo mbalimbali yalizingatiwa ikiwemo uhusiano wa makadirio hayo na Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2021/22 – 2025/26, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025.

Aidha, vipaumbele vya mpango na bajeti katika makadirio ya mwaka 2025/2026 vimezingatia miongozo iliyowekwa na Serikali.

**Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania – Fungu 92 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 8,280,832,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 2,787,579,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi bilioni 5,493,253,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 20,867,978,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 5,280,000,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 15,587,978,000.00** ni Fedha za nje.

**KIELELEZO NA 2: Fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa Mwaka 2024/2025**




***Chanzo; Randama ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kwamba bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania imeongezeka kwa **asilimia 64** ambapo ongezeko hilo linajumuisha fedha za matumizi ya kawaida na fedha za miradi ya maendeleo.

Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida ongezeko ni la **shilingi bilioni 3,738,349,000.00** sawa na asilimia 82 na kwa fedha za miradi ya maendeleo ongezeko ni la **shilingi bilioni 7,601,480,000.00** sawa na asilimia 57. Lifuatalo ni jedwali linaloonesha ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 na fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa kipindi cha mwaka 2025/2026.

**KIELELEZO NA 3: Ulinganisho wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025 na 2025/2026**

| MAELEZO | 2024/2025 | 2025/2026 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI MENGINEYO (OC)** | 2,725,125,000.00 | 5,493,253,000.00 | +2,768,128,000.00 | **101** |
| **MISHAHARA** | 1,817,358,000.00 | 2,787,579,000.00 | +970,221,000.00 | **53** |
| **JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA** | **4,542,483,000.00** | **8,280,832,000.00** | +3,738,349,000.00 | **82** |
| **MAENDELEO NDANI** | 1,880,000,000.00 | 5,280,000,000.00 | +3,400,000,000.00 | **180** |
| **MAENDELEO NJE** | 11,386,498,000.00 | 15,587,978,000.00 | +4,201,480,000.00 | **+37** |
| **JUMLA YA FEDHA ZA MAENDELEO** | **13,266,498,000.00** | **20,867,978,000.00** | +7,601,480,000.00 | **+57** |
| **JUMLA** | **17,808,981,000.00** | **29,148,810.000.00** | **+11,339,829,000.00** | **+64** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania 2024/2025 na 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla ongezeko la bajeti ya Tume kwa mwaka 2025/2026 linaenda kuongeza nguvu katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Tume kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango na bajeti kwa mwaka 2025/2026. Ongezeko la fedha za matumizi ya kawaida litasaidia kuimarisha utekelezaji wa shughuli za kila siku za Tume ikiwemo kulipa mishahara watumishi na kugharamia matumizi mengineyo ya Tume.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Fedha za Maendeleo za ndani kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(Aids Trust Fund – ATF)* zimeongezeka hadi kufikia **shilingi bilioni 5,280,000,000.00** zitakazotumika katika maeneo makuu matatu ambapo asilimia 60 ni kwa ajili ya kutekeleza afua za kinga kwenye jamii hususani udhibiti wa maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) ikijumuisha utoaji wa elimu ya VVU na UKIMWI; asilimia 30 zimeelekezwa kuwezesha uendeshaji wa mfuko ikiwemo kugharamia vikao vya kila robo mwaka vya bodi ya mfuko; na asilimia 10 ni kwa ajili ya kukabiliana na madhara ya UKIMWI *(Impact mitigation)* ikihusisha kuwawezesha WAVIU kiuchumi *(Economic Empowerment)*.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kuongezeka kwa bajeti ya Tume, hususan bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo lakini bado fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazina uwiano mzuri zikilinganishwa na fedha za nje zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo hauridhishi kwani kati ya fedha zote za miradi ya maendeleo ni asilimia 25.3 tu ndio fedha za ndani na asilimia 74.7 ni fedha za nje. Hali hii inadhihirisha kuwa bado kuna utegemezi wa fedha za wafadhili kwa kiwango kikubwa katika kuratibu Masuala ya UKIMWI nchini. Hivyo, ni muhimu Serikali kutoa kipaumbele zaidi katika kutenga kiwango kikubwa cha fedha za ndani katika uratibu na utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI nchini.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – **Fungu 92**, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

**Mwenendo mdogo wa utoaji wa Fedha za ndani za maendeleo zilizotengwa mwaka 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na kutolewa kwa kiwango kidogo cha fedha za ndani za maendeleo, kiwango cha asilimia 50 tu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji wa fedha zote za ndani zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Utegemezi mkubwa wa fedha za nje za Maendeleo kutoka kwa wafadhili**

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na kuwepo kwa utegemezi mkubwa wa fedha za nje kutoka kwa wafadhili katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

i) Iongeze kiwango cha fedha za ndani za maendeleo zinazotengwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI *(Aids Trust Fund)* ili kuhakikisha afua za UKIMWI zinatekelezwa bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi; na

ii) Itekeleze kikamilifu mpango wa uendelevu wa mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini *(HIV Response Sustainability Roadmap)* ili kupata rasilimali endelevu za ndani katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI bila kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ya nchi.

**Mwenendo usioridhisha wa huduma ya upimaji wa Virusi vya UKIMWI (VVU)**

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mwenendo usioridhisha wa huduma ya upimaji wa Virusi vya UKIMWI (VVU), Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupima ili kujua hali zao za maambukizi.

**Uzalishaji wa Dawa za Kufubaza Virusi vya UKIMWI na Dawa Kinga za Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kuwa Serikali ina utaratibu wa kuagiza dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI (VVU) na dawa

kinga za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kutoka nje ya nchi, utaratibu huo unasababisha nchi kutumia gharama kubwa kuagiza bidhaa hizo. Hivyo ili kupunguza gharama na kuhakikisha kunawepo na uhakika wa upatikanaji wa dawa, Kamati inaishauri Serikali iwekeze kwenye viwanda vya ndani kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya kuzalisha dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI na dawa kinga za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

**Uundaji na Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufikia malengo ya kidunia ya kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030, zinahitajika jitihada madhubuti kwa kila sekta na taasisi za umma nchini kushiriki mapambano dhidi ya UKIMWI. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kila Sekta na taasisi za umma zinaunda na kutekeleza mpango mkakati wa kudhibiti UKIMWI.

**Utekelezaji wa afua za Virusi vya UKIMWI gerezani**

**Mheshimiwa Spika**, Afua za Virusi vya UKIMWI zinatekelezwa gerezani kwa lengo la kutoa huduma kwa WAVIU waliopo gerezani na kuzuia maambukizi ya VVU gerezani. Katika kuboresha na kuimarisha mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI gerezani, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuna upatikanaji wa uhakika wa dawa gerezani kwa ajili ya kutibu wafungwa na mahabusu wanapopatwa na maradhi.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, Namshukuru pia Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia

Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim James Yonazi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Dkt. Catherine Joachim na Watendaji wote wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka Mb, - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - Mjumbe
7. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Seif Salum Seif, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Agness Mathew Marwa, Mb - Mjumbe

19. Mhe. Jacquline Andrew Kainja, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**

9 Aprili, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, dakika 10.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante sana. Ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha

kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, naomba taarifa hii ya Kamati yote iingie kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge yani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuzingatia matakwa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya kwanza imetoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(c) Sehemu ya tatu ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

(e) Sehemu ya tano ni sehemu ya hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yapo katika Taarifa ya Bunge ambayo imeletwa kwako. Naomba niende kwenye uchambuzi wa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu iliidhinishiwa jumla ya bilioni 23.77 kwa ajili ya matumizi ya

kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.638 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 7.7 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 5.3 kwa ajili ya ruzuku ya mishahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi *(OSHA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilipokea jumla shilingi bilioni 14.76 sawa na 62% lakini pia shilingi bilioni 7.51 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 4.37 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 2.87 kwa ajili ya ruzuku ya mishahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida katika Fungu 65 unaonesha kwamba jumla ya shilingi bilioni 14.763 sawa na 62% ya bajeti imeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida na yamepokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* Fungu 15 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 6.76 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 2.86 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 3.44 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni 460.07 ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2025, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 3.65 sawa na 58.25% kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.37 ni mishahara, na shilingi bilioni 2.28 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi milioni 222.98 ni fedha kwa ajili ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha umeonekana katika jedwali namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ipo katika taarifa ya Kamati, kwa hiyo sitaisoma kwa sababu najua ipo katika taarifa hiyo. Sambamba na hilo, jumla ya miradi mitano imetekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu Fungu 65 na 15 Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo, nitasoma tu vichwa vya habari vya miradi ile.

(a) Mradi Na. 6205 Programu ya Kukuza Kazi za Staha *(Decent Work Country Program)*

(b) Mradi mwingine ambao uliyokuwepo ni Mradi wa 6581 Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini,

(c) Mradi mwingine ulikuwa ni Mradi wa Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu.

(d) Mradi mwingine ulikuwa ni Mradi Na. 4952 ambao ni mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo wa kieletroniki wa usimamizi na uendeshaji mashauri *(OCMS)*, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 460 kwa ajili ya kukamilisha usimikaji wa mfumo, lakini hadi kufikia Februari, 2025 Tume imepokea jumla ya Shilingi bilioni 222.982.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa Mfumo huu umefikia 92% kwa kiasi kikubwa mfumo upo tayari, lakini ni hatua chache zimebaki ili kukamilisha ikiwa ni pamoja na kurasimishwa kwa Kanuni za Uendeshaji wa Mfumo. Pia Kamati ilibaini kuwa licha ya mfumo huu kukamilishwa kwa kiasi kikubwa lakini bado haujaanza kutumika kutokana na kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya masuala madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa utekelezaji unaridhisha na kwa baadhi ya maeneo, ofisi inaendelea na utekelezaji wa ushauri huo wa Kamati kwa kuwa utekelezaji wake ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ambao haujazingatiwa ni pamoja na Serikali kuongeza bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili uweze kuwafikia vijana wengi. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti hii haijaongezwa kama Kamati ilivyoshauri. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha ili kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu itakayowezesha kuanzisha na kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya ukuzaji ujuzi nchini pia haijaongezewa bajeti kwa kuzingatia makubaliano baina ya sekta binafsi na Serikali ambapo moja ya tatu ya tozo ya *SDL* inatakiwa itumike kugharamia programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali itenge moja ya tatu kama ilivyo kwenye makubaliano ili zielekezwe katika kuwaongezea ujuzi na kufikia lengo la kuongeza ujuzi kwa vijana laki 681,000 wanaotakiwa kupata mafunzo haya katika kipindi cha miaka mitano ambapo hadi kufika Februari, 2025 ni vijana 87,749 tu wamepatiwa ujuzi kupitia programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeonyesha pale kwenye suala zima la maduhuli, kutokana na uchambuzi huu Kamati imebaini yafuatayo:-

a) Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yameongezeka kwa shilingi bilioni 9.5 sawa na ongezeko la 23.46%.

b) Makusanyo ya maduhuli kutoka kwenye chanzo cha ada za vibali vya ajira kwa wageni kimeongezeka kwa 23.68% ada za wakala binafsi wa huduma za ajira kwa 64.3% na ada za maombi ya kufanya kazi nje ya nchi kwa 16.77%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa ongezeko hili la makisio ya maduhuli liendane na kuweka mikakati thabiti ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi na kuweka mfumo madhubuti wa kukusanya

mapato yatokanayo na ujira kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ili kuweza kuongeza mapato yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Fungu 65 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 30.25.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nenda kwenye maoni muda wako umekwisha. Maoni na ushauri.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maoni na ushauri wa Kamati, maoni na ushauri wa Kamati ya ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(a) Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo ya Mapato kwa Fungu 65 kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato, siyo wa kuridhisha hasa katika vyanzo vya ada za wakala binafsi wa huduma za ajira, ada za maombi ya kufanya kazi nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuwaunganisha Watanzania na ajira za nje ya nchi ili kuongeza ajira nyingi na kuongeza mapato ya nchi.

(b) Kukosekana kwa mfumo wa kukusanya mapato kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi, kunapelekea nchi kukosa mapato. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufanya maboresho ya mfumo wa huduma za ajira *(Employment Services Management Information System - ESMIS)* ili kuwezesha kubadilishana taarifa mbalimbali.

(c) Mradi Na. 4954 Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu, Kamati ilibaini kuwa katika mwaka wa fedha mradi huu ulitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 1.15 ili kutekeleza kazi

zilizopangwa. Hata hivyo hadi Kamati inapokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Fungu 65 fedha hizi zilikuwa hazijatolewa.

(d) Mradi Na. 4952, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana utolewaji wa fedha kwa ajili ya mfuko huu siyo wa kuridhisha, kwani katika kipindi cha miaka Sita Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni moja tu badala ya shilingi bilioni 5.6 zilizokuwa zimetengwa kwa miaka yote sita, hivyo Kamati inashauri Serikali ilifanyie kazi jambo hili.

(e) Mradi Na. 6581 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini. Hali kadhalika Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa mgao wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii umekuwa ukishuka kila mwaka hivyo tunaishauri Serikali iweze kufanya yanayotakiwa.

(f) Serikali ihakikishe kuwa ujuzi unaopatikana katika programu ya uanagenzi haupotei ili Serikali ione namna ya kutoa vifaa/vitendea kazi kwa vijana wanaonufaika na programu hii.

(g) Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa vijana katika mradi huu haujulikani miongoni mwa Watanzania. Serikali ihakikishe inamrahisishia mwananchi kupata taarifa kuhusiana na mradi huu.

(h) Vyuo vinavyotoa mafunzo haya ya uanagenzi ni vichache ukilinganisha na uhitaji wa mafunzo haya kwa vijana hivyo vyuo vinatakiwa viongezwe zaidi.

(i) Maendeleo ya mradi wa kusimika mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu yani Fungu 15. Inatakiwa mfumo huu kukamilika, umekamilika kwa 92% lakini bado haujaanza kufanya kazi, tunashauri uweze kuanza kazi mapema.

(j) Kamati ilibaini kuwa mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu haufahamiki miongoni mwa wanufaika wengi, kwa hiyo, ni budi watu waweze kupewa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Naibu Waziri Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Mbunge kwa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Bi. Mary Ngelela Maganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**9 APRILI, 2025**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

### *(i) Msingi wa Uchambuzi wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kanuni ya 6 (5)(a) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7 (1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya ofisi hii. Aidha, Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge lako Tukufu liijadili hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu pamoja na Taarifa hii.

### *(ii) Mawanda ya Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inagusa mafungu mawili. **Fungu 65** ambalo ni Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na **Fungu 15** ambalo ni Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mafungu yote mawili tarehe 19,20 na 21 Machi 2025.

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika mambo makuu manne yafuatayo:-

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

***(i) Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli***


**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 40,500,000,000**.

Hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilikuwa imekusanya **Shilingi 29,594,331,225.88** sawa na **Asilimia 73** ya malengo yaliyokusudiwa. Vyanzo vya makusanyo hayo ni Ada za Vibali vya Ajira za Wageni **Shilingi 29,079,929,878.38** sawa na **asilimia 77**, Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira **Shilingi 79,500,000** sawa na **asilimia 46,** Ada za Maombi ya kufanya kazi nje ya Nchi **Shilingi 0,** Ada ya kuunganisha watafuta kazi nje ya nchi **Shilingi 434,871,347.50**. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika Jedwali Na. 1.

***JEDWALI NA. 1: FUNGU 65 - MAKADIRIO NA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025***

| **MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2024/2025** | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| Ada za Vibali vya ajira za Wageni | 37,980,505,600 | 29,079,929,878.38 | 77 |
| Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira | 174,000,000 | 79,500,000 | 46 |
| Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni | 1,000 | 30,000 | 300 |
| Pango la Mnara wa Simu | 1,000 | 0 | 0 |
| Ada za kuunganisha Watafuta kazi nje ya Nchi | 600,000,000 | 434,871,347.50 | 72 |
| Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi | 1,725,000,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **40,500,000,000.** | **29,594,331,225.88** | **73.07** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2025/2026 fungu 65***




**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo;-

(a) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 29,594,331,225.88** sawa na **asilimia 73.07** ya makusanyo yote yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo ni pango la mnara na Ada ya maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi havijakusanya kabisa na chanzo kimoja kimekusanya chini ya aslimia 50.

**Mhesimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa mwaka huu kwenye baadhi ya vyanzo vya makusanyo si wa kuridhisha. Mathalani, Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira imekusanya kwa asilimia 46 na Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi hajakukusanya kabisa. Kamati imeona kuwa sababu za makusanyo kuwa madogo kwenye baadhi ya vyanzo hivi ni kutokana na kasi ndogo ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira za nje ya nchi na kukosekana kwa mfumo wa kukusanya mapato yanayotokana na ujira kutoka kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi.

***(ii) Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida***


**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 23,776,408,010.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 10,638,868,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 7,798,238,676.00** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 5,339,301,334.00** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilipokea jumla **Shilingi 14,763,572,470.05** sawa na **asilimia 62** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 7,514,448,127.07** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 4,374,690,342.08** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 2,874,434,000.00** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2**

***JEDWALI NA. 2: FUNGU 65 - MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025***

| **MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2024/2025** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | **7,798,238,676.00** | **4,374,690,342.08** | 71 |
| Oc | **10,638,868,000.00** | **7,514,448,127.07** | 56 |
| Ruzuku ya mshahara (OSHA) | **5,339,301,334.00** | **2,874,434,000.00** | 54 |
| **Jumla** | **23,776,408,010.00** | **14,763,572,470.05** | **62** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 65***




**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida katika Fungu 65 unaonesha kwamba jumla ya **Shilingi 14,763,572,470.05** sawa na **asilimia 62** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kwaida imepokelewa.


**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) **Fungu 15** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6,769,053,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 2,861,776,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 3,447,200,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 460,077,000** ni fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2025, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 3,657,112,827.72** sawa na **asilimia 58.25.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,373,059,355.46** ni mishahara, na **Shilingi 2,284,053,472.26** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi 222,982,000** ni fedha kwaajili ya maendeleo**.** Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2025 ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na.3

***JEDWALI NA. 3: FUNGU 15 MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025***

| MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2024/2025** | **Fedha zilizopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | **2,861,776,000** | **1,373,059,355.46** | 47.98 |
| Oc | **3,447,200,000** | **2,284,053,472.26** | 66.26 |
| Maendeleo | **460,077,000** | **222,982,000** | 48.46 |
| Jumla | **6,769,053,000** | **3,657,112,827.72** | 58.25 |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 15*




**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi kuhusu mwenendo wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu 65 na 15 Kamati imebaini yafuatayo;

(a) Mapokezi ya fedha za Matumizi ya kawaida kwa **Fungu 65** ni **Shilingi 14,763,572,470.05** sawa na **asilimia 62** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

(b) **Fungu 15** limepokea fedha ya matumizi ya kawaida kiasi cha **Shilingi 3,657,112,827.72** sawa na **asilimia 58.25** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida si

wa kuridhisha kwani upo chini ya asilimia 75. Hivyo ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe kiasi cha fedha kilichosalia kwa mafungu yote mawili kabla ya tarehe 30 Juni ili waweze kutekeleza majukumu yao kama yalivyopangwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

***(iii) Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi wa Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilitengewa jumla ya **Shilingi 14,491,387,990** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,629,011,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,862,376,990** ni fedha za nje.


**Mheshiniwa Spika,** hadi kufikia Februari 2025 Ofisi imepokea kiasi cha **Shilingi 10,280,325,616.00**, sawa na **asilimia 70.9** ya fedha zote. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 9,629,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 651,325,616** ni fedha za Nje. Mgawanyo wa fedha hizo umeainishwa katika Jedwali Na. 4.

**JEDWALI NA. 4: FUNGU 65 - MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2024/2025**

| MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2024/2025 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Namba na jina la mradi** | **Bajeti iliyotengwa 2024/2025** | | **Mapokezi ya fedha hadi kufikia marchi 2024** | | **Asilimia ya mapokezi** |
| | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | **fedha za ndani** | **fedha za nje** | |
| Na. 6205: Programu ya Kukuza Kazi za Staha Nchini | 0.00 | 1,862,376,990 | | 651,325,616 | 34.9 |
| Na. 6581: Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 10,812,374,311 | 0 | 9,629,000,000 | 0 | 89.05 |
| Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu | 1,159,0000,000 | | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 657,252,868 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla Kuu** | **14,491,387,990** | | **10,280,325,616** | **651,325,616** | **70.09** |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 65*




**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo;

(a) Kwa ujumla mapokezi ya fedha za maendeleo kwa Fungu 65 ni **asilimia 70.09**. Mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichotarajiwa ambapo ilipokea **asilimia 34.9** ya makadirio. Hali hii ya mapokezi ya fedha za nje si wa kuridhisha na kwa kiasi kikubwa yameathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa;

(b) **Fungu 15**-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) inatekeleza mradi mmoja wa mfumo wa Usimamizi wa Uendeshaji Mashauri (ECMS). Fungu hili limepokea **asilimia 48.46** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo.

(c) Kamati pia imebaini kwamba, **Fungu 65** ilitengewa **Shilingi 1,159,0000,000** kwa ajili ya Mfuko wa watu Wenye Ulemavu na **Shilingi 657,252,868** kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 19 Machi 2025 hakuna fedha

yoyote iliyopokelewa na Ofisi hiyo kutekeleza miradi husika. Ni maoni ya Kamati kuwa mwenendo huu wa mapokezi ya fedha hauleti tija na unaweza kuathiri utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya miradi **mitano** ilitekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Fungu 65 na 15. Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

***Mradi Na. 6205 Programu ya Kukuza Kazi za Staha* (Decent Work Country Program)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu kukuza na kujenga stadi za Maisha kwa vijana kupitia programu ya kazi za staha. Taarifa zinaonyesha kuwa, fedha zinazotumika kutekeleza mradi huu ni fedha za nje. Jumla ya **Shilingi 1,862,376,990** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia Februari, 2025 mradi ulipokea **Shilingi** 651,325,616

Aidha Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kupitia ufadhili wa UNFPA ilitoa vifaa mtaji wenye thamani ya **Shilingi 91,000,000** kwa vikundi vya uzalishajimali 36 vyenye idadi ya vijana 16. Vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na Cherehani za kawaida, Cherehani za kudalizi, cherehani za *overlocking,* mashine za kutotoreshea vifaranga, mashine za kukoboa na kusaga mahindi, mixer za sementi na mchanga, *moter*, mashine za kufyatua matofari, jiko la mtungi mkubwa, Kompyuta, mashine za welding na mashine ya kufuma sweta. Kazi nyingine iliyofanyika ni kuandaa na kuzindua Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vija na (2007) Toleo la Mwaka 2024 na Kuzindua Mfumo wa Uratibu wa Kinga ya Jamii nchini.

***Mradi Na. 6581 Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini***

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 10,812,374,311**. Hadi kufikia Februari, 2025 programu hii ilikuwa imepokea **Shilingi 9,629,000,000.** Kupitia Programu hii Serikali imeweza kufadhili mafunzo ya uanagenzi kwa vijana 8,000 katika Vyuo 52 vya mafunzo ya ufundi stadi katika

fani za ubunifu wa Mitindo na ushonaji nguo,Ufundi Bomba, Uashi, Uselemala, Uchomeleaji na Uungaji Vyuma, Upakaji Rangi na Maandishi ya Alama, Utengenezaji wa Vipuri vya Mitambo, Ufundi Magari na Mitambo, Umeme wa Majumbani na Viwandani, TEHAMA, Umeme wa Magari, Huduma za Hoteli na Utalii, Ukataji Madini ya Vito na Kilimo. Mafunzo yaliyotolewa ni ya muda mfupi, wa kati na mrefu kulingana na aina ya ujuzi ambao hutolewa kwa watu wa ngazi mbalimbali za elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika chuo cha Don Bosco Vocational Training Centre-Dar Es Salaam ambapo jumla ya vijana 210 wanapata mafunzo ya uanagenzi katika chuo hicho. Lengo la ziara ilikuwa ni kuona utekelezaji wa mradi huu na kubainisha mafanikio na changamoto za utekelezaji wake. Udadisi wa Kamati ulidhihirisha kuwa vijana wanaonufaika na mafunzo haya hupata ujuzi wenye manufaa, lakini inakuwa vigumu kwa ujuzi huo kuwasaidia katika Maisha yao. Hali hiyo inatokana na ukosefu wa mitaji ya kupata vifaa na vitendea kazi vya kuweza kujiajiri na kuajiri wengine. Hali hiyo isipofanyiwa kazi, programu ya kukuza ujuzi nchini haitakuwa na tija.

**Mheshimwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa makusanyo ya fedha za tozo ya maendeleo ya ujuzi kwa kipindi cha miaka 8 (2016/2017 hadi 2023/2024) na kubaini kuwa fedha zinazotengwa kwaajili ya kukuza ujuzi kwa sekta binafsi ni chini ya kiwango kinachotakiwa kisheria cha moja ya tatu. Mathalani katika Mwaka 2016/2017 kiasi kilichokusanywa ni **Shilingi 280,119,900,000,** mgao wa 1/3 **ni Shilingi 93,372,970,000** lakini kiasi kilichoidhinishwa **ni Shilingi 15,000,000,000 tu,** Mwaka 2022/2023 kiasi kilichokusanywa ni **Shilingi 374,321,000,000** mgao wa 1/3 ni **Shilingi 124,773,700,000** lakini kiasi kilichoidhinishwa ni **Shilingi 9,000,000,000 na Mwaka 2023/2024** kiasi kilichokusanywa **ni Shilingi 358,924,100,000** mgao wa 1/3 ni **Shilingi 119,641,370,000** lakini kiasi kilichoidhinishwa **ni Shilingi 9.000.000.000.**

Hali hii imesababisha kushuka kwa idadi ya vijana wanaonufaika na programu hii kutoka wastani wa vijana **42,000** hadi kufikia **10,000** kwa mwaka kinyume na Mpango wa Taifa wa Meendeleo ambao unaeleza kuwa jumla ya vijana **681,000** walitakiwa

kupatiwa mafunzo kwa kipindi cha miaka 5, sawa na vijana **136.000** kwa mwaka.

**Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi huu ulitengewa kiasi cha **Shilingi 1,159,383,821** ili zitekeleze kazi zilizopangwa ikiwemo utoaji wa Ruzuku kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu**.**Hata hivyo hadi kufikia tarehe 19 Machi wakati Kamati inapokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Fungu 65 fedha hizi zilikuwa hazijatolewa na Serikali. Ni rai ya Kamati kuwa fedha hizi zitolewa kabla ya kuisha kwa mwaka huu wa fedha tarehe 30 Juni 2025**.**

***Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana***

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 657,252,868** kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya kupunguzwa kiasi cha fedha katika mwaka huu wa fedha lakini hadi kufikia tarehe 19 Machi, 2025 , hakuna fedha ya maendeleo iliyopokelewa katika mradi huu. Uchambuzi wa kamati unaonesha kuwa katika kipindi cha miaka sita Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** tu kati ya **Shilingi 5,657,252,868** zilizokuwa zimetengwa kwa miaka yote sita hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana na kusababaisha kushindwa kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Mathalani katika kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba 2023 hadi Machi 2025 jumla ya maombi 216 yenye thamani ya **Shilingi 7,800,000,000** yaliyowasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kutoka katika Halmashauri mbalimbali ikilinganishwa na fedha iliyokuwepo ambayo ni **shilingi 3,600,000,000 (**Revolving Fund)

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha katika mradi huu ili kuwawezesha vijana wengi kufanya shughuli za uzalishaji na hivyo kusaidia kupunguza ombwe la vijana wasio na ajira nchini.

***Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi na Uendeshaji Mashauri (OCMS)***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi 460,007,000** kwaajili ya kukamilisha usimikaji wa Mfumo huu, lakini hadi kufikia Februari 2025 Tume imepokea jumla ya **Shilingi 222,982,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa utekelezaji wa Mfumo huu umefikia **asilimia 92** kwa kiasi kikubwa Mfumo upo tayari lakini ni hatua chache zimebaki ili kukamilisha ikiwa ni pamoja na kurasimishwa kwa Kanuni za Uendeshaji wa Mfumo. Aidha kukamilika kwa Mfumo huu kutasaidia kuboresha utendaji kazi wa Tume katika kusuluhisha na kuamua migogoro kwa kupokea, kusajili, kupanga na kusikiliza migogoro ya kikazi kwa wakati. Pia utasaidia kusomana kwa Mfumo wa Tume na Mahakama Pamoja na Taasisi nyingine zenye maslahi na taarifa za migogoro ya kazi na kurahisha upatikanaji wa takwimu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa licha ya Mfumo huu kukamilisha kwa kiasi kikubwa lakini bado haujaanza kutumika kutokana na kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya masuala madogomadogo. Ni rai ya Kamati kuwa Tume ikamilishe mapema hatua zilizobaki ili Mfumo huu uanze kutumika na kuleta tija iliyokusudiwa.

***Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa utekelezaji unaridhisha na kwa baadhi ya maeneo Ofisi inaendelea na utekelezaji wa ushauri huo wa Kamati kwa kuwa utekelezaji wake ni endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** ushauri ambao haujazingatiwa ni pamoja na Serikali kuongeza Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili

uweze kuwafikia vijana wengi. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bajeti hii haijaongezwa kama Kamati ilivyoshauri. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha ili kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu itakayowezesha kuanzisha na kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji Ujuzi Nchini pia haijaongezewa bajeti kwa kuzingatia makubaliano baina ya Sekta Binafsi na Serikali ambapo moja ya tatu ya tozo ya SDL inatakiwa itumike kugharamia programu hii. Kamati inaendelea kusisistiza kuwa Serikali itenge moja ya tatu kama ilivyo kwenye makubaliano ili zielekezwe katika kuwaongezea ujuzi na kufikia lengo la kuongeza ujuzi kwa **Vijana 681,000** wanaotakiwa kupata mafunzo haya katika kipindi cha miaka mitano ambapo hadi kufika Februari 2025 ni **Vijana 87,749** tu wamepatiwa ujuzi kupitia Programu hii.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026


### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira, na Wenye Ulemavu, inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya Shilingi **50,000,000,000** ikilinganishwa na **Shilingi. 40,500,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Makadirio yameongezeka kwa **Shilingi 9,500,000,000** sawa na **asilimia 23.46** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika ada za maombi ya Vibali vya Kazi kwa Wageni, Malipo ya Usajili wa Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira nchini, Ada za maombi ya kufanya Kazi nje ya Nchi na kodi ya mnara wa mawasiliano. Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 65 unaonekana katika Jedwali Na.5 hapa chini.

***JEDWALI NA. 5: FUNGU 65 - ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/026***

| MAKADIRIO NA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **Maelezo** | **2024/2025 (Tsh.)** | **2025/2026 (Tsh.)** | **Asilimia/Pungufu au ongezeko %** |
| Ada za Vibali vya ajira za Wageni | 37,980,505,600 | 46,975,630,595 | 23.68 |
| Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira | 174,000,000 | 285,875,005 | 64.3 |
| Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni | 8,492,400 | 9,492,400 | 11.78 |
| Pango la Mnara wa Simu | 12,000,000 | 14,000,000 | 16.67 |
| Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi. | 2,325,000,000 | 2,715,000,000 | 16.77 |
| **Jumla** | **40,500,000,000** | **50,000,000,000** | **23.46** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2025/2026 Fungu 65.***




**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo;

(a) Makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa **Shilingi 9,500,000,000** sawa na ongezeko la **asilimia 23.46**

(b) Makusanyo ya maduhuli kutoka kwenye chanzo cha ada za Vibali vya Ajira kwa Wageni kimeongezeka kwa **asilimia 23.68**, Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira kwa **asilimia 64.3** na Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi kwa **asilimia 16.77.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa ongezeko hili la makisio ya maduhuli liendane na kuweka mikakati thabiti ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi na kuweka mfumo madhubuti wa kukusanya mapato yatokanayo na ujira kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ili kuweza kuongeza mapato yaliyokusudiwa.

### 3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida


**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu **Fungu 65** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 30,251,309,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shlingi 8,103,911,000** ni mishahara, **Shilingi 7,030,030,000** ruzuku ya mishahara (OSHA) na **Shlingi 15,117,368,000** ni matumizi mengineyo (OC). Kiasi hicho ni ongezeko la **a silimia 27.23**

ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo iliidhinishiwa **Shilingi 23,776,408,010.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 10,638,868,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 7,798,238,676** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 5,339,301,334** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi (OSHA) kama ilivyochanganuliwa katika **Jedwali Na. 6**

***JEDWALI NA. 6: FUNGU 65 - ULINGANISHO WA BAJETI KW KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026***

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 65 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2024/2025 (Tsh.)** | **2025/2026 (Tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (%)** |
| Mishahara | **7,798,238,676** | 8,103,911,000 | 305,672,324 | 26.8 |
| OC | **9,138,868,000** | 15,117,368,000 | 5,978,500,000 | 50 |
| Ruzuku (OSHA) | **5,339,301,324** | 7,030,030,000 | 1,690,728.676 | 48.2 |
| **Jumla** | **23,776,408,000** | **30,251,309,000** | **6,474,901,000** | **27.23** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti 2024/2025 Fungu 65***





**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **Fungu 15** imekadiriwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,740,847,000** sawa na ongezeko la **asilimia 14.36** Ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka

2024/2025. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 3,151,421,000** ni kwa ajili ya Mishahara sawa na ongezeko la **asilimia 10.13** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 4,313,380,000** sawa na ongezeko la **asilimia 50.72** na **Shilingi 276,046,000** kwa ajili ya Maendeleo sawa na upungufu wa **asilimia 40.00.** Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa Mwaka 2025/2026 ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.7**

***JEDWALI NA. 7: FUNGU 15 - ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA***

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 15 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2024/2025 (Tsh.)** | **2025/2026 (Tsh.)** | **Ongezeko/pungufu (tsh.)** | **Ongezek/ pungufu (%)** |
| Mishahara | 2,861,776,000 | 3,151,421,000 | 289,645,000 | 10.13 |
| OC | 2,861,776,000 | 4,313,380,000 | 1,451,604,000 | 50.72 |
| Maendeleo | 460,077,000 | 76,046,000 | 184,031,000 | 40.00 |
| **Jumla** | **6,769,053,000** | **7,740,847,000** | **971,794,000** | 14.36 |

***Chanzo. Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 15***




**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo;

(a) **Fungu 65** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 27.23** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha.

(b) **Fungu 15** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 14.36** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, moja ya sababu ya ongezeko hili la **asilimia 27.23** katika Fungu 65 ni kutokana na maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni matumaini ya Kamati kuwa fedha hizo zitatolewa kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.


**3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, (Fungu 65) imetengewa jumla ya **Shilingi 13,322,106,000** sawa na punguzo la **asilimia 8.06** Ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2024/2025 kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,812,374,000** sawa na ongezeko la **asilimia 1.46** ni fedha za ndani, na **Shilingi 509,732,000** sawa na punguzo la **asilimia 72.63** ni fedha za nje. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 8.**

**JEDWALI NA. 8: FUNGU 65 - ULINGANISHO WA BAJETI YA FEDHA ZA *MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026***

| **ULINGANISHO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2024/2025 na 2025/2026** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **NAMBA NA JINA LA MRADI** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025** | | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026** | | **Ongezeko au Pungufu (%)** |
| | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | |
| Na. 6205: Programu ya Kukuza Kazi za Staha Nchini | 0 | 1,862,376,990 | 0 | 509,732,000 | 72.63 |
| Na. 6581: Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 10,812,374,311 | 0 | 10,812.374,311 | 0 | 0 |
| Na.4954 Mfuko wa Watu wenye Ulemavu | 1,159,000,000 | 0 | 1,000,000,000 | | 13,72 |
| Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 657,252,868 | 0 | 1,000,000,000 | 0 | 52.15 |
| **Jumla Kuu** | **12,629,011,000** | **1,402,474,504** | **12,812,374,000** | 509,732,000 | 8.06 |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2024/2025 Fungu 65*




**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa

a) Bajeti ya fedha za Maendeleo katika Mwaka wa **Fedha 2025/2026 zimepungua kwa** Shilingi **1,169,281,990** sawa na **asilimia 8.06** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha.

b) Fedha za Programu a Kukuza Staha za Kazi zimepungua kwa **Shilingi 13,592,742,504** sawa na **asilimia 72.63** ambapo mradi huu ulikuwa unategemea fedha za Nje pekee. Kwa Upande Mwingine fedha za miradi ya Maendeleo kwa Fungu 15 zimepungua kwa **Shilingi 184,031,000** sawa na **asilimia 40.00** Jambo litaloathiri ukamilishaji wa usimikaji wa mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za maendeleo ili Ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo:

i) Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo ya Mapato kwa **Fungu 65** kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato si wa kuridhisha. Hasa katika vyanzo vya Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira, Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuwaunganisha Watanzania na ajira za Nje ya Nchi ili kuongeza ajira nyingi na kuongeza mapato ya Nchi.

ii) Kukosekana kwa Mfumo wa kukusanya mapato kwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi kunapelekea nchi kukosa mapato. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kufanya maboresho ya mfumo wa huduma za ajira (Employment Services Management Information System-ESMIS) ili kuwezesha kubadilishana taarifa mbalimbali zikiwemo za kibenki ili kurahishishisha upatikananji wa takwimu za mapato yanayorejeshwa na Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi.

iii) Katika **Mradi Na.4954 Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu,** Kamati ilibaini kuwa Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi huu ulitengewa kiasi cha **Shilingi 1,159,383,821** ili kutekeleza kazi zilizopangwa ikiwemo utoaji wa Ruzuku kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu**.**Hata hivyo hadi kufikia tarehe 19 Machi, 2025 wakati Kamati inapokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Fungu 65 fedha hizi zilikuwa hazijatolewa na Serikali. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizi kwa wakati kabla Mwaka huu wa Fedha haujaisha ili kuweza kutekeleza majukumu yaliyopangwa.

iv) Katika **Mradi Na. 4952, Mfuko wa Maendeleo wa Vijana** utolewaji wa fedha kwa ajili ya mfuko huu si wa kuridhisha, kwani katika kipindi cha miaka Sita Serikali imetoa kiasi cha Shilingi 1,000,000,000 tu kati ya Shilingi 5,657,252,868 zilizokuwa zimetengwa kwa miaka yote sita hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya mkopo kwa vijana na kusababisha kushindwa kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha hizi kila mwaka na kwa wakati na kuongeza kiasi cha mtaji wa mfuko huu ili kuongeza idadi ya vijana wanaopata

mkopo kupitia mfuko huu ili waweze kupata mtaji wa kuanzisha shughuli za uchumi.

v) **Mradi Na. 6581 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini**. Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa mgao wa fedha kwaajili ya utekelezaji wa programu hii umekuwa ukishuka kila mwaka katika kipindi cha miaka nane mfululizo kinyume na makubaliano ya matumizi ya michango wanayotozwa waajiri ya kukuza ujuzi (Skills and Development Levy-SDL). Hali hii imesababisha kushuka kwa idadi ya vijana wanaonufaika na programu kwa mwaka. Kamati inashauri Serikali kutenga theruthi moja kama yalivyo makubaliano baina ya Serikali na Sekta Binafsi ili fedha hizo zitumike kufikia lengo la vijana **681,000** kama ilivyoishinishwa kwenye Mpango wa Miaka mitano ifikapio 2025. Aidha Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Programu ya Kukuza Ujuzi zielelekwe zaidi kwenye kuwanufaisha vijana moja kwa moja

vi) Serikali ihakikishe kuwa ujuzi unaopatikana katika programu ya uanagenzi haupotei. Serikali ione namna ya kutoa vifaa/ vitendea kazi kwa vijana wanaonufaika na programu mara baada ya kumaliza ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ione namna ambayo mikopo itokanayo na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana inawanufaisha vijana ambao tayari wana mafunzo mbalimbali yanayotolewa na programu hii.

vii) Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa vijana katika mradi huu bado haujulikani miongoni mwa Watanzania. Serikali ihakikishe inamrahisishia mwananchi kupata taarifa kuhusu programu hii ili kuwezesha vijana wengi kunufaika na fursa hii.

viii) Vyuo vinavyotoa mafunzo haya ya Uanagenzi ni vichache ukilinganisha na uhitaji wa mafunzo haya kwa vijana hivyo kushindwa kuwafikia vijana wengi. Ni vema Serikali ikaongeza idadi ya vyuo vinavyotoa mafunzo haya hadi katika ngazi ya Wilaya ili kuwafikia wanafufaika wengi zaidi kwenye maeneo yao wanayoishi.

ix) Maendeleo ya Mradi wa kusimika mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu katika **Fungu 15**. Kamati ilibaini kuwa licha ya Mfumo huu kukamilika kwa asilimia 92 lakini bado haujaanza kutumika kutokana na kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya masuala madogomadogo ikiwa ni pamoja na kurasimishwa kwa Kanuni za Uendeshaji wa Mfumo ambayo yanaweza kukamilika ndani ya muda mfupi. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mfumo huu na uanze kutumika haraka iwezekenavyo ili kurahisisha utoaji haki kwa waajiriwa kwenye masuala ya migogoro ya kazi.

x) Kamati ilibaini kuwa mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu haufahamiki miongoni mwa wanufaika wa Mfumo hasa walalamikaji wa masuala ya migogoro ya kikazi kutokana na ukweli kwamba wengi wao wanaelimu ya chini. Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa Waajiriwa ili waweze kujua namna ya kutumia mfumo huu na elimu hiyo pia itolewe kwa Wasuluhishi na Waamuzi ambao ndio watumiaji wakuu wa Mfumo huu.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb. – Mwenyekiti
2. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb.
6. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe. Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.

10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
12. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
13. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
16. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
17. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
18. Mhe. Neema Kachiki Lugangira, Mb.
19. Mhe. Khamis Yusufu Mussa, Mb
20. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe.Ridhiwan Jakaya Kikwete, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Naibu Waziri Mhe. Paschal Patrobass Katambi, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Bi. Mary Ngelela Maganga.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**Mhe. Fatma H. Toufiq, (Mb)**
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
**9 Aprili, 2025**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa namtafuta Mheshimiwa Kuchauka hapa, nafikiri amekwenda kusherekea barabara yake imefunguliwa na sasa inapitika.

Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali kwa hatua iliyochukua kurudisha mawasiliano kati ya maeneo haya mawili na kukuza uchumi na kuwafanya wananchi wa maeneo hayo waone umuhimu wa Serikali namna inavyowafanyia kazi. Tumpongeze na Waziri husika Mheshimiwa Ulega kwa kazi nzuri ya kuweka kambi na Waheshimiwa Mawaziri wote ambao walioshiriki naye kuhakikisha zoezi lile limekamilika.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba mwende mkasome Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ndiyo inagusa Wizara zote. Mkaitafakari, na hoja zenu zote mzilete Bungeni na zitajibiwa na Waheshimiwa Mawaziri.

Niwaombe Waheshimiwa Mawaziri mwepo Bungeni kipindi chote, mweze kusikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge na mzijibu kwa ukamilifu ili nao wapeleke taarifa nzuri za utendaji mzuri wa Serikali kwa wananchi wetu katika maeneo yetu nchini.

Naomba sana Waheshimiwa Mawaziri, ninyi ndio wataalamu wetu na ninyi ndio mpo na Mheshimiwa Rais mje kutoa majibu sahihi, mazuri ya kuwapa imani wananchi kuwa nchi inakwenda vizuri na *In Shaa Allah* tutafanikiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.25 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 10 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*